BUNGE LA TANZANIA

_____

MAJADILIANO YA BUNGE

_____

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Nane - Tarehe 20 Juni, 2003

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza naomba nitoe taarifa kwamba ule Muswada wa Sheria ya Fedha, *The Finance Bill* unaoendana na Bajeti tumeshauweka kwenye *pigeon hole* ya kila Mbunge, mnaweza kuanza kuusoma sasa. Lakini utasomwa Mara ya Kwanza hapa Bungeni siku ya Jumatatu, halafu siku hiyo hiyo nitaupeleka kwenye Kamati inayohusika ili waanze kuuchambua.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 70

Sekta Binafsi

MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH aliuliza:-

Kwa kuwa sekta binafsi ndiyo mhimili wa uchumi wa Taifa letu na ndiyo inayotujengea uwezo wa ushindani wa kiuchumi wa soko. Je, Serikali ina mipango gani ya kujenga uwezo wa kudhibiti ili kuweza kulinda walaji na kuzuia maslahi ya Taifa yasiathirike?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mbunge wa Kilosa, kuwa ni kweli kwamba Serikali imedhamiria kabisa kuifanya Sekta Binafsi iwe ndiyo mhimili wa uchumi wa Taifa letu na kwa maana hiyo, iwe ndiyo sekta inayotegemewa kutujengea uwezo wa ushindani wa uchumi wa soko.

Mheshimiwa Spika, katika mfumo wa kujenga uchumi wa soko, majukumu ya msingi ya Serikali ni kuweka mazingira bora, kuhakikisha kwamba unakuwepo ushindani wa haki baina ya washiriki wa ndani na kati ya washiriki wa ndani na wa nje na wakati huo huo, kuhakikisha kwamba maslahi na afya za walaji hazidhuriki kutokana na uhafifu wa bidhaa zinazozalishwa ndani au kuingizwa kutoka nje.

Aidha, watumiaji wa huduma na bidhaa zinazozalishwa au kuingizwa katika soko kutoka nje, wanahitaji kulindwa kutokana na kutozwa bei au gharama za juu sana. Kwa mtazamo huo, uanzishwaji wa *Competition Commission* pamoja na *Regulatory Authorities* una lengo la kuboresha ushindani, kuboresha ubora wa viwango vya bidhaa na huduma na kulinda walaji.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na umuhimu wa kuwa na ushindani wa haki pamoja na kulinda walaji ndiyo maana Serikali katika nyakati mbalimbali imekuwa ikiunda taasisi za kudhibiti ushindani na kusimamia ubora wa bidhaa na huduma kwa lengo la kulinda walaji. Taasisi zilizoundwa kwa lengo la kulinda afya za walaji ni pamoja na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, *National Food Control Commission* na taasisi ya kudhibiti ubora wa bidhaa Tanzania. Aidha, katika siku za hivi karibuni taasisi na

mamlaka kadhaa zimeundwa kwa lengo la kudhibiti ushindani na ubora wa huduma zitolewazo na wawekezaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi nchini. Taasisi na Mamlaka hizo ni kama ifuatavyo:-

Mamlaka ya Kudhitibi Sekta ya Nishati na Maji, Mamlaka ya Kudhibiti Usafiri wa nchi kavu na majini, Mamlaka ya kudhibiti usafiri wa anga, Kamisheni ya kudhibiti upashanaji habari na matangazo, Mahakama ya mwenendo wa haki katika biashara na Mamlaka ya kudhibiti mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunda mamlaka na taasisi nilizozitaja hapo juu kwa lengo la kuimarisha ushindani wa haki na kulinda mlaji, Serikali vile vile inaendeleza mipango ya kuimarisha maabara za uchunguzi wa kemikali na vimelea haribifu itakayokidhi viwango vya Kimataifa kama ule unaojengwa huko Mwanza kwa ajili ya biashara ya minofu ya samaki.

Aidha, Serikali vile vile inakusudia kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni, hasa zile zilizopitwa na wakati kwa lengo la kuimarisha udhibiti, kuweka mazingira ya biashara na uwekezaji chini ya mpango maalumu wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Ni mataumini ya Serikali kwamba baada ya kuweka mazingira bora ya ushindani pamoja na kumlinda mlaji, uchumi wa soko utaendeshwa kwa mfumo na utaratibu ulio bora zaidi na unaojali afya na maslahi ya mlaji kwa uju mla.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Katika kujenga uchumi wa nchi, sarafu yetu ni muhimu iwe na nguvu katika soko kulinganisha na fedha za Kimataifa. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba shilingi ya Tanzania haitetereki katika soko la Biashara? Ahsante. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, njia mojawapo madhubuti na ya kuaminika ya kuongeza thamani ya sarafu yetu katika soko, ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa tunazouza nje. *(Makofi)*

Na. 71

Ujenzi wa Barabara ya Jiji la Mwanza

MHE. STEPHEN M. KAZI aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa barabara za Jiji la Mwanza unaofadhiliwa na Nchi za Umoja wa Ulaya unaendelea; na kwa kuwa kati ya barabara zinazojengwa baadhi yake ziko chini ya Serikali Kuu na nyingine ziko chini ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza na zina urefu wa km 54 kwa ujumla wake; na kwa kuwa endapo mradi utakamilika bado zipo barabara zitakazobaki bila kujengwa kwenye Jiji la Mwanza, kutokana na kwamba hazimo ndani ya mradi huo kama vile Nkurumah, *Mission,* Karuta, Mtakuja, Uvinza, Sukuma, Miti Mirefu, *Liberty,* Unguja, Mkanyenye na zingine nyingi kwenye maeneo ya Isamilo, Kitangiri, *Capri Point,* Nyamanoro, Kirumba, Pasiansi, Nyegezi, Nyakato, Igoma na kadhalika.

Je, Serikali Kuu ina utaratibu gani wa ujenzi wa barabara za Jiji la Mwanza nilizozitaja ikizingatiwa kuwa Halmashauri ya Mwanza haina uwezo kifedha?

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi na ukarabati wa Baraza za Mkoa wa Mwanza, unahusisha ujenzi na ukarabati wa Barabara ya Mwanza Nyanguge yenye jumla ya km 34.58, Barabara ya Mwanza Mjini km 12.08

Vile vile barabara zifuatazo za Mwanza Mjini hadi Uwanja wa Ndege km 9.08 na barabara zifuatazo za Mwanza Mjini ambazo zina jumla ya km 12.08, barabara hizi ni barabara ya Balewa km 0.94, Bugando km 1.48, Kenyatta km 3.04, Machemba km 0.45, Miti Mirefu km 0.32, *Nasser Drive* km 1.9, Penda km 0.94, Rufiji km 0.6, Rwegasore km 0.7 na *Uhuru Road* km 1.71 na hivyo kuwa na jumla ya km 55.74 zinazojengwa chini ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zinajengwa na kukarabatiwa kwa kiwango cha lami na zinagharamiwa na msaada kutoka Jumuiya ya Nchi za Ulaya na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kueleza kuwa, Wizara yangu haina mpango wowote wa kuziingiza barabara mpya zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge kwenye mpango huu unaoendelea.

Barabara hizi ziko ndani ya Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza, hivyo ni jukumu la Jiji la Mwanza kupanga mipango yake ni kwa namna gani barabara hizo zitakarabatiwa. Hata hivyo, kutokana na ahadi ambayo Serikali iliitoa mwezi Aprili, 2003 ya kuchangia fedha iwapo Halmashauri husika itatoa mchango wake pia, kuanzia mwaka wa fedha 2003/04, Serikali Kuu kupitia Mfuko wa Barabara itatoa shilingi milioni 500/= zitakazojumuishwa na ahadi ya shilingi milioni 500/= zilizoahidiwa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa ajili ya kukarabati barabara zaidi za Jiji la Mwanza. *(Makofi)*

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na pia juhudi za Serikali ambazo zinajionyesha sasa kwenye ujenzi na kuuboresha Mji wa Mwanza, ningependa kuomba kwamba Mji wa Mwanza ni Mji ambao unakua sasa, una wakazi wengi, unahudumia maeneo mengi na unahitaji kuendana na ushindani wa miji mingine iliyo katika ufuko wa *Lake Victoria*.

Je, Serikali haioni kuwa kwa uzito wa shughuli hizi kuwaachia wakazi wa Mwanza peke yao kuwaachia itakuwa ni vigumu kukamilisha kazi hizi? *(Makofi)*

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa kwamba Jiji la Mwanza, lina majukumu mengi, ni Jiji ambalo linakua na ndiyo maana lina hadhi ya Jiji baada ya Jiji la Dar es Salaam. Lakini hata hivyo pamoja na kwamba ni Jiji, bado jukumu la Jiji ikiwa ni pamoja na uongozi wa Jiji bado unabaki pale pale.

Kwa kutambua hilo, ndiyo maana Serikali imetoa zaidi shilingi bilioni 21 ambazo zimehusika katika ukarabati wa barabara ambazo nimezitaja. Lakini pia katika ahadi ambayo ilitolewa na Serikali kwa mwaka huu ni kwamba Serikali itachangia shilingi bilioni moja ikiwa Halmashauri ya Jiji itatoa shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2003/04, tumeanza kutoa shilingi milioni 500. Kwa hiyo, ombi ambalo ningependa nitoe kwa Mheshimiwa Mbunge ni kwamba sasa jukumu la Jiji la Mwanza lihakikishe linakusanya mapato ya kutosha katika kuhakikisha kwamba linatengeneza barabara zake kama ambavyo majiji mengine yamekuwa yakifanya. *(Makofi)*

MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza kwamba kwa vile Jiji la Mwanza sasa ni Jiji na linajengewa barabara ambazo ni nzuri zenye hadhi na sasa hivi Mwanza kunakuwa

na msongamano mkubwa sana wa magari. Je, Waziri haoni kwamba kuna haja sasa ya ujenzi wa barabara za Mwanza ukaenda sambamba na taa za kuongozea magari, pamoja na taa za barabarani? *(Makofi)*

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali Kuu, lilikuwa ni kutengeneza barabara za Mwanza. Katika jibu la msingi tumeeleza kwamba jumla ya km 57 zimetengezwa kwa kiwango cha lami. Katika jukumu hili tumetengeneza pia hata baadhi ya barabara ambazo nimezitaja kama Miti Mirefu, Bugando na *Nasser Drive*, ambazo ziko chini ya Halmashauri ya Jiji, lakini bado zimetengenezwa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba na ningezidi kuomba kwamba Jiji la Mwanza, sasa lipange ni namna gani litaweka taa za kuongozea barabarani, namna gani litaweka *trafic right* na kadhalika katika ku-*make sure* kwamba Jiji la Mwanza linakuwa na hadhi kama Miji mingine. *(Makofi)*

Na. 72

Nyumba za Mashirika ya Umma Yaliyobinafsishwa

MHE. PONSIANO D. NYAMI (k.n.y. MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA) aliuliza:-

Kwa kuwa ni wajibu wa Serikali kuwapatia Mawaziri na Manaibu wake nyumba za kuishi:-

(a) Je, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita 1995 hadi 2000 ni Mawaziri na Manaibu wangapi walipangishiwa na Serikali nyumba za Makampuni ya Umma, Binafsi na ni Makampuni gani hayo na Serikali iligharimu fedha kiasi gani?

(b) Kwa kuwa baadhi ya Mawaziri walikuwa wakipangishwa katika nyumba hizo wakati ni za umma je, ni Mawaziri na Manaibu Waziri gani walionunua nyumba au majengo yaliyobinafsishwa tena kutoka kwa makampuni binafsi yaliyokuwa yameuziwa nyumba/majengo hayo?

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali ina wajibu wa kuwapatia nyumba watumishi wake wakiwemo Mawaziri, Manaibu Waziri na watumishi wengine wote wanaostahili kupatiwa nyumba.

Mheshimiwa Spika, kulingana na takwimu tulizonazo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita 1995 hadi 2000 Mawaziri 6 na Manaibu wanne walikuwa wanaishi kwenye nyumba za Mashirika ya Umma.

Kwa nyumba za *NHC* wahusika walikutwa wamekwishakuwa wapangaji hata kabla ya kuteuliwa kuwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri, hivyo Serikali iliamua waendelee kukaa kwenye nyumba hizo hadi nyumba za Serikali zitakapopatikana.

Aidha, kwa nyumba za Dodoma, kila Wizara inawajibika kuwatafutia Mawaziri na Manaibu Waziri, *Rest House* ambapo Wizara husika huwajibika kulipia na baadhi ya nyumba hizo ni nyumba 12 za Shirika la *NIC* ambazo zilikuwa zimepangishwa kwa Mawaziri na Manaibu Waziri pamoja na nyumba zilizokuwa za *NSSF* ambazo baadaye zilirudishwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano, 1995 hadi 2000, jumla ya shilingi 79,200,000/= zililipwa na Serikali kama gharama za pango kwa nyumba za Mashirika ya Umma.

Aidha, Wizara ya Ujenzi haina taarifa ya Mawaziri na Manaibu Waziri waliouziwa nyumba na Mashirika ya Umma au Makampuni binafsi.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili.

Kwa kuwa suala la kuteua Mawaziri na Manaibu Waziri, ni suala la kuendelea na kwamba wanalazimika kupewa nyumba za Serikali ili kupunguza gharama kwa Serikali kutokulipa fedha nyingi:-

(a) Je, hao watakaokuwa wameteuliwa mnategemea wataishi wapi wakati nyumba zote za Serikali mmekwishauza? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa katika uuzaji wa nyumba, Bunge halikujulishwa na wala halikuidhinisha kuuza nyumba hizo. Ni nani aliyeidhinisha na akaruhusu ninyi wenyewe muuziane hizo nyumba? *(Makofi)*

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza swali la msingi lilikuwa linazungumzia nyumba za Mashirika ya Umma walizokuwa wakiishi Mawaziri na Manaibu Waziri, katika mwaka 1995 hadi 2000. Suala la kuuza nyumba ambalo ameliuliza Mheshimiwa Mbunge linahusu Waraka namba 30 wa mwaka 1997 ambapo nyumba zake zimeanza kuuzwa kwenye mwaka wa 2002 hadi 2003. Kwa hiyo, kwa msingi huo unaona kabisa kwamba swali la msingi halikuzungumza hivyo.

Lakini kwa manufaa ya Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Ponsiano Nyami, ameuliza kwamba je, hawa Mawaziri na Manaibu Waziri watakaoteuliwa wataishi wapi?

Mheshimiwa Spika, nchi nzima in nyumba 6,000 tangu 1961 hadi leo kuna nyumba 6,000. Wafanyakazi wa Serikali wakiwemo Mawaziri na wengine wote ni 315,000, kwa hiyo, unaweza ukaona tangu tupate Uhuru hadi leo hapajawahi kutokea hata siku moja ambapo wafanyakazi wakiwemo na Mawaziri na kadhalika wameweza kupatiwa nyumba wote.

Kwa hiyo, jukumu lililopo kwa sasa hivi ni kwamba tumepanga kujenga nyumba zingine. Kuna baadhi ya nyumba zimeuzwa na katika mwaka huu ziliuzwa nyumba 3,000, hizo nyumba 3,000 zinauzwa lakini watakaouziwa hawatakiwi kuziuza hizo nyumba kwa zaidi ya miaka 25 na fedha zinazopatikana kutoka kwenye nyumba hizo ni zaidi ya shilingi 24 bilioni na nyumba zinajengwa nyingine. Kwa mwaka huu zimejengwa nyumba 173, mwaka unaokuja ni nyumba 500 zitajengwa.

Kwa hiyo, hao watakaoteuliwa wataishi kwenye nyumba zinazojengwa, lakini pia zimetengwa nyumba zingine 3,000, lakini zimetengwa tena nyumba 45 kwa ajili ya makazi ya Mawaziri watakaoteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, ameuliza huu uamuzi ulitolewa na nani. Uamuzi huu umetokana na sheria namba 30 ya mwaka 1997 ambayo ilianzisha *Executive Agency*. Kwa hiyo, kitengo cha nyumba chini ya *TBA* ni *agency* kwa hiyo, kinatakiwa kifanye kazi yake kutokana na sheria namba 30 ya mwaka 1997 ambayo imeamuliwa na Bunge. *(Makofi)*

Na. 73

Zana za Kilimo kwenye Kaya Binafsi

MHE. JOB Y. NDUGAI aliuliza:-

Kwa kuwa kutokana na matokeo ya takwimu zitokanazo na utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2000/2001 inaonyesha kwamba kiwango cha utumiaji wa zana bora za kilimo miongoni mwa kaya za vijijini ni kidogo kwa ukweli kwamba ni

asilimia 11 ya wakulima wanaomiliki majembe ya plau na karibu asilimia 0.2 wanaomiliki trekta. Je, Serikali ina mikakati gani ya kubadilisha hali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, kiwango cha utumiaji wa zana za kurahisisha kazi katika kilimo miongoni mwa kaya za vijijini ni cha chini sana. Sensa ya kilimo iliyofanyika mwaka wa 1994 ilionyesha kwamba asilimia 70 ya wakulima wadogo wanategemea jembe la mkono na asilimia 20 wanatumia wanyamakazi na asilimia 10 wanatumia matrekta. Sensa nyingine ya kilimo inatarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza muhimu ya kuchukua katika kubadilisha hali hiyo ni kupanua matumizi ya wanyamakazi katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003 kiasi cha shilingi milioni 287 kilitumika katika mpango wa kuendeleza kilimo cha wanyamakazi nchini kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, vituo 20 vya mafunzo ya wanyamakazi vilikarabatiwa ili viweze kutoa mafunzo kwa mabwana shamba na mabibi shamba na wakulima juu ya matumizi ya zana bora za kilimo. Mabwana shamba 520, kutoka katika Wilaya 50 za Mikoa 17 na wakulima 500 kutoka katika Wilaya 44 walipata mafunzo.

(b) Mwaka wa 2000 na 2002 Serikali ilipokea msaada wa matrekta madogo 170 kutoka Serikali ya Japan na 15 kutoka Serikali ya China na kuyasambaza Mikoani kwa ajili ya kuwauzia wakulima wadogo.

Aidha, Serikali imepunguza bei ya awali ya matrekta madogo kutoka shilingi milioni 4.4 hadi kufikia shilingi milioni 2.5 ili kuwawezesha wakulima wadogo wamudu kuyanunua. Vile vile Wizara imebuni utaratibu wa kuwakopesha wakulima matrekta hayo kwa masharti nafuu ambapo wakulima wanatakiwa kulipa nusu ya gharama ya mkopo kabla ya kuchukua trekta na nusu kulipwa ndani ya kipindi cha miaka miwili chini ya udhamini wa Halmashauri za Wilaya na Miji husika.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya 2003/2004, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha wanyamakazi na matrekta kwa kupitia mfuko wa bembejeo, watu binafsi,vikundi na mashirika yasiyokuwa ya Serikali watapata mikopo kwa ajili ya kununua matrekta mapya 20 na kukarabati yaliyokuwa mabovu 243. Aidha, Sekta binafsi itahamasishwa katika kuanzishwa na kueneza vituo vya kuboresha matrekta na zana nyingine za kilimo ili waweze kutoa huduma kwa wakulima wengi na kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi pia itahamasisha kuingiza nchini matrekta yaliyokarabatiwa ambayo bei yake ni nafuu ili kuwawezesha wakulima wengi kuyamudu kuyanunua.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba umiliki wa matrekta kwa wakulima wetu Tanzania ni mdogo sana kama ilivyoonyeshwa kwenye takwimu ambao ni asilimia 0.2 ya wakulima wa Tanzania.

Sasa swali langu la kwanza ni kwamba kwenye Hotuba Waziri, ameahidi kwamba Serikali itasaidia wakulima hawa kujinunulia zana za kilimo kwa kudhaminiwa na Serikali.

(a) Je, ahadi hii kwa upande wa mikopo ya matrekta Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima? *(Makofi)*

(b) Miaka ya nyuma kulikuwa na karakana za kilimo kwa mfano kule Kongwa, sehemu ya Mtanana, kuwasaidia wakulima kutengeneza matrekta yao; je, Serikali ina mpango wowote wa kufufua karakana hizo kama ilivyokuwa siku za nyuma ili kuendeleza kilimo? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Job Ndugai, kama ifuatavyo:-

Kwanza, swali linalohusu kudhamini wakulima, katika jibu langu la msingi nilieleza kuwa Halmashauri za Miji na za Vijijini zinawasaidia wakulima kuyapata hayo matrekta siyo tu yameteremshwa bei, lakini vile vile kuwasaidia kuyanunua kwa awamu mbili, nusu mwanzo na nusu baadaye. Huo ndiyo udhamini wenyewe na naomba hilo atusifu.

Pili, kuhusu karakana tunaamini shughuli zote siyo tu za kushughulikia ufundishaji wa kutumia maksai pamoja na karakana hizo zitashughulikiwa vilivyo.

MHE. STEPHEN M. KAHUMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa kigezo kimoja muhimu cha maendeleo ni kuona kizazi kipya kinabadili nyenzo za kufanyia kazi au kubadili kazi yenyewe. Kwa kuwa wakulima wa Tanzania, hata hawa wachache ambao wameanza kutumia wanyama kwa kilimo wamekwama vile vile kwa kutumia hawa wanyama hawajaendelezwa kubadili kama kuwatumia kwa palizi au kupanda. Wizara ina mpango gani wa kuwakwamua watu hao kutoka walipokwama miaka ya nyuma sana ili wabadili zana za kilimo na mtindo wa kufanya kazi? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu moja la Mheshimiwa Stephen Kahumbi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika hayo mafunzo niliyoyaeleza wakati nikisoma jibu langu la msingi, siyo kufundisha tu jinsi ya kuwatumia wanyamaka zi, vile vile walipewa vifaa na kuonyeshwa namna ya kutumia vifaa vya kupandia, kupalilia na kutengeneza matuta na kadhalika. Kwa hiyo, mafunzo yatahusu hayo yote na tunaendelea katika msimu wa fedha huu unaokuja.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, ameelekeza hapa kwamba Halmashauri zitasaidia katika kudhamini na kupatikana kwa matrekta hayo. Je, anaweza akanithibitishia kwamba maelekezo haya yametolewa kwa Wakurungezi wa Halmashauri za Wilaya ili tuweze kufuatilia? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ndiyo, maelekezo haya yamo kwa sababu katika kipindi cha mwaka huu unaoishia Juni 30, Kilimanjaro kumefanyika mafunzo na pia Kilimanjaro wamepata matrekta 11 kwa msimu huu. Tunatekeleza na tutaendeleza kutekeleza. *(Makofi)*

Mawasiliano ya Simu Kondoa

MHE. KHALID S. SURU alijibu:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kuweka mtambo wa simu wa kisasa na kuondoa simu za kukoroga mwaka 1997, lakini mpaka sasa bado ahadi hiyo haijashughulikiwa na kwa kuwa ahadi hiyo ilibainisha kuweka na kufunga simu za *STD* sambamba na zile za mkononi za *Celtel* au *Vodacom:-*

(a) Kwa kuwa wananchi wanataka kujua sababu ya kutotekelezwa kwa ahadi hiyo, je, kazi hiyo itaanza lini na kutarajiwa kukamilika?

(b) Je, kwa kuwa Miji ya Pahi, Kolo, Haubi, Masange, Kisese, Kingala, Busi, Kikore, Changaa, Thawi na Mnenia ilikuwa imeombwa na kukubaliwa ufungaji wa simu hizo pamoja na zile simu za mkononi ambazo Serikali iliahidi ziende sambamba na hizo zinaanza lini?

(c) Je, ahadi ya sasa itakuwa na ukweli wa kiwango gani cha asilimia dhidi ya ahadi ya zamani?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa maendeleo wa kampuni ya simu *TTCL* wa mwaka 2003, Mji wa Kondoa utapatiwa mtambo wa simu za kisasa wenye uwezo wa kuunganisha jumla ya wateja, 1000 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2003. Vijiji vya Pahi, Kolo, Haubi, Masange, Kisese, Kingala, Busi, Kikore, Changaa, Thawi na Mnenia vitafikiriwa kupewa huduma za simu za kisasa iwapo vitakidhi masharti ya kibiashara.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri katika swali langu la msingi.

Kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri, ameniwahi asubuhi kwamba tutakwenda naye Kondoa tarehe 26 Juni, 2003 na atarudi tarehe 27 Juni, 2003 kwa shughuli hii hii. Lakini nitakuwa na maswali mawili mepesi mepesi. *(Makofi/Kicheko)*

(a) Je, atakapokuwa Kondoa atakubali kukutana na wadau wote wa simu?

(b) Kwa kuwa Waziri ametambua tatizo hilo, je, atakuwa karibu kusimamia ili shughuli za simu ziweze kutekelezwa kwa haraka zaidi katika Wilaya ya Kondoa? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Khalid Suru, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni kweli na napenda nithibitishe kwamba Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, atafanya ziara ya kwenda Kondoa tarehe 26 na kurudi tarehe 27 Juni, 2003 na katika muda huo mkimpangia kukutana na wadau, yuko tayari kukutana nao. *(Makofi)*

Pili, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, si Mheshimiwa Waziri tu hata mimi na wote tunaoshughulikia suala la mawasiliano ya simu tuko tayari kuwa karibu kushughulikia kusimamia masuala ya simu Kondoa na kwingine kote kwa sababu ndiyo wajibu uliotuweka hapa.

MHE. ASHA A. NGEDE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na ahadi nyingi za Serikali ya CCM kwa wananchi wa Kondoa kuwawekea mitambo mipya ya kisasa ya simu; je, Waziri haoni agizo linafanya Vyama vya Upinzani kukimbia sana katika Wilaya ya Kondoa na kuwapa shida wagombea wao wakati wa uchaguzi? *(Kicheko/Makofi)*

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nikiwa Waziri ninayesimamia shughuli za Mawasiliano na Uchukuzi, nakwenda Kondoa wiki ijayo. Mojawapo ya shughuli nitakazofanya ni kusimamia utekelezaji wa ahadi za Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwezi kusema sababu ya pili, lakini kwa sababu umenisukuma, nitaisema nayo ni kwenda kuvuruga mikakati ya Kambi ya Upinzani. *(Kicheko/Makofi)*

Wananchi Kunyang'anywa Ardhi

MHE. PONSIANO D. NYAMI aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Kata ya Sintali, Kate na Kipande katika Vijiji vya Sintali, Nkana, Nkomanchindo, Ntalamila, Kalundi na Nkundi wamenyang'anywa ardhi yao na Ranchi za Kalambo na Nkundi:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuwarudishia na kuwagawia wananchi hao baadhi ya maeneo ya kulima ili wazalishe chakula na wasidhurike na njaa?

(b) Je, ni sahihi kwa Serikali kumjali zaidi Mwekezaji wa nje kuliko wananchi wake ambao wamebaki kuhangaika kupata ardhi kwenye eneo walilozaliwa ambayo ni makwao kikatiba?

(c) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kuwagawia wananchi wa Vijiji vilivyotajwa mashamba ya Kalambo na Nkundi Wilayani Nkasi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sio kweli kwamba Serikali iliwanyang'anya ardhi wananchi waliokuwa wakimiliki maeneo ya Ranchi za Kalambo na Nkundi. Mashamba hayo yalianzishwa baada ya kuwafidia wananchi waliokuwa wakiyamiliki mashamba hayo. Mpaka sasa Serikali haidaiwi na mwananchi yeyote kuhusu ardhi ya mashamba hayo. Kwa mantiki hiyo,
Serikali haiwajibiki kuwarudishia wananchi ardhi ya mashamba hayo ya Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali haijabinafsisha shamba lake lolote kwa mwekezaji wa nje. Shamba lililobinafsishwa ni la Nkundi na limebinafsishwa kwa mwekezaji mzalendo ajulikanaye kama *Sumbawanga Agricultural and Animal Food Company*, tangu mwezi Machi, 2003. Kwa hiyo, si kweli kwamba Serikali inajali zaidi wawekezaji toka nje kuliko wazawa kuhusu suala la ugawaji wa mashamba haya na sio sahihi kuona wananchi wa Kata au Wilaya nyingine kuonekana ni wageni katika sehemu yoyote hapa Tanzania. Tanzania ni ya wote. *(Makofi)*

Ranchi ya Kalambo yenye eneo la hekta 64,650 ipo kwenye utaratibu wa kugawanywa katika vipande vya hekta 20,000 kwa ajili ya Ranchi maalum chini ya Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* na hekta nyingine 44,650 kwenye Ranchi ndogo ndogo zenye ukubwa wa hekta 4,000 kila moja. Naamini wananchi wa maeneo hayo watajitokeza kugawiwa mashamba hayo kwa nia ya kufuga kibiashara punde utaratibu wa kuyagawa mashamba hayo utakapokamilika. Mkoa tayari umearifiwa juu ya utaratibu huu na utasimamiwa kwa ushirikiano wa Mkoa na Wilaya husika katika zoezi zima.

(c) Mheshimiwa Spika, shamba la Kalambo na mashamba mengine ya namna hiyo yaliyokwishatolewa uamuzi na Serikali yatagawanywa katika maeneo madogo madogo ya hekta 4,000 na kuyatoa kwa wafugaji wadogo wadogo ambao ni pamoja na wananchi wa meneo hayo na ambao watatakiwa kuendeleza ufugaji wa kibiashara. Hivyo, nawashauri wananchi wa Nkasi akiwemo Mheshimiwa Mbunge na maeneo ya jirani wavute subira kidogo ili utaratibu wa kuyagawa mashamba hayo ukamilike.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge asaidie kuwahamasisha wananchi wa Nkasi akiwemo Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ili waweze kupewa hayo mashamba na kuwekeza katika ufugaji wa kibiashara. Kwa vile eneo la hekta 4,000 ni kubwa, wananchi wanaweza kujiunga kama vikundi halali kisheria na kuomba eneo kwa shughuli ya ufugaji. Maeneo hayo hayataruhusiwa kutumika katika shughuli nyinginezo isipokuwa ufugaji.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu hayo, naomba kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali iliahidi kwa wananchi kwamba kabla mashamba hayo hayajaanza kubinafsishwa, itazingatia maombi ya wananchi kutokana na ardhi ilivyo finyu; ni kitu gani kilichoifanya Serikali hiyo hiyo ikawashirikisha wananchi katika shamba la Kalambo ili waweze kugawiwa? Lakini ni kitu gani pia kilichofanya Serikali hiyo hiyo isione umuhimu wa kuwashirikisha wananchi katika shamba la Nkundi ili wawezæ kugawiwa wakati maombi yapo na ushahidi ninao na kwamba wananchi wanalalamika lakini wakaamua kugawa kinyemela? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, mashamba hayo baada ya kutolewa hekta 20,000 yatagawiwa kwa wananchi na wananchi kama nilivyoeleza inajumuisha mwananchi mmoja mmoja au wananchi waliojiunga pamoja kama ushirika au wananchi waliounda Kampuni chini ya Sheria za Makampuni na ndivyo tulivyofanya kwa shamba la Nkundi.

Pili, maombi ya wananchi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema yapo, nina hakika yataletwa na yatashughulikiwa wakati ugawaji utakapoanza. Kwa hiyo, naomba kama nilivyoeleza, wakati wa ugawaji au wakati wa kuomba kupatiwa mashamba hayo, wananchi ambao hawawezi ku-*manage* hekta 4,000 ni vizuri wakajiunga kama vikundi vya ushirika au kama Kampuni kama ilivyofanyika kwa shamba la Nkundi.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, alitoa maelekezo na maagizo yakatangazwa hata kwenye vyombo vya habari kuhusiana na utaratibu mzima utakaotumika katika kubinafsisha mambo haya; lakini kwa kuwa wawekezaji popote walipo hawatakubali kuwekeza katika masuala ya ardhi kama suala la wananchi bado halijatatuliwa; na kwa kuwa tatizo la Serikali hivi sasa inaonekana kuna kigugumizi katika kutoa maeneo haya labda kwa sababu ya gharama ya kugawa maeneo hayo.

Je, Serikali na hasa Waziri, anaweza kuliambia nini Bunge hili ya kwamba katika Bajeti inayofuata ameandaa utaratibu upi ili maelezo yasiwe tena ya kila siku kwamba mpango unaandaliwa wakati muda unakwisha na wananchi wanakata tamaa? *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, ugawaji wa mashamba haya unazingatia au ulizingatia kwanza kuhakikisha kwamba mashamba haya yamepimwa na kuwa na hati maalum kama sheria ya ardhi inavyohitaji.

Pili, vile vile katika kugawa mashamba madogo madogo ya hekta 4,000, hekta ambazo zimetolewa kwa ajili ya kuwagawia wananchi kuendeleza ufugaji pia inazingatia kupima hayo mashamba na kuyatayarishia karatasi au hati ambazo atakayemilikishwa atakuwa na urahisi zaidi wa kupata hati inayokubalika na ambayo anaweza kuitumia kukopa Benki.

Kwa hiyo, utaratibu na maamuzi yalifanyika mwaka 2002 na utaratibu umeanza kutekelezwa kama nilivyoeleza, mwezi Machi mwaka 2003, Kampuni ya Kizalendo ilipewa ardhi. Kwa hiyo sidhani kama kipindi cha mwaka mmoja au chini ya mwaka mmoja kimekuwa ni kirefu sana. Ni vizuri tukaelewa kwamba inahitaji tufuate taratibu zote za kisheria na masuala ya ardhi sio kitu rahisi ambacho unaweza kukifanya katika muda mfupi bila kuleta matatizo. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, napenda kuongezea majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kumwelewesha Mheshimiwa Paul Kimiti, kwamba Serikali haina kigugumizi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, tumekwishagawa Dakawa, tumegawa Nkundi na hivi karibuni tutagawa kule Morogoro. Kwa hiyo, hakuna kigugumizi. Tunatekeleza kama tulivyokubaliana kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Sera ya Maji ya Mto Zigi

MHE. MBARUK K. MWANDORO aliuliza:-

Kwa kuwa maji ni msingi mkuu wa uhai na kwa kuwa Mto Zigi wenye maji mengi unaanzia Wilayani Muheza na kupita kando kando ya Vijiji vingi Wilayani humo; na kwa kuwa wananchi katika Vijiji hivyo na Taasisi zilizo karibu na Mto huo wanakabiliwa na shida kubwa sana ya maji kutokana na haki ya maji ya mto huo *(water rights)* kuwa kwa ajili ya wakazi wa Taasisi za Manispaa ya Tanga pekee:-

(a) Je, Mamlaka husika zinakusudia kuchukua hatua gani ili kuwa na vihifadhia *(reservoirs)* vya kutosha kwa ajili ya mahitaji ya Manispaa ya Tanga ili hata yale maji yatakayokwenda Bahari ya Hindi kutoka Bwawani, Pande, Mabayani, yasipotee bure?

(b) Je, iwapo sera hii ya maji ya Mto Zigi kuwa kwa ajili ya Manispaa ya Tanga pekee itaendelea, Serikali inakusudia kuchukua hatua gani kuikabili kero kubwa ya maji inayowasibu wananchi wa Vijiji kama vile Segoma, Lanzoni, Bamba, Mavengere, Mjesani na Mnyenzoni?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilijenga bwawa la Mabayani kando ya Mto Zigi ambalo sehemu kubwa inaanzia Muheza na kupitia kando kando ya Vijiji vingi vya Wilaya ya Muheza. Bwawa hilo lina uwezo wa kutoa meta za ujazo 42,000 za maji kwa siku ambayo yanaweza kutosheleza mahitaji ya Manispaa ya Tanga hadi 2010.

Hata hivyo, Mamlaka ina mpango wa muda mrefu wa kujenga bwawa lingine la maji katika Mto Zigi ambalo litatunza maji wakati wa mvua na kuyaachia wakati wa kiangazi. Bwawa hili litatumika kuhifadhi maji ya ziada na ya tahadhari kwa ajili ya Manispaa ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Sera ya Maji ya Mwaka 2002 na Sheria ya Maji Na.42 ya 1994 iliyorekebishwa mwaka 1981 na 1997, Mamlaka ya Maji hairuhusiwi kuzuia maji yoyote yasiende baharini, kwani pamoja na mahitaji ya binadamu, kuna viumbe hai na uoto wa asili ambavyo vyote hutegemea maji hayo. Hivyo, kiasi cha maji kinachochukuliwa na Mamlaka na watumiaji wengine kinapaswa kuhakikisha kuwa kuna maji yanayobaki kwenye Mto. Kwa msingi huo, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Tanga inazingatia hilo kikamilifu.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka inayo hati ya kutumia maji ya Mto Zigi. Lakini kwa bahati nzuri, hati hiyo haizuii watumiaji wengine kuchukua maji kutoka Mto huo. Hivyo, tunashauri Halmashauri ya Wilaya ya Muheza iandae mpango wa kuvipatia maji Vijiji vya Segoma, Lanzoni, Bamba Mavengere, Mjesani na Mnyenzoni kutoka katika Mto huo kwa sababu ni wajibu wake. Hata hivyo, Wizara ipo tayari kutoa utaalam na ushirikiano wa karibu kwa Halmashauri ya Muheza na Vijiji hivyo pindi utakapohitajika na watakapoomba kufanya hivyo.

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wananchi wengi sana katika Vijiji nilivyovitaja na vinginevyo wanaathirika kwa kuuliwa na mamba na kuuawa; je, Serikali haioni umuhimu wa kuchukua hatua za haraka kutekeleza haya niliyopendekeza?

NAIBU WAZIRI WA MAJI, MAENDELEO NA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda tumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuliambia Bunge lako kwamba kuna mamba ambao wana

soko zuri kama hawatahitajika maeneo hayo na kwa uharibifu wanaoufanya. Lakini pili, ni vizuri wananchi wakafuata utaratibu wa sheria za uvunaji wa maliasili.

Hivyo basi, pamoja na majibu niliyoyatoa kwamba maji yanahitajika yabaki katika mto huo, ni pamoja na kuwafanya hawa mamba wasife ikizingatiwa kwamba maji yote yanatakiwa kutumika kwa ajili ya binadamu na kwa ajili ya wanyama waliopo kwenye maeneo husika. Kwa hiyo, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, pindi mradi utakapobuniwa, Serikali iko tayari kutoa ushauri na inapowezekana tutajaribu kutafuta upatikanaji wa msaada kutoka Serikalini au kwa wahisani, lakini ni baada ya kupata maombi ya mradi ambao utakuwa umebuniwa.

MHE. HERBERT S. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mji wa Muheza ndio upo karibu sana na chanzo cha maji ya Mto Zigi, lakini haupati huduma hii ya Maji kutoka katika Mto huu; je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuwasaidia wananchi wa Mji wa Muheza na vitongoji vyake kupata maji kutoka katika Mradi wa Ubembe Kwemhosi? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Utawala Bora, tunashauriwa miradi ianze kubuniwa kutoka ngazi za chini. Kwa mantiki hiyo, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, tunaomba Wilaya au Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ibuni mradi huo na kama nilivyotoa ahadi, Serikali iko tayari kusaidia katika kutatua tatizo la maji la wananchi wa Wilaya ya Muheza na Mji wa Muheza vikiwemo Vijiji alivyovitaja.

Na.77

Jukumu la Usimamiaji wa Sheria za Barabarani

MHE. DR. JAMES A. MSEKELA aliuliza:-

Kwa kuwa usimamiaji wa sheria za barabarani ni jukumu la *Traffic Police*:-

(a) Je, maandalizi yao kitaaluma hujumuisha masomo gani na kwa muda gani?

(b) Je, ni kwa kiwango gani hawa *Traffic Police* wanakidhi kwa idadi na ni Polisi wangapi wa kawaida bado huhitajika kufanya kazi kama *Traffic Police* ingawa hawajaandaliwa kitaaluma kwa majukumu yao?

(c) Je, ni ajali ngapi za barabarani zimesababishwa na Polisi wakati wakitekeleza majukumu yao ya usalama barabarani katika kipindi cha miaka mitano iliyopita?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi nchini ndilo lenye jukumu la kusimamia Sheria za Usalama Barabarani. Askari wote wa Jeshi la Polisi hupatiwa mafunzo ya mwanzo yanayohusu Sheria za Usalama Barabarani wanapojiunga na Jeshi. Askari wanaopelekwa katika Kikosi cha Usalama Barabarani hupatiwa mafunzo ya nyongeza ya sheria zihusuzo usalama barabarani kwa miezi mitatu ili kuwawezesha kuzisimamia sheria hizo kwa ufanisi zaidi. Pamoja na kufundishwa kwa undani mambo mbalimbali ya usalama barabarani masomo mengine yanayotolewa katika mafunzo hayo ni pamoja na Kazi za Polisi, Huduma ya Kwanza yaani *First Aid,* Upelelezi na Mawasiliano.

(b) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limekuwa na upungufu wa Askari kwa muda mrefu. Upungufu huu pia huathiri maeneo ya Vikosi vingine ikiwa ni pamoja na Kikosi cha *Traffic.* Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani waliopo sasa ni 1,255, idadi ambayo ni nusu tu ya mahitaji. Kama nilivyoeleza awali, Askari wote wanaojiunga na Jeshi la Polisi hupatiwa mafunzo ya awali ya shughuli za Usalama Barabarani. Hivyo, pale ambapo Kamanda wa Mkoa anaona kuna upungufu mkubwa wa Askari

wa Usalama Barabarani, Askari wa kazi za kawaida huteuliwa kufanya kazi hizo chini ya viongozi wenye uzoefu, kabla ya kupelekwa kwenye mafunzo ya Usalama Barabarani.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita hakuna ajali ya barabarani iliyosababishwa na *Traffic* wakati wakitekeleza majukumu yao ya usalama barabarani. Madreva wakorofi wanaokiuka taratibu na Kanuni za Sheria za Usalama Barabarani ndio chanzo cha ajali ambazo baadhi yake zimehusisha Askari wa *Traffic* kugongwa na wengine kupoteza maisha yao au kuumia na kupata vilema. *(Makofi)*

MHE. DR. JAMES A. MSEKELA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali la msingi ameonyesha kwamba hawa Askari Polisi wote wanakuwa na mafunzo angalau ya awali juu ya Sheria za Barabarani; je, sasa anasemaje au anaweza kuagiza sasa kwa mfano *Police Traffic* ambao wanakuwa wanasimama barabarani Dar es Salaam kwenye *traffic lights* ambazo zinafanya kazi, wanaanza kutoa *direction* tofauti na zile taa ambazo huonekana mbali wakati Polisi mwenyewe amesimama hapo chini na haonekani, kiasi ambacho wameshapata ajali wao wenyewe?

(b) Kwa kuwa pia anasema hawa Askari Polisi wamepata hayo mafunzo ya awali karibu wote na kwa kuwa hawa *Traffic Police* wanahusishwa sana na rushwa; je, anasemaje kuhusu utaratibu wa kuanza kuwazungusha basi, ili sura zile zile ambazo tunaziona kwenye Miji mikubwa kama Dar es Salaam ziondoke barabarani kwa sababu wanaonekana kuwa ni vichaka vya rushwa? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Askari wa *Traffic* kwa utaratibu hawatakiwi kuingilia taa za barabarani kama zinafanya kazi sawasawa. Anaweza akaingilia kama pengine kuna msafara wa kiongozi mkuu wa nchi ambaye hawezi akangoja kwenye taa au kama kuna dharura nyingine yoyote. Lakini katika hali ya kawaida hawaruhusiwi. Kama kuna baadhi ya wanaofanya hivyo, nataka kutumia nafasi hii kuwakemea na kusema kwamba lazima tufuate utaratibu wa kazi zao. *(Makofi)*

Pili, kuhusu suala la rushwa, Mheshimiwa Mbunge anasema tuwazungushe. Suala la kuwazungusha Askari Polisi ni la kawaida. Kuwe na rushwa au hakuna rushwa ni utaratibu wa kawaida kuwazungusha katika Vikosi mbalimbali. Lakini dawa ya rushwa sio kuwazungusha. Dawa ya rushwa nataka niwaombe Watanzania wenzangu watueleze wale ambao wanajihusisha na rushwa ili tuwachukulie hatua za kisheria.

Kwa mwaka 2002, tunawashukuru baadhi ya wananchi walitupa taarifa kamilifu, tulichunguza tukakuta ni kweli kuna *Traffic* watano na wamefukuzwa kazi kwa makosa ya rushwa. Tunaomba tupewe taarifa kamilifu na tutachukua hatua ili tukomeshe tatizo la rushwa katika kikosi cha *Traffic* na katika Jeshi zima la Polisi. *(Makofi)*

SPIKA: Nawaona Waheshimiwa, lakini bado nina maswali mawili na zimebaki dakika kumi tu. Kwa hiyo, subirini Wizara itakapowasilisha hoja zake Bungeni. Tunaendelea, Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, swali linalofuata. Hayupo, kwa hiyo Mheshimiwa Lekule Laizer, muulizie kwa niaba yake. *(Kicheko)*

Na.78

Kuanzishwa kwa Bima ya Abiria Wanaosafiria Mabasi

MHE. LEKULE M. LAIZER (k.n.y. MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN) aliuliza:-

Kwa kuwa kuna ongezeko kubwa la ajali za barabarani zinazosababisha maafa makubwa kwa raia wasio na hatia pamoja na mali zao; je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuanzisha Bima ya maisha ya abiria wanaosafiria mabasi kwa lengo la kuongeza uangalifu na uwajibikaji wa wamiliki wa mabasi hayo kwa wasafiri?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna ongezeko la ajali barabarani ambazo husababisha maafa na uharibifu wa mali. Wasafiri wa mabasi wanaopata ajali wanakingwa na Sheria ya Bima ya Magari yaani *The Motor Insurance Ordinance No.169*. Chini ya sheria hii, kifungu Na.4(1) ni kosa kwa gari lolote kuendeshwa barabarani likiwa halina Bima halali na hai. Zipo aina mbili za Bima za magari. Aina ya kwanza ni ile inayomkinga mmiliki wa gari, gari lake na watumiaji wengine wa barabara na mali zao yaani *Comprehensive Insurance Policy*. Aina ya pili ni ile inayotoa kinga kwa watumiaji wengine wa barabara na mali zao yaani *The Third Party Insurance Policy* na aina hii ya Bima ni ya lazima kabisa. Bima hizi ndizo hutumika kulipa fidia kwa wasafiri wanaopata ajali kwenye magari ya abiria. Sheria ya Bima ya magari iliyopo hivi sasa bado ni nzuri na inakidhi matakwa yaliyopo kwa waathirika wa ajali pindi zinapotokea. Kwa hiyo, Serikali kwa hivi sasa haioni umuhimu wa kutunga sheria nyingine ya Bima kwa waathirika wa ajali za magari ya abiria. *(Makofi)*

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wananchi hawajui utaratibu huu wa Bima, kwa hiyo, wanapopata hasara hawawezi kudai; Serikali haioni kwamba sasa umefika wakati wa kuwaelimisha wananchi ili waweze kudai walipwe fidia? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa najibu hivi karibuni swali la nyongeza la Mheshimiwa Edson Halinga, nilieleza kwamba sheria hii ya Bima, wananchi wengi hasa kule Vijijini hawaifahamu vizuri, kwa hiyo, wakati mwingine wanashindwa kufuatilia haki zao. Nilitoa wito siku ile na leo tena nataka kurudia kwamba wajibu wa kuelimisha wananchi kuhusu haki zao mbalimbali pamoja na hii ya kudai fidia ya Bima, Waheshimiwa Wabunge tuifanye kazi hiyo katika Majimbo yetu na viongozi wengine wote na Makampuni ya Bima nayo yana wajibu vile vile wa kuelimisha umma kwa sababu vile vile hii ni biashara yao. *(Makofi)*

SPIKA: Nazingatia muda. Swali la mwisho kwa leo Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji.

Na.79

Kodi ya Zuio - *Withholding Tax*

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoza kodi ya zuio *(Withholding Tax)* ya asilimia kumi kwa malipo ya *Directors Fees* kwa Wakurugenzi wasio wa kudumu *(Non Full Time Board Directors)* wa Bodi mbalimbali kwa lengo la kukusanya mapato ya ndani ili kupunguza hatua kwa hatua utegemezi wa Bajeti kwa misaada na mikopo kutoka nje:-

(a) Je, hivi sasa kuna Bodi ngapi ambazo zinahusika na Wakurugenzi wasio wa kudumu?
(b) Je, kuanzia Julai, 2002 hadi Machi, 2003, kwa Bodi hizo zisizo za kudumu kuna Wakurugenzi wangapi wasiokuwa wa kudumu?

(c) Je, ni fedha kiasi gani zinakusanywa kutoka kwa Wakurugenzi hao tangu utaratibu wa zuio la asilimia kumi uanze kutumika?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, napenda kutoa maelezo mafupi kuwa kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanywa Juni, 2002 kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 katika kifungu nambari 34, Malipo ya Mwaka ya Ada

ya Ukurugenzi yaani *Director Annual Fee* kwa Mkurugenzi ambaye si mfanyakazi wa kudumu wa Taasisi husika, yanapaswa kukatwa kodi ya zuio ya asilimia kumi ya kiasi cha ada inayolipwa kwa mwaka.

Ada hii haihusu malipo ya Vikao vya Bodi *(Sitting Allowances)* ambazo hutakiwa kutozwa kodi ya mapato kama malipo ya ajira. Kwa kawaida, malipo ya ada ya mwaka hufanywa baada ya mwaka wa fedha yaani *accounting year* wa Taasisi husika kuisha.

Baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hivi sasa kuna Bodi 78 ambazo zinahusika na malipo ya ada kwa Wakurugenzi wasio wa kudumu.

(b) Kuanzia Julai, 2002 hadi Machi, 2003 kwa bodi hizo kuna Wakurugenzi wasio wa Kudumu wapatao 272.

(c) Kiasi cha kodi kilichokusanywa kuanzia utaratibu huu ulipoanza kutumika ni shilingi 26,294,090.80.

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza. Katika Wakurugenzi hawa, anaweza akatuambia kuna Wakurugenzi wangapi ambao ni Wazalendo na kuna Wakurugenzi wangapi ambao si wazalendo? Ahsante sana.

SPIKA: Wazalendo kwa maana ya raia?

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Raia wa Tanzania.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwenyewe, majibu.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mapato ya Kodi, haibagui raia wala asiye raia. Inalipwa pale mtu anapopatia mapato yake. Kwa hiyo, hatuna takwimu hizo kwa sasa hivi kwa sababu hatuzihitaji. Tunahitaji kujua tu ni Wakurugenzi wangapi ambao tumetaja kwenye Jimbo letu na ndiyo hao nawalipa hiyo asilimia 26 ya *Withholding Tax*.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, kabla sijaendelea na shughuli nyingine kama kawaida kuna matangazo. Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, alipokuwa akijibu swali hapa alisema, ameshinikizwa, amesukumwa na muuliza swali, ili aweze kutoa taarifa, ametoa majibu ambayo pengine asingeyatoa ni kwamba amesukumwa.

Sasa na mimi leo asubuhi nimesukumwa, nimeshinikizwa niwatambulishe Watanzania ambao kwa kawaida wanakuwa kwenye *Gallery* yetu, ambao kwa kawaida huwa hatuwatambulishi, Watanzania ni haki yao kuja kwenye *Gallery* kusikiliza majadiliano ya Bunge. Kwa hiyo, huwa siwatambulishi. Lakini leo nimeshinikizwa. *(Kicheko/Makofi)*

Niwatambulishe walioko kwenye *Gallery* ya Spika, *diplomatically*. Basi kutokana na shinikizo hilo napenda kusema kwamba walioko huko ni *Miss Tanzania* wa mwaka 2002, pamoja na warembo, nikikutaja usimame, pamoja na warembo wa Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma pamoja na Maafisa wa Kamati ambayo inaandaa mashindano ya *Miss Tanzania*. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya shinikizo sasa natangaza kikao cha Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athumani Janguo, ameomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 20 Juni, 2003 saa 4 asubuhi au mara baada ya kipindi cha maswali katika Kumbi zetu za Kamati. Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2002 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2003/04 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/04

(Majadiliano Yanaendelea)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika hoja mbili kwa nia ya kuziboresha hususan kulingana na jinsi hoja hizi zilivyopokelewa na wananchi na wapiga kura wangu wa Babati Magharibi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kupandishwa kiwango au kima cha chini cha pensheni kwa wastaafu. Serikali inastahili pongezi na kwa kweli imepongezwa sana na wananchi. Lakini naomba kwa msisitizo mkubwa kurekebishwa kwa haya yafuatayo:-

(a) Wastaafu hawa walipwe kila miezi mitatu badala ya miezi sita. Wastaafu wanasema sababu iliyofanya muda wa kulipwa wa miezi sita haipo tena kwani sasa kuna ahueni ya shilingi 60,000/= kwa miezi mitatu inaridhisha.

(b) Wastaafu waliolipwa kwa mkupuo na bado wanaishi baada ya miaka waliokadiriwa kuishi na wananchi kwa tabu sana. Yaletwe marekebisho ya sheria husika ili kuwaangalia wastaafu wetu hawa.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu gharama za simu katika nchi yetu ni kubwa mno. Hiki kimekuwa kikwazo kikubwa. Naomba Serikali itueleze ni kwa jinsi ipi gharama za simu kubaki zilivyo au kupanda kwa upande wa simu za mkononi kuendana na suala zima la kufikisha umeme vijijini. Hali ilivyo sasa ni kwamba wananchi wa kawaida wanashindwa ku-*afford* kuwa nazo naomba tusaidiwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. USSI YAHYA HAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nashukuru kwa dhati hotuba ya Waziri wa Fedha pamoja na Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Serikali yetu tukufu ambayo inaongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wa kishindo walioupata Wabunge wanne wa Chama cha Mapinduzi kwa majimbo ni Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Mbunge wa Bukoba Vijijini, Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Edward Nziriye Ndeka, Mbunge wa Kigoma Kusini na Mheshimiwa Sumri Abdullah Salum Mohamed Mbunge wa Mpanda Magharibi. Ushindi wao huo ni dalili tosha kwamba Chama cha Mapinduzi kinakubalika katika majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, hotuba ambazo zimetolewa na Mawaziri wote wawili ni hotuba ambazo zimejaa matumaini kwa wananchi wa Tanzania pia zimeonyesha muelekeo ambao Watanzania wanaelekea na pia zimewapa mwanga wa matumaini kwa maisha yao kwa kuona Serikali yao imepania kuwakomboa katika dimbwi la umaskini ambao wakati mwingi huwa unachangiwa na Bajeti tegemezi.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri, naomba nishauri wakati uchapishaji wa noti ambazo tunatumia ndani ya Jamhuri yetu ni vema wachumi na watalaamu kutoka Tanzania Zanzibar nao wakashirikishwa wapo lakini hawashirikishwi. Pia naomba Serikali kuchukua tahadhari kubwa wakati wa uchapishaji wa noti hizo kwani noti mpya zilitoka safari hii zimeleta matatizo makubwa kwani wajanja wameweza kuzitengeneza na kutumia isivyo halali.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kwa dhati kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza kwa dhati Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa hatua yake ya kuitumia kikamilifu Banki Kuu ya Tanzania kwani kwa muda mwingi hawakuwa wakitumia Benki hiyo. Kwa kuitumia kikamilifu Benki hiyo Wananchi wa Zanzibar watapata faida hasa itakokanayo na Benki hiyo. Tofauti na baadhi ya watu ambao hawapendi Serikali kuitumia Benki hiyo na kuvumisha usemi usemao fedha za Zanzibar zimewekwa katika Benki ya

Tanzania Bara, kwani Benki hiyo ni mali ya Serikali mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 44 ambao umesema kwamba Bajeti hii imetenga asilimia 4.5 ya mapato yatakayotokana na misaada *(Programe Assistance)* ya nje kwa ajili ya kuisaidia Bajeti ya Zanzibar siyo sahihi, kwani huu siyo msaada ni wajibu kwa mujibu wa makubaliano ya nchi hizi mbili. Tangu awali na siyo kwa mujibu wa muafaka kwani Mheshimiwa Waziri ukitamka kwa mujibu wa muafaka wananchi labda wengine watafahamu ule muafaka na Chama cha Mapinduzi na *CUF*.

Mwisho naomba Mheshimiwa Waziri suala la matumizi ya bandari zetu Bara na Viwasini lichukuliwe hatua na mamlaka zinazohusika ili kuondoa kabisa bughudha ambazo hazina msingi na wala hazitoi sura nzuri kwa wananchi wetu ambao kwa sasa wameanza kuendelea kufaidi matunda yao ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maumbile ya Bajeti ya mwaka huu namna ilivyoletwa ni wajibu wangu pia kuwapongeza kwa dhati wale wote ambao wamefanikisha Bajeti hii hususan wachumi, washauri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Mhasibu Mkuu wa Serikali na wengine wote walioshiriki kwa muono wao wa kutuwezesha kuletwa Bajeti hii Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

MHE. ALI MACHANO MUSSA: Mheshimiwa Spika na mimi naona niungane na Waheshimiwa Wabunge, wenzangu kumpongeza Waziri wa Fedha, pamoja na Watendaji wa Wizara yake ambao walishiriki katika utayarishaji wa hotuba hii ya Bajeti na sina budi kusema naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kuwapongeza Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, walioshinda katika uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni. Nafikiri sasa ni wakati muafaka kutoa sababu zilizonifanya niunge mkono hotuba ya Bajeti ni yale mambo ambayo yameigusa jamii imeonyesha mfano mzuri wa kuwajali sana kwa kuchukulia hatua ya kuwaondolea kodi nyingi ambazo zilikuwa kero kwa wananchi zilikuwa zinawanyima raha wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, pia naona nitoe wazo langu kuhusu ile ruzuku ya asilimia 4.5 ambayo Serikali ya Tanzania kuipa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hili ni sawa lakini nahisi limechelewa sana ilikuwa lianze mara tu baada ya kuundwa kwa Benki lianze mara tu baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wazo langu binafsi nahisi kuna haja ya kuyaangalia mahesabu ikiwekana Zanzibar ipewe ruzuku zaidi kama ikiwezekana.

Mheshimiwa Spika, pia naona nizungumzie kuhusu hali ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Idara ya Jeshi la Polisi. Katika hotuba hii safari hii inaonekana imepata fedha zaidi hali inayoonekana ni tofauti na bajeti zingine zilizopita. Polisi wamepata fungu kubwa ambalo halitoshi lakini litasaidia vizuri zaidi kuliko kipindi kilichopita. Kwa hiyo, naona nitoe wazo kwa Jeshi la Polisi kwamba umefika wakati Wakuu wa Polisi kujaribu kununua vitendea kazi na pia kuwajali watendaji kazi ambao ni polisi wenyewe. Wapewe vifaa na mishahara minono ambayo angalau waweze kufanya kazi kwa uangalifu na raia warejeshe imani kwa jeshi lao la polisi.

Mheshimiwa Spika, naona nizungumzie suala la vitambulisho vya Taifa hili napendekeza kuwa pamoja na kuwa tuna uhaba wa pesa, lakini kama tulivyooamua kuhesabu Sensa ya Taifa, kwa kutumia gharama kubwa naomba pia tutumie gharama yoyote ile tupate vitambulisho kwa wananchi wetu ili tuweze kutambuana kwa sababu kuna Watanzania wengi na makabila mengi ambayo yanafanana na makabila ya nchi jirani. Hii itapunguzia wahamiaji wageni ambao wengi usalama wao ni mdogo na wanasababisha hofu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, pia baada ya kutoa maoni ya vitambulisho pia naona nizungumzie katika vitambulisho *(Passport).* Hili suala la *passport* lina maana kubwa ambalo likizungumziwa wengi wao huona hakuna haja ya kuwepo *passport* kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mimi maoni yangu iwapo kutokana na mambo ambayo yanajitokeza, nafikiri kama tunavyokubali kujikosoa kwa mambo mengine na hili nalo tukubali lilikuwepo zamani na tukaliondoa kama tulivyolirekebisha suala la kodi tumeiweka na tumefika wakati tumeona kuna haja ya kuiondoa.

Kwa hiyo, nashauri *passport* zirejeshwe ili tuondoe matatizo ya wahamiaji haramu ambao huiingia Zanzibar na kufanya uhalifu mkubwa wa kutumia silaha na wakitumia kama wao ni makabila ya Tanzania Bara kwa kweli makabila hayo yapo Tanzania lakini siyo Watanzania bali ni watu wa mipaka ya jirani na hii nafikiri liwatoe wasiwasi Watanzania *passport* hizi isiwe vikwazo vya kuingia Zanzibar, isipokuwa tuwe na uwezo wa kuelewana ni nani anayeingia na anatoka wapi. Pia tukitilie maanani kuwa Kisiwa hata wakimbizi wanatakiwa wasikimbilie sana kwenye visiwa kutokana na hali ya visiwa kuwa havina maeneo makubwa ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, mwisho sina budi kusema kuwa naunga mkono hotuba hii na iweze kusimamia mipango iliyoipanga itekelezeke na itoa mfanikio.

MHE. HADIJA K. KUSAGA: Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu waliotangulia kuchangia hotuba hizi mbili kwa kuwapongeza Mawaziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinashaji, kwa hotuba zao nzuri hivyo ninaunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kufuta kodi ya maendeleo kwani ilikuwa ni kero kwa wananchi na hasa wafanyakazi wa Serikali na Mashirika ya Umma kwani wao walikuwa wanakatwa moja kwa moja kwa kuwa asilimia katika mishahara yao. Walikuwa wanatutuma sisi kuiomba Serikali angalau walipe kiwango sawa na wananchi wengine kilichopendekezwa na Serikali. Kwa upande wa Mkoa wa Dar es Salaam hatukuwa tunafanikisha sana katika kudai kodi kwa mtu mmoja mmoja. Tulifanikisha pia kwa wafanyabiashara wanapokata leseni za biashara zao. Ninampongeza sana Mheshimiwa Basil Mramba.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtovu wa shukrani kama sitamshukuru Waziri wa Fedha, kwa kuweza kutenga fedha shilingi billioni 5 kwa ajili ya ujenzi wa awali wa uwanja wa kisasa wa Taifa wa michezo ambao amesema utaanza kujengwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kama tutakumbuka nimekuwa nikilipigia kelele sana na hasa kila ninapomuona Mheshimiwa Rais, nilikuwa nikimuomba kuwa uwanja huo wa kisasa ujengwe Temeke. Mheshimiwa Rais, alikubali ombi langu na uwanja huo sasa unajengwa Temeke. Kwa niaba ya wananchi wa Temeke napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kukubali ombi letu na pia kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kutenga fedha ili uwanja huo uanze.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia moja.

MHE. MWADINI ABASS JECHA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba niipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuunda Tume ya pamoja ya fedha ya Muungano ambayo kazi yake ni kuzishauri Serikali zetu kuhusu utaratibu wa kugawana mapato ya Muungano.

Labda niseme kwamba suala la mgao wa mapato ya muungano ni suala la tete na nyeti na lina mvuto mkubwa katika siasa ya Tanzania. Hiki ndiyo kimekuwa ni kilio kikubwa cha Wazanzibar kwa muda mrefu sasa ninaona kuna dalili ya mwangaza unaoonekana.

Mheshimiwa Spika, aidha, asilimia 4.5 iliyotengwa ya mapato yatokanayo na misaada ya nje *(program assistance)* kwa ajili ya kusaidia Bajeti ya Serikali ya Zanzibar. Suala hili lilifanyiwa uamuzi zamani kidogo. Sijui ni kwa nini utekelezaji wake umechelewa?

Mheshimiwa Spika, lakini la kushangaza zaidi ni kutokuonekana kifungu au sura yoyote ndani ya kitabu cha Bajeti iliyowasilishwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri, anieleze ni kasma gani ya hiyo 4.5%

ambayo Zanzibar itapatiwa. Aidha, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, anihakikishie kwamba hii asilimia 4.5 itapatikana kikawaida au ni kilichoelezwa kwenye Bajeti ni kiini macho tu.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aipatie Serikali ya Zanzibar, mgao wa mapato yatokanayo na Benki Kuu *(BOT)* ambao mgao huo ulingane kwa asilimia ya mtaji wa kila upande wa Jamhuri uliochangia katika mtaji ulioanzisha Benki hiyo.

Aidha, mimi sioni sababu kwa nini Zanzibar haipati mgao wa fedha zitokanazo na msamaha wa madeni ya nje, tukijua wazi kuwa hili ni suala la Muungano nadhani sasa umefika wakati Mheshimiwa Waziri, kuhakikisha kwamba Zanzibar nayo inafaidika na *HIPC.*

Mheshimiwa Spika, penye nia nzuri haya yote yanatekelezeka licha ya kuzungumzika.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuuona ule umuhimu wa kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu. Kwani sekta hii licha ya kulipatia Taifa letu chakula lakini pia sekta hii ndiyo inayotoa ajira kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuona umuhimu wa kuwapunguzia wakulima bei ya mbolea hususan Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Iringa na Ruvuma, kwamba ndiyo Mikoa ambayo huzalisha chakula kwa wingi. Aidha, maandalizi ya kuwapatia mikopo ili kuongeza uzalishaji ni jambo la busara kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kuitanabaisha Serikali kwamba nafuu hiyo iliyotolewa kwa wakulima hao siyo kichocheo pekee cha kukuza uzalishaji, ni lazima Mheshimiwa Spika, azingatie pia upatikanaji wa mbegu bora na tena kwa wakati unaofaa, elimu ya uzalishaji mazao na hifadhi bora ya mavuno, upatikanaji wa hiyo mikopo iwe ya riba nafuu na ipatikane pale inapohitajika, upatikanaji wa dawa za magugu na za wadudu waharibifu, Serikali kutoa bei nzuri kwa mazao ya wakulima, kuboresha miundombinu ya barabara na masoko *(transport, market and market facilities).*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuiomba Serikali katika azma yake ya kutaka kuongeza mazao ya kilimo basi hapana budi mambo niliyoyataja hapo juu yazingatiwe kwa upeo mkubwa.

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa nitoe ufafanuzi katika hoja yangu ya kutoruhsu *contractors* wa wenye migodi kupewa *exemptions* kama wenye migodi. Hawa *contractors* kwa sababu aghalabu atakuwa na shughuli biashara zake zingine na ile ya u-*contractor* ni sehemu tu ya biashara zake. Kuna uwezekano mkubwa akatumia mwanya huo kupata *exemption* kwa bidhaa zinazokwenda kwenye biashara zake zingine na siyo kwa *(principal)* wake wenye migodi.Tuwe makini sana kwenye hili tusiruhusu mwanya huu na utitiri wa *contractors.*

Mheshimiwa Spika, pili, kwenye suala la magari yenye *exemption* ya wafanyakazi wa Serikali. Kwa sasa magari haya hayaruhusiwi kuandikishwa kama *taxi* na unachoona ni kwamba wafanya kazi hawa wanavyotumia kama *taxi* bubu. Napendekeza wafanyakazi hawa waruhusiwe kuyaandikisha kama *taxi* ingawa ni *exempted.* Kuna faida kwa pande zote ambazo ni kama ifuatavyo:-

(a) Wafanyakazi hawa watapelekwa kazini, kisha magari haya *(taxi)* yataweza kuwaongezea kipato baada ya hapo mishahara yao ni midogo.

(b) Serikali itapata kodi halali ya *taxi,* leseni, *income tax* na kadhalika.

(c) Tutazuia *taxi* bubu na kukosesha Serikali mapato.

MHE. ANTHONY M. DIALLO: Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa *Budget* yake nzuri. Pia Bajeti yetu haipo *balanced* kwa vile baada ya kutoa *Development Levy* kuna *gap* ya *over 42 bilion* ambazo hujaonyesha utazipata vipi katika Bajeti yako hasa ikizingatiwa kuwa Bajeti za Halmashauri zilikuwa zimefungwa *by May 15th.* Hivyo *you/we can not claim* kuwa Bajeti iko *balanced at all. You need to recalculate it by either* kukata baadhi ya matumizi au kuanzisha/kurekebisha baadhi ya kodi ili kupata *(deficit)* nakisi hii katika Bajeti yetu.

Pia vile vile ununuzi wa bidhaa za Serikali kwa hivi sasa hauhitaji ukaguzi wa bidhaa kupata ubora, wingi au ubora wa bei *(price quality and quantity)* hivyo tunategemea tu utaratibu wa *tender*. Utaratibu wa kupata *tender* zaidi ya moja siyo suluhisho la kutatua uwezekano wa kuuziwa vitu bei ghali *(over invoicing)* kwa vile kampuni nyingi za wazabuni zina uhusiano wa kikampuni au kifamilia hivyo uwezekano ni mkubwa wa ku-*cartel* wakati wa *tender* hivyo basi suluhisho pekee ni kukagua mizigo yote kabla ya *supply*. Mizigo au manunuzi yote toka hapa nchini na nje, maunuzi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu gharama yake ni kwamba asilimia 1.5 ya bei ya manunuzi lakini *saving* yake ni zaidi ya asilimia 40 au 50. Hivyo basi utaratibu huu ukianzishwa fungu la *supply (supply vote)* na Maendeleo utapata *saving* ya *more than 40% ,* hivyo kuwa na *surplus* ya zaidi ya bilioni 350 mwisho wa mwaka huu wa fedha 2003/2004. Mapendekezo utaratibu huu uanze na nakisi yoyote. *Cases* za *over invoicing* ni nyingi hata Wizara kwetu, *TVT* na kila eneo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja yetu.

MHE. REMIDIUS E. KISSASSI: Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu.

Kwanza kabisa napenda kuunga mkono suala suala la Wabunge na wananchi wa kawaida kupewa elimu zaidi juu ya mwekezaji katika hisa na namna ya kumwezesha Mwananchi wa Tanzania.

Pili, pamoja na *PSRC, PTF* na *TIC* kupeleka ripoti zake kwa Kamati ya Fedha na Uchumi. Lakini vile vile wawemo *LART*.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu wake pamoja na watendaji kwenye Wizara hii, kwa jitihada zao za kina, kuhakikisha kuwa wanatuletea Bajeti ambayo ni ya ukombozi wa Watanzania wanyonge, ni Bajeti makini ya yenye kuwaondolea kero Watanzania. Bali inaonesha wazi tafsiri ya kukua kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza vile vile Wajumbe wa Kamati ya Uchumi na Fedha, ikiongozwa na Mheshimiwa Njelu Kasaka kwa kweli wamekuwa makini na wameichambua bajeti hii kwa kuielekeza CCM katika uchaguzi wa 2005.

Mheshimiwa Spika, mwisho nikupongeza wewe Mheshimiwa Spika, kwa umahiri na upeo mkubwa ulionao kwa namna ulivyozipanga upya Kamati za Kudumu za Bunge na ulivyozipangia majukumu nakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninaunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia na naikubali kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza kwanza kwa kuwaondolea kodi ya maendeleo Watanzania. Kodi hii ilikuwa ni kero na kwa kweli iliwanyima uhuru wao wananchi na kuwafanya watumwa kwenye nchi yao. Kodi hii haingepaswa kuwepo kwa sababu kadhaa zifuatazo:-

(a) Makusanyo yake yalikuwa ya ubabaishaji zaidi, fedha zilizokusanywa zilikuwa zinaishia kwenye mikono ya watu badala ya Halmashauri.

(b) Ilikuwa inaleta bughudha kwa wananchi kufika hadi walizikimbia nyumba zao na kulala misituni. Lakini zaidi ni kuwa kulikuwa na watu wakatumia mwanya huu kuchochea utengamano.

(c) Ilikuwa inahatarisha Watanzania na Chama chao cha CCM. CCM ilionekana kama mtawala na si Chama cha watu.

Pili, lakini naipongeza vile vile kwa kutenga fedha zaidi katika kilimo. Hapana shaka palizingatiwa zaidi katika kilimo. Hapana shaka palizingatiwa umuhimu wa kilimo na Pato la Taifa. Siyo hivyo tu bali kilimo ni ajira na tegemeo kubwa kwa Mtanzania wa kawaida asilimia 80% ya Watanzania ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa siku za baadaye miaka ijayo tujielekeze zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji *(irrigation)*. Kilimo cha kutegemea mvua siyo endelevu na ni hatari.

Mheshimiwa Spika, tatu, naipongeza Wizara (Waziri) kwa mara ya kwanza tangu nchi hii kuungana kwa kutelekeza Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuunda Tume ya pamoja ya fedha baina ya Serikali zetu hizi mbili. Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Naelewa juhudi na jitihada za makusudi zilichukuliwa baina yetu ili kutekeleza azma hii kwa hilo nalo nawapongeza.

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusu mgawanyo wa fedha za misaada kwa kweli asilimia 4.5 imepitwa na wakati na ni ndogo mno hasa ukizingatia hali ya uchumi na thamani ya fedha na zaidi ni kuwa Zanzibar ilitengwa kimisaada muda mrefu sana. Nashauri kwa hiyo basi kima hiki kiongezwe na vile vile ya undugu angalau kufikia asilimia 10 hakuna lisilowekezekana kama nia ipo.

Mheshimiwa Spika, tano, suala la biashara na umoja wa soko la Afrika ya Mashariki Zanzibar, haionekani kuwemo kwenye ramani umoja huo moja kwa moja bali inaingia kama Tanzania Zanzibar ni kisiwa kina viwanda uchumi wake wategemea iagize kutoka nje na iuze. Bila ya kuwepo utaratibu mahususi na jitihada za makusudi kuchukuliwa kwa kuwekewa maeneo maalum ili iweze kujiendesha, hali ya baadaye itakuwa mbaya sana na itahatarisha umoja muungano wetu. Wapinzani wanalichukulia suala hili la uchumi kama ni agenda yao ya baadaye na kwa kina ndiyo matokeo ya uchaguzi wa Pemba mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, sita, nashauri suala hilo lizingatiwe haraka iwekezanavyo. Hivi sasa Zanzibar na wananchi wake wanateseka na Wapinzani wanalishangilia hilo.

Mheshimiwa Spika, saba, nampongeza Waziri kwa mara nyingine kwa kuiongezea fedha Wizara ya Mambo ya Ndani. Naelewa wamelizingatia hili na kuliona bila ya utulivu hakuna maendeleo. Lakini kuna malalamiko kwa fedha hizi mara nyingi huwa haziwafikii walengwa polisi wa kawaida huwa zinaishia juu kwa wakubwa. Naomba safari hii hili liangaliwe vizuri. Vijana wetu wanafanya kazi kubwa. Jeshi la Polisi kama walinzi wa mali za Wananchi na wananchi wenyewe ni hazina kubwa. Lazima tuitetee kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, nane, kuna mengi ambayo yanapaswa kutajwa kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kama vile, pensheni kwa wazee, kutengwa/kuongezwa fungu la mishahara, kuondoshwa kwa kodi ndogo ndogo zaidi ya 50 na kuwalipa wakuu wa vijiji mishahara, kuweka mfuko maalum kwa wafugaji wakulima wadogo wadogo na wavuvi, kuondoa mfumo wa malipo ya fedha kuwalipa mikoa na sasa kulipa moja kwa moja Wilayani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo na mengine mengi naunga mkono tena Bajeti hii. Ahsante.

MHE. SHAAME SIJAMINI MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa na taadhima napenda kukushukuru kwa kukubali nichukue fursa hii maalum kuchukua fursa ya kutoa mchango wangu kwa Wizara zetu mbili ambazo Wizara ya Fedha na Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu mimi na wapiga kura wote wa Jimbo la Kitope, naona fahari kubwa kuipongeza hotuba hii ya Bajeti ya Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii Bajeti imeandikwa vizuri imekuwa wazi na imekuwa ya uchambuzi wa kina na imekuwa na mwelekeo wa kumkomboa zaidi mnyonge na takribani watu wenye kada mbali. Hii hotuba kwa hakika mbali na kuwakidhi wananchi wenye kipato cha chini tu bali imeleta faraja. Zanzibar kwa kuanishwa rasmi katika maelezo yaliyoelezwa kwa ufasaha katika muundo wa Kamati ya pamoja ya Fedha jambo ambalo kwa hamu kubwa tulilisubiri sana sisi kule Zanzibar kwani sasa nina hakika kuwa Zanzibar itaelewa kutumia

fursa ya kuitumia Benki Kuu ya Tanzania. Nina hakika kuwa yale mashaka ya wananchi wengi hususan *CUF* hii ilikuwa sera yao kuwavunja moyo kwamba eti Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa inanyonywa tokea Mapinduzi hayo na fedha zote na wanaofaidika ni watu wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kuona kuwa Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, pamoja na watalaam wake walivyoonyesha nini maana ya uongozi wa Serikali na ahadi yake pamoja na kufuata sera zake. Ni kweli naona sababu ya kufanya haya ambayo kwa wapinzani imekuwa *issue* ya *suprize* jambo ambalo Serikali hii inafanya na kuahidi mambo kwa mujibu wa kipimo cha uwezo wa nchi kimapato na hivyo ndiyo maana ya kufuta kodi ambazo zimekwishatajwa.

Mheshimiwa Spika, nimeshangazwa sana na anayejiita kuwa Profesa kudai kuwa Bajeti yetu ina kasoro eti kwa sababu hakuona maainisho ya kununua Ndege ya Serikali, hili si jambo la kudhibiti Bajeti hasa kwa kuwa huyu mtamkaji wa lugha hii inaonyesha dhahiri kuwa hana tabia ya kusoma na anashida ya kufahamu kiswahili.

Kwa kuwa mimi nimeridhika sana mwelekeo wa Bajeti hii sioni sababu ya kutaja kwake kwani kwa binadamu yeyote mwenye akili njema asingelikuwa na la kusema ila kuwapa idhini ya matumizi ya fedha hizo zote, ingawa mimi ninaomba kuhusu kupandishwa kwa bei ya *coil* ya mbu.

Naomba sasa niwaombe Mawaziri wetu wa pande zote za Muungano kwa kufanya kwa makusudi kuyapitia maamuzi yetu ya busara kuangalia tena uwezekano wa kuzungumza ili kiwango cha hisa za mgao wa fedha angalau uongezwe kiwango cha asilimia angalau 6.4.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu mdogo, sasa natamka rasmi kuunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja.

MHE. SAMWEL M. CHITALILO: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Baraza lote la Mawaziri na hasa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji. Kwa kusema kweli hotuba hizi mbili zimepokelewa kwa vifijo na vigelegele na wananchi wangu wa jimbo langu la Buchosa wanatoa shukrani nyingi sana kwa Wizara zote mbili, hasa pale Waziri wa Fedha ulipoona umuhimu wa kuondoa kodi ya maendeleo kwa Watanzania wote. Wazo langu ni kutaka kumwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kubinafsisha kitu chochote mie sikatai, lakini kuna mambo mengine lazima tuangalie kuhusu mikataba ya madini, lazima iangaliwe upya.

Jambo lingine ni kutaka kubinafsisha shirika la elimu *supply*. Shirika hili liangaliwe kwa undani kabla ya kubinafsisha kwa utafiti wangu shirika hili halina hasara na wale halisababishi hasara yoyote.

Kuhusu mipango ya kutaka kuendelea na hoja ya kutaka kuibinafsisha *Bank* ya Wananchi *(NMB). Bank* hii ndiyo *bank* inayostahili kuendelea kutumiwa na wananchi. Hakuna haja ya kuunda *bank* nyingine wa ajili ya wakulima, wafugaji na wavuvi. Majukumu yote haya ipewe *NMB* ambayo iko kila pembe ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawatakia kazi njema katika juhudi ya kutaka kulikomboa Taifa hili dhidi ya umaskini unaonyemelea Taifa letu kila kunapokucha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili asilimia mia moja.

MHE. ZAKIA H. MEGHJI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi hii. Katika kuleta hoja ya kukuza utalii na kupunguza ughali katika mahoteli yetu ili tuvutie watalii, wakae siku zaidi uchumi nilieze kuwa kuna kodi nyingi sana katika hoteli zetu mfano ukiwa na baa ndani ya hoteli inabidi uwe na leseni, mgahawa, duka na kadhalika. Hii inawafanya wenye hoteli kuweka bei ya juu ya nyumba hotelini, ili kufidia kodi/leseni hizi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kuwa wakate leseni moja tu. Huwa wanakata leseni ya *TALA* na kwa kweli kwa upande wa leseni hii ingetosheleza. Isipokuwa leseni ya *gaming (Casino)* walipie.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru hili likizingatiwa katika *winding up* yako ya Bajeti hii.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niwapongeze watoa hoja wote wawili, kimsingi Bajeti hii ni nzuri sana.

Napenda pia nitamke kwamba naunga mkono hoja hii. Ninatoa shukrani za pongezi nyingi hasa kwa kuwaondolea wananchi kodi ya maendeleo. Kodi ilikuwa na lengo zuri, lakini ulipishaji wake uligeuka kero na wananchi waliichukia kodi. Aidha, matumizi ya kodi hayakuwa yakizingaita lengo. Shukrani sasa wote tumefarijika, amani itatawala.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu kila Wilaya kuwa na zao moja la biashara na moja la chakula. Hili liangaliwe kwa makini, kwani mfano, Wilaya ya Muleba inazalisha chai kwa wingi, Muleba Kaskazini tu na kahawa kwa Wilaya nzima kama zao la biashara, sasa tuchague nini? Maana Kusini chai haistawi. Lakini sisi tatizo letu ni soko nataka kujua utaratibu wa soko ukoje?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja hizi napenda pia nitamke yale ambayo siyaungi mkono.

Kwanza, kuongeza kodi katika dawa ya mbu na vyandarua, siungi mkono. Malaria ni ugonjwa unaoongoza kwa kuua idadi kubwa ya Watanzania. Hao ni wazalishaji wa nchi hii uchumi unalegea. Panapokuwepo na wagonjwa wengi wa Malaria wanaoumia kuuguza ni akina mama. Hawa akina mama wafikiriwe kupunguziwa mzigo wa kuuguza kwa kuondoa kodi katika vyandarua na dawa ya mbu.

Watanzania pia wanaolipia huduma ya afya Serikali inawapunguziaje mzigo badala ya kuwakinga na Malaria Serikali inataka watu wake waugue! Aidha, vifo vingi vya wananchi, wengi ni watoto na watoto ni taifa la kesho. Natamka kwamba kodi hii iondolewe.

Mheshimiwa Spika, pia siungi mkono uongezaji wa kodi katika simu kutoka asilimia 5 hadi asilimia 7, hivi wakulima wangu wa kule Muleba Kaskazini, hawana haki ya mawasiliano? Mawasiliano ni haki ya msingi ya kila raia, kuongeza kodi ni kuwanyima haki wananchi. Sasa hii ni kuondoa uzuri wa hii Bajeti maana ni Bajeti ya wanyonge. Hii ni historia. Sasa kodi ya mawasiliano ya simu iwe ndogo anayomudu kila mmoja. Nchi haitakwenda mbele haraka ikijijengea matabaka kiunjanjaujanja kama hivi.

Mheshimiwa Spika, mimi natamka wazi kwamba kodi ya simu kutoka asilimia 5 mpaka 7 ifutwe.

Tatu, siungi mkono kuona pensheni inawabagua wale ambao bado wanaishi bila kuwekwa katika orodha eti walilipwa mkupuo. Huu nao ulikuwa mtazamo uliofaa wakati ule lakini leo ni mtazamo hafifu, inawezekanaje wanaoishi wasilipwe sheria iletwe tuibadilishe.

Katika msingi huo huo, pensheni iendelee kuongezwa hadi ifikie kima cha chini, hakuna mtu anayeishi kwa 20,000/= kwa mwezi bado ni kidogo mno. Aidha, ilipwe kwa miezi 3 badala ya miezi 6 ni mingi mno.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kuwapongeza Wabunge wanne wa CCM walioshinda hivi karibuni katika uchaguzi mdogo.

Vile vile niwapongeze Waziri wa Fedha, Manaibu Mawaziri wa Fedha, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, watalaam wote walioshiriki kuanda bajeti hii murua sana bila kumsahau Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Katibu Mkuu wake na Wataalam wote.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2003/2004 inaendelea kuipongeza kwa jinsi ilivyojielekeza katika kutatua na kuondoa kero za wananchi zilizokuwa zinakwamisha juhudi zao za kupiga vita umaskini na kujiletea maendeleo. Kufutwa kwa kodi ya maendeleo na kuondolewa kwa msururu wa kodi ndogo ndogo katika Halmashauri zetu umetoa nafuu kubwa kwa wananchi wa kawaida na hasa kuwafikiria mama vijijini, kwani vikodi vya kuku wawili, watatu ama mboga mboga za majani, vitumbua vya mama lishe vilikuwa kero na adha kubwa sana kwa akinamama vijijini.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo itaondoa sana unyanyasaji wa wananchi na hasa akinamama na wakulima wadogo wadogo vijijini uliokuwa unafanywa na baadhi ya watendaji waliokuwa wanakusanya kodi baadhi walikuwa miungu watu.

Changamoto iliyopo mbele yetu ni kufanya maamuzi haya mazuri na Bajeti hii inayomjali mkulima na wananchi vijijini itekelezeke badala ya kutuburudisha sisi humu ili wananchi waweze kuona *impact* ya ubora wa Bajeti hii inayosifiwa na wananchi wa hali zote za maisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetamka kuwasaidia mikopo wafanya biashara ndogo ndogo hasa akina mama ambao masharti ya mabenki kwa ni magumu sana kuwawezesha kupata mikopo hiyo kupitia fedha za kudhamini mikopo ya sekta hiyo ya wenye shughuli ndogo ndogo za kibiashara *(Small and Micro enterpries).*

Mheshimiwa Spika, ni vema usimamizi wa mfuko huu uwe makini ili wengi zaidi vijijini na mijini waweze kunufaika. Vile vile kutokana na umuhimu wa mfuko huu itafaa sana endapo masharti, taratibu na matumizi ya mfuko huu yatatangazwa mapema iwezekanavyo kwenye kikao hiki hiki cha Bajeti.

Napenda kupongeza juhudi za sasa zinazofanywa na jeshi letu la polisi katika kupambana na ongezeko la uhalifu, bali fedha zilizotengwa kwa idara ya polisi ni kidogo sana labda kama takwimu hizi zimekosewa kweli kima hiki hakionyeshi kama kweli tuko *serious enough* kulisaidia Jeshi hili kukabiliana na wimbi la uhalifu.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kuona umuhimu kuboresha sera na mipango iliyowekwa ili kupata maendeleo endelevu katika kupunguza umaskini hususani katika sekta za kilimo barabara, afya, elimu na maji na uboreshaji wa huduma vijijini pamoja na kufufua kilimo.

Mheshimiwa Spika, mikakati yote hii mizuri inafaa kuwa ovyo ovyo kiasi cha wahasibu wengi kushidwa hata kutoa. Matumaini kuwa tutakumbuka methali isemayo...

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Serikali imeona umuhimu wa kuwapelekea wakulima zana za kilimo na mashine za kukamua mazao mfano alizeti, pamba na kadhalika basi vema mashine hizo zipelekwe kwenye mikoa ambayo inalima mazao hayo kupunguza gharama za kusafirisha. Nimesoma Bajeti bali sijaona mahali ilipotoa msamaha kwa kutoa huduma bure kwa akinamama wajawazito na wazee ambao wengi wao hupotea maisha kwa kukosa fedha za matibabu.

Mheshimiwa Spika, nazidi kuipongeza Serikali kwa kuongeza kima cha chini cha posho ya kila mwezi wa wastaafu pamoja na pensheni. La msingi zaidi ni lile la kusogeza huduma ya malipo ya wastaafu mikoani kweli hili mtakuwa mmefanya la maana kwani wengi wao hufa kabla ya kupata hizo fedha kutokana na huduma mbaya ya malipo haya na umbali huko vijijini. Kama kweli Serikali imepokea kilio cha wakuu wa Wilaya kuwapelekea *Other Charges (OC)* zao moja kwa moja kwani Makatibu Tawala wengi wa Mikoa waliwanyanyasa sana kwa kucheleweshe fedha zao kwa kupunguza kiasi kilichotumwa ninaomba na taasisi zingine zipelekwe vivyo hivyo mfano hospitali za mikoa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusisitiza tena umuhimu wa kutekeleza kwa vitendo yaliyomo kwenye Bajeti yenye matumaini makubwa kwa wananchi wetu.

Hivyo basi naunga mkono Bajeti hii Mungu awabariki waliondaa kwa kujali maoni ya Wabunge kwa asilimia kubwa.

MHE. KIJAKAZI KHAMIS ALI: Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, sina budi kuipongeza hoja hii ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya, wote kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru Serikali kwa mapendekezo ya kufuta ushuru unaotozwa kwenye zao la samaki ambalo ni zao la kilimo, kifungu cha 58, ukurasa wa 66.

Mheshimiwa Spika, kufutwa kwa ushuru ni faraja kwa wakulima kwani mapato ya mkulima ni madogo na utaona mapato yenyewe ni ya msimu, mara nyingi mazao ya wakulima yanakumbwa na maradhi mbalimbali au kushuka kwa soko na kadhalika. Kwa hiyo, uamuzi huu wa Serikali wa kufutwa kwa ushuru ndio umewasaidia wakulima.

Ukurasa wa 41, kifungu cha 4 Serikali inatambua matatizo yanayowapata wafanyabiashara wadogo, wakiwemo wanawake katika kupata mikopo kwa ajili ya shughuli zao za kibiashara na Bajeti ya mwaka 2003/2004 imetenga fedha kwa ajili ya kudhamini mikopo kwa sekta hiyo ya wenye shughuli ndogo ndogo za kibiashara. Mfuko huu utasimamiwa na Benki Kuu kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO)*. Utaratibu na masharti ya matumizi ya Mfuko huo yatatangazwa baadaye. Mimi naipongeza Serikali kwa hatua hii na pia Bajeti hii kutekelezwa. Maandalizi yakikamilika haya ya kupatiwa mikopo kwa yovyote iwafikie wananchi walio wanyonge huko Vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, napenda kuunga mkono hoja zote mbili za Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuungana na wenzangu katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambayo imewasilisha katika Bunge mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia hotuba hiyo sina budi kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya, ambao wamechaguliwa hivi karibuni katika uchaguzi mdogo. Napenda kuwaambia ya kwamba, wakaribie ili tuweze kulijenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imepata sifa kubwa sana kwa kitendo cha kuwaangalia wastaafu kwa kupandishwa kima cha chini cha pensheni kuwa Sh. 20,000/=. Kiwango hiki si kidogo kwani hapo siku za nyuma baadhi ya wastaafu walikuwa wanapata Sh. 5,000/= kwa mwezi. Baadhi ya wastaafu baada ya kupata taarifa hiyo wameanza kutupigia simu za kuipongeza hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limenifanya niipongeze hotuba hii, ni kitendo cha kuondoa kodi ya maendeleo. Kodi ya maendeleo ilikuwa kero kubwa sana kwa wananchi. Ingawa malipo hayo yalikuwa Sh. 3,000/=, lakini kutokana na umaskini, hizo pesa ni nyingi sana ambapo wananchi wa Vijijini hawawezi kulipa.

Mheshimiwa Spika, vile vile naipongeza hotuba hii kwa kueleza bayana juu ya uzuiaji wa usafirishaji wa *Tanzanite* ghafi isiyokatwa na kutaka *Tanzanite* yote inayouzwa nje iwe imekatwa. Kitendo hiki cha uzuiaji wa *Tanzanite* isiyokatwa kitaiwezesha Serikali kuongeza pato kutokana na madini hayo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Bajeti hii imeweka bayana na limewafurahisha watu wa sehemu zote za Muungano, ni kuhusu kutenga asilimia 4.5 kwa mapato yatokanayo na misaada *(Program Assistance)* ya nje, kwa ajili ya kusaidia Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Baada ya kuteuliwa Tume ya pamoja ya fedha ya Muungano, sasa malalamiko kuhusu kero hiyo yatapungua na Waheshimiwa Wabunge, watapumua kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Ukumbi wetu wa Bunge umekwishajaa kabisa baada ya kuongezeka kwa Waheshimiwa Wabunge wapya, ambao wamechaguliwa hivi karibuni katika uchaguzi mdogo. Ni jambo la faraja kabisa kuona Bajeti hii ya mwaka 2003/2004 imetenga shilingi milioni 5,000/= kwa ajili ya kuanza kazi ya kujenga Ukumbi mpya wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni sote tumeshuhudia wimbi la majambazi ambao baadhi yao wamewaua vijana wetu wa Polisi. Kitendo cha Jeshi letu la Polisi kukabiliana na majambazi hayo kimetupa moyo kabisa na hatuna budi kulipongeza jeshi hili. Silaha nyingi za majambazi hao zimekamatwa. Kutokana na jeshi hilo kutengewa Sh. 70,786/= milioni katika Bajeti ya mwaka 2003/2004, kutalifanya jeshi letu la Polisi lifanye kazi kwa ujasiri.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya na mimi naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuipongeza Serikali, kwa hotuba iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze na ushuru wa vyandarua na dawa ya mbu. Ninaiomba Serikali iangalie upya ushuru wa vifaa hivi kwani ninavyojua mimi ni kwamba, homa ya malaria inaendelea siku hadi siku na kuna Watanzania walio wengi bado wanashindwa kununua vyandarua na hukimbilia kwenye dawa ya mbu. Vipi leo tupandishe ushuru kwenye dawa ya mbu na vyandarua, hatuoni kwamba ni kuwakatisha tamaa Watanzania kwa ununuzi wa vifaa hivi? Ninaiomba Serikali iondoe ushuru wa vifaa hivi.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imetenga fungu la fedha la Askari Polisi kwa ajili ya vitendea kazi. Lakini ushauri wangu ni kwamba, askari wetu hawa tunawaona jinsi wanavyojitahidi kupambana na kazi ngumu usiku na mchana hasa pale wanapoweza kupambana na majambazi na kulinda usalama wa raia na mali zao. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iliangalie jeshi hili ili mishahara yao iweze kulingana na kazi ngumu wanazokabiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuona kilimo ndiyo uti wa mgongo na kuweka fungu kubwa la fedha kwa ajili ya kilimo cha kisasa. Ninaomba Serikali isimamie hilo tatizo, liko kwenye utekelezaji wa hicho kilimo chenyewe. Kama usimamizi utakuwa mzuri, basi Watanzania wataweza kuondoa umaskini kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

MHE. DR. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba zao nzuri, ambazo zimewathibitishia Watanzania ya kwamba, tuendako kuna mwanga wa kuaminika.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii pia kuwapongeza Watendaji wote wa Wizara hizi mbili, kwa jitihada zao za kutayarisha hizi hoja mbili.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kuwasilisha salaam za wanawake na maskini wa aina zote kutoka Morogoro. Wao wanaipongeza Serikali kwa kuwaondolea kero ya kodi nyingi ambazo zilikuwa zinawakosesha raha, pamoja na kuwacheleweshea maendeleo yao. Sasa wanaahidi kufanya kazi kwa bidii ili waweze kupunguza umaskini wa kipato ambao umekithiri kati yao, kwani sasa wanaweza kufanya biashara ndogo ndogo, pamoja na kulima bustani za mboga mboga kwa ajili ya biashara bila bughudha ya mlolongo wa kodi za Vijiji na Halmashauri. Lakini wanaomba mpango huu wa kuondolewa na kufutwa kwa kodi ndogo ndogo, pamoja na kodi ya maendeleo, uwe ni wa kudumu na siyo wa Bajeti ya mwaka 2003/2004 tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuondolewa kwa kero ya kodi nyingi ikiwepo kodi ya maendeleo, ningependa kuiomba Wizara ya Fedha iangalie suala la malipo ya wastaafu na wafiwa.

Mheshimiwa Spika, inakuwaje raia anastaafu halafu inachukua muda zaidi ya mwaka kabla hajalipwa marupurupu yake? Wengi wanahangaika sana, wanatumia hata akiba zao haba kwa ajili ya gharama ya kufuatilia mafao hayo Hazina. Hivi haiwezekani kukawepo na mfumo wa kuwalipa katika kanda zetu nne? Pia Wizara husika ibuni mbinu za kuweza kuwatenganishia wastaafu mafao yao ili wanapostaafu tu walipwe ili kuwapunguzia kero ya safari za Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kero nyingine ni ile ya wafiwa hususan wajane na yatima, kufuatilia mafao ya marehemu ndugu zao. Hili ni tatizo kwa hiyo liangaliwe namna ya kulitatua kwani linawaongezea wafiwa machungu pamoja na kujisikia kunyanyasika baada ya ndugu zao kufariki.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupendekeza kwamba, ni vema Wizara ya Fedha, ingetoa orodha ya kodi zilizoondolewa kimaandishi katika kijarida kwa lugha ya kiswahili ili wananchi waweze kujisomea na kuelewa nini haki yao. Hii itampa mwananchi ufahamu wa huu mfumo mpya wa kodi, pamoja na kuondoa uwezekano wa kujenga mianya ya rushwa kwa watendaji wasio waadilifu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningependa kuwapongeza sana wale wote waliohusika kwa njia moja ama nyingine, kutayarisha Bajeti hii nzuri ambayo imewahakikishia wananchi kwamba, Serikali yao inawajali na ipo tayari kuzishughulikia kero zote zinazowanyima raha na kuzuia maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, Serikali imekiri mapungufu katika suala zima la kukuza uchumi kama vile madeni makubwa inayodaiwa Serikali, viwanda hafifu bila ya kuwa na teknolojia za kisasa lakini suala kubwa ni *tariff* ya umeme.

Mheshimiwa Spika, suala hili haliwezi kutukomboa kwenye uchumi wetu kama tutaendelea hivi tulivyo sasa. Kuna haja ya Serikali kulitazama kwa mara nyingi ili viwanda vyetu viweze kukidhi haja na ushindani wa kibiashara katika masoko ya Afrika Mashariki na dunia yote.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii ni chanzo kimojawapo cha kukuza uchumi wetu. Kuna maeneo ambayo hivi sasa yamekwishaiva kwa shughuli hizo, lakini Serikali haikuweka mikakati ya upendeleo ili kuharakisha shughuli hizo ili zianze kuingiza mapato nchini kwa mfano, barabara ya kutoka Horohoro - Tanga - Pangani na Bagamoyo, ambapo Serikali karibu itaanzisha Hifadhi ya Taifa ya Saadani.

Mpango wa MMEM wa mwaka 2002 wa kuongeza idadi ya watoto watakaoandikishwa darasa la kwanza, matokeo yake ni kwamba, hivi sasa tayari kuna mrundikano mkubwa wa wanafunzi waliofaulu kuingia madarasa ya sekondari lakini hawana nafasi kutokana na uhaba wa shule za sekondari na walimu hivyo hivyo kwa wanafunzi wa sekondari kwenda vyuo vikuu. Kuwe na mpango wa haraka kwa ajili ya kuleta ufumbuzi wa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, suala la ubinafsishaji wa viwanda vilivyonunuliwa na Watanzania, toka vichukuliwe mpaka hii leo havizalishi na bado wanadaiwa madeni ya ununuzi wa viwanda hivyo. Nashindwa kufahamu ni vigezo gani vinavyotumika kuvirudisha na kupewa wengine au pale walipoweka thamani wao wenyewe walijua hali halisi ya viwanda hivyo au walishauriwa na nani kuweka thamani hizo walizoweka? Nashauri Serikali itafute ufumbuzi wa suala hili ili viwanda hivi vifanye kazi na viongeze mapato katika mfuko wa nchi ili kuboresha maisha ya wananchi kwa kupata ajira na kuboresha familia zao. Naomba tupewe maelezo ya kina juu ya namna Serikali itakavyolishughulikia suala hili la viwanda vilivyokwama katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Mheshimiwa Waziri la kufuta kodi kwa Taasisi mbalimbali, juu ya magari yenye injini zenye uwezo zaidi ya *c.c. 3000* linatutia mashaka sisi Wabunge wenye magari ya mkonga, ambayo yana uwezo wa zaidi ya *c.c. 4000* kwamba, tutaanza kulipa ushuru.

Mheshimiwa Waziri, nakushauri usianzishe malumbano na Waheshimiwa Wabunge, bila ya kuwa na jambo la msingi. Nashauri ufute kauli yako juu ya suala hili na wataalam wako wa *TRA* watakufikisha pabaya, kama huamini basi tutakumbushana siku itakapofika. Ahsante sana.

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika hotuba ya Bajeti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi za dhati kwa Bajeti yenye mwelekeo mzuri. Pamoja na pongezi hizi, ningependa kupata ufafanuzi ufuatao:-

(i) Baada ya kutoa na kufuta kodi ya maendeleo na Serikali kuahidi kutoa ruzuku badala yake na ili ufuatiliaji uwe rahisi; je, ruzuku hiyo sasa itakuwa kiasi gani kwa Bajeti ya mwaka 2003/2004 na inaonekana chini ya kasma ipi yaani Wizara na kasma husika ili tuweze kufuatilia kwa karibu? Nimetafuta

kwenye *Volume II (Ministerial)* na *Volume IV* sijaona. Hivyo, nitafurahi kwa ufafanuzi, kwa manufaa ya wananchi na Halmashauri zetu.

(ii) Kwenye Bajeti ya mwaka 2002/2003 tulitenga fedha shilingi bilioni saba kwa ajili ya kununua Ndege ya Rais. Ningependa kujua kama ndege hiyo sasa imeshafika nchini. Je, tumeinunua kutoka nchi na kampuni ipi na gharama halisi sasa imekuwa kiasi gani? Mwaka huu fedha hizo zimetengwa chini ya kasma ipi?

(iii) Kwa vile *radar* tuliyoinunua imekwishafika na kufungwa, ningependa kujua gharama halisi sasa ya *radar* hiyo na tumelipa kiasi gani hadi sasa na je, fedha hizo kama bado tunalipa, mwaka huu tumetenga kiasi gani na zinaonekana chini ya kasma ipi? Nimepitia kasma zote lakini sikuweza kupata majibu halisi na kwa bahati mbaya hotuba yako haikusema chochote juu ya mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati na kwa kweli japo kimsingi sina tatizo na Bajeti, pamoja na niliyoyasema kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani, nitaunga mkono iwapo nitapata majibu ya kina.

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Spika, zaidi ya niliyochangia kwa mdomo ningependa kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mashirika yaliyobinafsishwa hayafuati masharti ya mikataba ya mauzo, hasa kuhusu kuboresha uwekezaji, teknolojia na kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kitu kimoja kibaya ni kwamba, katika sehemu nyingi wananchi hata wale wenye ujuzi na uzoefu katika kazi husika, hawapewi nafasi katika uongozi wa mashirika bali hupewa nafasi katika ngazi za chini au nafasi za kazi zinakuwa za vibarua tu. Hivyo, Serikali iwe macho katika kutoa vibali vya kazi *(Work Permit)*

Mheshimiwa Spika, hakuna ufuatiliaji madhubuti ama na *PSRC* au Wizara Mama kuhusu utekelezaji na uendelezaji wa mashirika hayo. Zaidi ya mashirika ambayo yanabinafsishwa kupitia *PSRC*, ipo haja ya kutupia macho ubadilishaji wa mmiliki katika sekta binafsi. Mfano ni kama pale *Amboni Limited* walipouziwa mashamba kama vile *Lugongo Estate, Tungi Estate*, Kwalaguru na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kupunguza utegemezi na ugumu wa kutekeleza malengo kwa kiwango kinachotarajiwa. Kama walivyoeleza Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili, hali ya kutekeleza Bajeti kwa asilimia 45, aya ya 28(i) ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuwa chini ya lengo kutokana na kuchelewa kukamilisha masharti ya mikopo kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika, aya ya 20, ukurasa wa 16 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni hali ya hatari. Aidha, misaada na mikopo kutoka nchi za *Paris Club* kupatikana kwa asilimia 36 tu, aya ya 24, ukurasa wa 19 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni miongoni mwa viashiria vinavyopelekea haja ya kuchukua hatua thabiti kupunguza utegemezi na kuwa na mpango kamambe wa kujitegemea katika hali endelevu kama ilivyosisitizwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika aya ya 40 ya hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa hatua za kufanya marekebisho kwa ushuru wa muda *(Suspended Duty)*, aya ya 52(i) ili kuchochea matumizi ya malighafi za hapa nchini pamoja na kuwezesha ushindani wa haki kwa bidhaa zinazotoka *EAC* na nje ya *EAC*. Mfano hai ni magunia ya mkonge ambayo yanapata ushindani mkubwa kutoka kwa magunia ya *jute*. Zaidi ya viwanda vya magunia kukwama kuuza mazao yake na kupata hasara, bidhaa za viwanda vya mkonge kama vile *flume tow*, zinachomwa badala ya kutumika hivyo kuleta hasara kwa wenye viwanda na kukosesha ajira kwa wananchi wengi hasa akina mama ambao ndio wanaochambua na kukusanya *flume tow*. Nashauri Serikali ilitazame hili kwa makini hasa kwa kuzingatia kwamba, wauzaji wa magunia ya *jute* wanapewa ruzuku *(subsidy)*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kupunguza kodi ya ardhi kutoka Sh. 600/= kwa ekari hadi Sh. 200/= kwa ekari, Ibara ya 31, ukurasa wa 21 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri

wa Fedha, bado kodi hii inaonekana kuwa juu hasa kwa wawekezaji katika mashamba makubwa ya mkonge ambao wanalazimika kuacha wazi *(fallow)*, sehemu kubwa ya ardhi yao kwa mujibu wa utaratibu wa mkonge ambao unalimwa kwa mzunguko *(rotation)*. Nashauri Serikali ilitazame kwa undani tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, napenda kuendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waheshimiwa Manaibu Waziri, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu na Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Makatibu Wakuu, Ndugu G. Mgonja na Ndugu P. Lyimo na Watendaji wote wa Hazina, kwa kazi nzuri wanayoifanya na hii inaonyeshwa dhahiri kwa Bajeti waliyoiandaa kitaalam na kumlenga Mtanzania aliyeko Kijijini.

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia kumwomba Mheshimiwa Waziri na wataalam wake kwamba, msiruhusu kupunguza kodi mliyoiweka kwenye mafuta ya chakula kutoka nje. Wananchi wameshawaamini kwa kazi nzuri mnayoifanya. Kwa hiyo, msiitie doa kwa kudanganywa na wafanyabiashara, ambao lengo lao ni kupata faida na kumuacha mkulima wa nchi hii akiteseka.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuomba masharti magumu yaliyoko kwenye Mfuko wa *Import Support* yalegezwe na wazawa wafaidike na Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Bajeti nzuri waliyoiandaa bado hapa nchini tuna upungufu mkubwa wa Wahasibu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atunishe fungu kubwa katika kuwasomesha wengi ukizingatia ya kuwa Serikalini wako wachache. Halmashauri, Miji Midogo kama Kibaha na Kondoa, Manispaa na Majiji, hawana wataalam wa fani hii ya Uhasibu, kumbuka ya kwamba, Hazina inapeleka fedha nyingi sana kwenye Halmashauri zetu. Kamati yetu ya *LAAC* mpaka sasa imeshagundua kwamba, fedha nyingi sana hazitumiki ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa leo naomba niishie hapa. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. MWADINI ABASS JECHA: Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kupunguza umaskini, hii ni dhana pana sana na inahitaji kufanyiwa uchambuzi yakinifu na wa kina kabisa.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba, kuongezeka kwa uchumi wa Taifa kutoka asilimia 5.7 mwaka 2001 kufikia asilimia 6.2 mwaka 2002 inaonyesha kuna mafanikio.

Mheshimiwa Spika, lakini kukua huku kwa uchumi wa Taifa hakujaleta tofauti ya maisha kwa Mtanzania wa kawaida. Mtanzania wa kawaida anashindwa kumudu milo mitatu kwa siku na pia anashindwa kuwapatia watoto wake huduma bora za elimu, afya na kadhalika. Hali hii inatisha na haiendani na dhana nzima ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aone kwamba, ukuaji wa uchumi wa Taifa unawafariji Watanzania walio wanyonge.

MHE. FATMA SAID ALI: Mheshimiwa Waziri Spika, ingawa nilichangia kwa mazungumzo, lakini kuna maeneo mawili napenda unisaidie kufafanua. Maeneo hayo ni yafuatayo:-

Moja, utendaji wa watumishi *TRA* Zanzibar. Wafanyabiashara (Mlandege) wengi wanasikitika na ushuru mkubwa unaotozwa Bandarini Zanzibar, hivyo, baadhi ya wafanyabiashara hao wamehamia Tanga na wanaendelea na biashara zao. Je Bandari ya Tanga ina unafuu gani kuliko Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, pili, usindikaji wa mafuta, karanga, mawese na kadhalika, wananchi wa Mikoa ya Pwani, Lindi, Tanga, Morogoro na Zanzibar waliitikia wito na wakapanda minazi mingi sana ambayo imezaa nazi kwa wingi. Tatizo lao ni soko la nazi hizi. Je, kwa nini hatuongezi zao la nazi katika orodha ya mazao yatakayoshughulikiwa na mitambo mipya ya kisasa ya kusindika mafuta?

Hivi sasa mafuta ya nazi tuna *import* kutoka India yanakuja kwa ajili ya kula na pia kujipaka mwilini.

MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninakushukuru kwa kutoa fursa ya kuchangia hoja Bungeni kwa kuzungumza au kwa maandishi. Nami ninachangia kwa maandishi hotuba ya Bajeti ya mwaka 2003/2004 ya Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa hotuba yake nzuri, ya kitaalam na yenye kugusa mioyo ya Watanzania wote. Kitendo cha kufuta kodi ya maendeleo na kutafuta vyanzo vingine vya fedha, ni kitendo ambacho Watanzania wa karne hii hawatasahau. Inakumbukwa kwamba, Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, alipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu Waziri Mkuu, aliwafutia kodi akina mama na akina mama Tanzania nzima wakampenda kweli kweli, sasa Mheshimiwa Basil Mramba na Serikali yako mmefuta kodi ya maendeleo kwa wanaume pia. Kwa nini wewe na Serikali yako msipendwe?

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, kodi ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi mwaka 2000/2001 ilipandisha kodi toka Sh. 2,000/= hadi Sh. 4,000/= . Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, akafanya maandamano Wilayani Moshi, kupinga ongezeko hilo la kodi ikashushwa hadi Sh. 3,000/= karibu Tanzania nzima. Hakika kodi hiyo ilikuwa ni kero.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwa nguvu zangu zote kuwa cheti cha kuzaliwa mtoto *(Birth Certificate)*, kitolewe bure na kipatikane kwenye hospitali, zahanati na vituo vya afya vya Serikali Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, malipo ya cheti hiki ni madogo sana. Lakini Watanzania wengi wanakuwa hawajajiandaa kwa malipo hayo wakati mtoto anapozaliwa. Hata mtoto anapozaliwa na hadi mtoto anaenda shule, mzazi bado akilini mwake hakumbuki kukipata cheti hicho mpaka anapojikuta, ama mzazi au mtoto anakwenda Mahakamani kupata *affidavit*.

Mheshimiwa Spika, mama mzazi wa mtotoanapompeleka mtoto *clinic*, Serikali iwasisitize Madaktari kumwuliza mzazi cheti cha kuzaliwa mtoto. Hata anapoandikishwa darasa la kwanza, Serikali kwa kutumia Waraka wake, wawalazimishe Walimu kuwauliza wazazi cheti cha kuzaliwa mtoto, kama mzazi hana cheti hicho alazimishwe kwenda kwenye hospitali au *clinic* au zahanati ya karibu kupata cheti hicho ndipo mtoto aweze kuandikishwa chekechea au darasa la kwanza. Kero hii ikiondolewa Serikali itatukuzwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Spika, napongeza na kuunga mkono hoja. Ninapenda kuchangia na kushauri yafuatayo:-

Katika Kitabu cha Mpango wa Maendeleo Barabara ya Mwanza-*Shinyanga Boarder* - Tinde - Isaka, pamoja na kwamba wanaobomolewa nyumba wamelipwa, lakini katika ukurasa wa 84 - 85 Mradi huu haukupangiwa fedha. Hii ni mbaya hasa kama Mradi huu hautatekelezwa. Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga na Tabora wanashangaa kwa nini barabara hii imerukwa na kuanzia Nzega - Shelui. Nitashukuru kupewa majibu maana kila siku tunaambiwa mkataba utawekwa sahihi tangu Aprili, 2003 na Serikali ilidai fedha zimepatikana tangu 1999 kutoka *EU*. Je, fedha hizi zimehamishiwa kwenye miradi mingine?

Nazipongeza juhudi za Jeshi la Polisi katika kupambana na uhalifu nchini. Ninaomba Serikali ione namna gani ya kuboresha vitendea kazi, pamoja na uwezekano wa kununua *helicopter* mpya. Ya sasa hivi ni ya zamani mno. Sijui tunangoja mpaka iharibike. Pia nashauri Serikali kununua *helicopter* mpya ya *engine* mbili ya Serikali kwa matumizi ya Wakuu wa Serikali, pamoja na Rais kwa kutembelea sehemu ambazo hazina viwanja vya ndege.

Natoa pongezi jinsi Serikali itakavyolishughulikia suala la ukwepaji kodi kwenye suala la mafuta ya dizeli. Utaratibu wa sasa utasaidia sana na huenda utaongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la njaa ni kubwa sana, naomba Serikali ijiandae kikamilifu. Katika Jimbo langu Kata karibu zote hazina chakula na uzalishaji wake umeshuka zaidi ya asilimia 20 ya pato la kawaida. Nimeona hata mikoa yote haina chakula.

Vile vile ninaomba Serikali izidi kuimarisha *SIDO* ili kuendelea kuboresha ukuaji wa viwanda nchini, pia Mfuko wa kuwakopesha wafanyakazi wadogo wadogo uzidi kutunishwa maana hata fedha za awali walizopewa bado wanazo na Mfuko unazidi kukua.

Kuhusu Mfuko wa *Exchange Rate* ni vyema Serikali ione namna gani inaweza kudhibiti tatizo hili, maana *Exchange Rate* inapopanda huleta madhara makubwa sana kwa matumizi hasa mafuta ya dizeli ambayo hupandishwa kila kitu. Mimi sielewi pamoja na biashara kubwa ya madini inakuwaje thamani ya shilingi inazidi kupanda? Hivi fedha hizi hazisaidii kupunguza mfumko wa *Exchange Rate*. Naomba kodi ya dhahabu iweze kuboreshwa kwa kweli *royalty* ya asilimia 3 ni ndogo mno, angalau ipandishwe ifikie asilimia 10 au zaidi. Kwenye Mikataba ya Madini suala la mazingira halikuzingatiwa na kwamba, Serikali itawezaje kukarabati mazingira yanayoharibiwa na shughuli za uchimbaji?

Fedha za maendeleo hazikugawiwa kutokana na idadi ya watu. Fedha tulizopewa Mkoa wa Shinyanga hazilingani na idadi ya watu. Mimi nilidhani baada ya sasa, fedha zitatolewa kulingana na wingi wa watu.

Nashauri mashirika ambayo yana sura za kibenki *(Quasi Financial Institution)*, kama vile *PPF, NSSF, LAPF, Insurance Companies*, yasimamiwe kama *Commercial Banks* ili kulinda kufilisika ambapo athari zake zinasababisha walioweka fedha zao humo kutolipwa. *NIC* sasa hivi inaonekana hawana udhibiti mkubwa hasa katika uwekezaji na ujenzi wa majumba. Inatakiwa uwekezaji wa kwenye majumba uwe unadhibitiwa na Benki Kuu.

Nazidi kuunga mkono hoja ila naomba maelezo kuhusu barabara ya Mwanza - *Shinyanga Boarder* - Tinde - Isaka, mbona haimo kwenye Kitabu cha Maendeleo cha mwaka 2003/2004, ukurasa 84 na 85. Ahsante sana.

MHE. TEMBE K. NYABURI: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Waziri wa Fedha, Manaibu wake na wataalam wote, kwa kuandaa bajeti nzuri inayolenga kumkomboa Mtanzania. Naanza kwa kuunga mkono hoja. Naipongeza Serikali kwa kufuta kodi ya maendelo. Pamoja na kuunga mkono hoja napenda kushauri m aeneo kadhaa ili yafanyiwe marekebisho kama ifuatavyo:-

1. Hotuba ya Bajeti haikuongelea ushuru utakuwaje wa zana za kilimo kama matrekta na kadhalika kutoka nje, yataingia bura kama ilivyokuwa au vipi? Nashauri zana za kilimo ziingizwe bure ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa mazao ya kilimo.

2. Mheshimiwa Spika, Serikali ishirikishe kikamilifu viongozi Wilayani juu ya mipango inayokusudiwa kutekelezwa kabla fedha kupelekwa Wilayani. Mfano bajeti iliyopita ya 2002/2003, Mheshimiwa Mramba, alitenga shilingi zaidi ya bilioni moja kusaidia wafanyabiashara wadogo wakiwemo vijana nchini kote, lakini tulipoongea na kuwaambia viongozi Wilayani waombe fedha hizo zisaidie vijana kama ilivyokusudiwa, wengi walisita na kueleza hawana taarifa kuhusu hilo. Mapema mwanzoni mwa mwaka huu wa 2003, Waziri aliwaambia Waandishi wa Habari na iliandikwa magazetini kuwa fedha zilitengwa lakini hakuna Wilaya iliyoomba fedha hizo na kwamba, kama zisingeombwa basi zisingetumika na kusubiri kupangiwa vinginevyo bajeti hii ya 2003/2004. Hii ni mipango mibovu, ni bora viongozi Wilayani washirikishwe kwa kutaarifiwa mipango inayowahusu.

3. Serikali kupitia *BOT* ifanye mazungumzo na vyombo na asasi za fedha nchini kwa lengo la kushusha kiwango cha riba ya mikopo ikibidi iwe sawa kote *(Flat Rate)*, ili kuwezesha wananchi wengi

kukopa na kukuza uzalishaji. Viwango vya riba vya sasa viko juu sana havishawishi wengi kukopa. Hili ni muhimu sana.

MHE. DR. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kuipongeza Wizara kwa bajeti nzuri na yenye matumaini.

Katika suala la kuondoa umaskini na kupunguza kero za wananchi, wakati umefika wa kusaidia miundombinu ya usafirishaji kwa njia ya reli na ujenzi wa magati katika maziwa yetu. *Hopefully* mwaka 2004 lifikiriwe hili.

Mheshimiwa Spika, kuongeza kodi kwenye *air time* itakuwa na *effect* kwa watu wengi. Katika karne hii ya sayansi na teknolojia, wakati simu Tanzania ni ghali, *at present* zinaweza zionekane ghali zaidi kwa kuongeza kodi hii. Sijui mantiki ya kuongeza kodi, kwa *radio call* ni nini?

Mheshimiwa Spima, ninashukuru na kuutakia utekelezaji mwema wa Bajeti hii. Hongera Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Kamishna wa *TRA* na Watendaji wote.

MHE. OMAR S. CHUBI: Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wa Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, kwa kutoa bajeti ya ukombozi kwa wananchi hususan wa vijijini, kwa jambo la faraja la kufuta kodi ya maendeleo ambayo ilikuwa kero kubwa kutokana na mtindo ambao ulisababisha wananchi wakimbie nyumba zao na kujificha msituni na kuhatarisha maisha yao. Mungu awabariki Mawaziri hao na Watendaji wao, kwa ushauri mzuri ambao umezaa matunda hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mheshimiwa Kigoda, nampongeza kwa juhudi zake za kusimamia kidete shughuli za ubinafsishaji wa mashirika ya umma, kama ilivyotamkwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000. Nijuavyo suala la kurekebisha uchumi ni kubwa kwani anayeweza kufanya kazi bila makosa ni Mwenyezi Mungu tu. Kinachotakiwa sasa Mheshimiwa Waziri, ajitahidi kufanya marekebisho pale ambapo Waheshimiwa Wabunge, wametoa ushauri ili kuondoa kasoro hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mheshimiwa Mramba, ambaye ni kiongozi mwenye hekima na mwadilifu, namwomba afuatilie tatizo la mgogoro wa wafanyakazi wa Shirika la Bima wapatao zaidi ya mia tatu, ambao wanateseka licha ya wafanyakazi hao kufanya kazi kwa uadilifu kwa vipindi vya mwaka mmoja hadi miaka thelathini. Waathirika ni pamoja na mimi mwenyewe, ambaye shauri langu liko kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima anatamba kwa kuwa yeye ameteuliwa na Mheshimiwa Rais, hakuna mtu ambaye anaweza kumbishia. Ushahidi kuhusu ubabe huo unaweza kuthibitishwa hata na baadhi ya Wabunge waliopo humu ndani, ambao wamefanyiwa mambo ya kudhalilishwa.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi hivi karibuni Mkurugenzi huyo kaiomba Bodi ilipomaliza muda yeye na marafiki zake walio mba wastaafishwe halafu wafanye kazi kwa mkataba mpya, wakati wanajua kuwa Shirika la Bima liko kwenye *Receivership*. Kilichofanyika ni kwamba, waliostaafishwa ni baadhi ya Mameneja ambao na marafiki zake na Wakurugenzi ambao ni marafiki zake. Mkataba mpya ni wa miaka mitatu 2003 - 2006. Marupurupu waliyojipangia ni kama ifuatavyo: Mkurugenzi Mtendaji mshahara Sh.4,000,000 kwa mwezi, nyumba Sh.300,000 kwa mwezi, simu ya mkononi Sh.250,000 kwa mwezi, walinzi watatu. Mkurugenzi wa Fedha na Utawala mshahara Sh.3,500,000 kwa mwezi, Walinzi wawili, simu ya mkononi Sh.200,000 na kwa upande wa Mameneja Viongozi mshahara ni Sh.2,900,000 kwa mwezi, simu Sh.150,000, nyumba na walinzi kama ilivyo hapo juu.

Mheshimiwa Spika, endapo Mheshimiwa Waziri, hatafuatilia masuala ya wafanyakazi 300 na masuala yangu, najiandaa kufanya maandalizi ili kukwamisha kifungu cha 50 ili kuishinikiza Serikai itoe maamuzi na kuchukua hatua kwa taasisi ambazo zina uozo. Niko tayari kuthibitisha uozo huo kwa tarifa yenye kurasa 30.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote niliyoyaeleza, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa Bajeti nzuri iliyojali wanyonge kwa mujibu wa Sera za CCM na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 1995 na 2000. Pamoja na uzuri wa bajeti hii ya 2003/2004 kuwa nzuri, nataka ufafanuzi wa maelezo kwa hoja zifuatazo:-

1. Mheshimiwa Spika, sikuona Barabara ya Minjingu-Babati-Kondoa-Mtera-Iringa katika vitabu vya Bajeti taanza kushughulikiwa lini kujengwa kwa kiwango cha lami? Kwa nini barabara hii haipewi umuhimu wake, ni mtu gani anapindisha Mradi huu?

2. Kama barabara hii imeanza kushughulikiwa, Serikali itoe maelezo kwamba ni hatua zipi zimefikiwa? Zitajwe.

3. Serikali imetamka wazi suala la kufuta kodi ya maendeleo kwa nchi nzima kwa sababu za msingi za kero na bughudha zingine. Hii ni hatua nzuri ya kuchangia kuondoa umaskini, lakini kodi nyingine ambayo nayo ni kero sana ni kodi ya mifugo zizini. Bado kuna badhi ya Halmashauri zinatoza kodi ya mifugo zizini. Bughudha au kero yake ni kwamba, kama hakuna tamko la Serikali la kufuta kodi hii yafuatayo yatajitokeza:-

(i) Wafugaji wanaoishi katika maeneo yenye kodi zizini watahamia au kuhamishia mifugo eneo lisilotoza kodi;

(ii) Mifugo kujaa sehemu moja tu ya nchi na kusababisha uharibifu wa ardhi;

(iii) Sehemu zingine kukosa maziwa, mbolea, nyama, kilimo cha plau na kuzidisha umaskini nchini; na

(iv) Pia kuwafanya wafugaji wengi sana kuwa wakimbizi badala ya wakazi wakikimbia kodi hii.

Hivyo basi, kwa nini kodi hii isifutwe ili wananchi wote wafugaji wafaidike? Tafadhali fafanua hilo.

MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA: Mheshimiwa Spika, ninaiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Lakini juu ya suala la Benki ya Uvuvi hizo pesa zitatolewa kwa masharti gani? Je, Wabunge watahusishwa hasa zile sehemu zenye uvuvi? Ziwa Tanganyika lina samaki wengi sana na dagaa, lakini uvuvi hafifu wa zana duni umechangia umaskini kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma. Ninaomba Mkoa wa Kigoma upewe kipaumbele katika mikopo hiyo ya uvuvi. Kuhusu mbolea kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, inaonekana mbolea hiyo itasambazwa kwa mikoa mingine ikitokea huko huko kwa mfano, Kigoma wafanyabiashara watafuata Rukwa. Kwani itakuwa na bei nafuu. Ombi, kusiwepo upendeleo wowote bali iwe sawa sawa na mikoa mingine.

MHE. STANLEY H. KOLIMBA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono Bajeti ya 2003/2004. Bajeti hii imejielekeza kutatua kero za wananchi wetu na kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi wa nchi hii ili hatimaye kupunguza umaskini.

Hata hivyo, yapo mambo yanayotakiwa kuwekwa bayana ili kusaidia utekelezaji wenye ufanisi. Wafanyabiashara au wasafirishaji wa mbolea na pembejeo zingine watangazwe kwenye vyombo vya habari kwa madhumuni ya kufahamika na kuonekana kama wamepewa dhamana ya mikoa au wilaya zilizopangwa. Makubaliano yafikiwe baina ya Serikali au chombo cha Serikali kilichoteuliwa kusimamia utekelezaji wa mpango huu na wafanyabiashara hao, juu ya bei za mbolea katika mkoa au wilaya zinazohusika. Ikiwezekana bei za mbolea kwa kila wilaya zitangazwe bayana baada ya kufanya *costing* au gharama.

Uongozi wa Wilaya upewe uwezo wa kuhoji au kutoa taarifa ya ukiukwaji wa mpango mzima wa kufidia mbolea na pembejeo kwani huko nyuma Serikai ilitoa nafuu ya *VAT* kwenye zana za kilimo lakini matokeo yake bei ya zana za kilimo ziliendelea kupanda au kubakia na bei zile zile tu.

Serikali itumie wafanyabiashara kila inapowezekana, wanaotoka katika wilaya zinazohusika kwa kudhaminiwa na Halmashauri zao za wilaya.

Kila wilaya ifanyiwe uchunguzi wa ratiba ya matumizi ya mbolea ili kuondoa kasoro ya kufikisha mbolea katika kipindi tofauti na mahitaji.

Mfuko wa mikopo midogo midogo kwa kila mkoa au wilaya uundiwe Kamati ya Kusimamia maombi ya mikopo hiyo, pamoja na Shirika la *SIDO* kuwepo, mara nyingi shirika hili halifikishi mikopo hiyo wilayani, walengwa wapo wilayani, wavuvi, wakulima, wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ni kubomoa viambaza vilivyopo katikati vinavyozuia mkulima, mvuvi wa mwisho kupata msaada au mkopo unaomhusu. Je, uwezo huo Serikali inao?

Aidha, Wizara ya Kilimo imewandaa vipi Maafisa wake wa Kilimo na Mifugo kupokea mabadiliko haya makubwa katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

MHE. PETER KABISA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo jana, mimi sina matatizo na hoja ya Waziri wa Fedha ya Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2003/2004, bali nina maombi rasmi na mahsusi kuhusu pensheni ya *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa kuanzisha *NSSF*. Bahati mbaya sana *through an oversight*, Bunge lilikubali bila kuangalia kwa uangalifu na kwa makini kifungu au vifungu vinavyohusu kumlazimisha mchangiaji na pensheni hiyo kwamba, hatapata pensheni yake mpaka akitimiza miaka 55 ya kustaafu ndipo apewe pensheni hiyo.

Mheshimiwa Spika, nina imani kwamba, Wabunge tuliteleza kidogo kwa kupitisha Muswada huo bila kubaini athari za kipengele au vipengele hivyo. Kinachojitokeza sasa kutokana na ukosefu wa ajira, upunguzaji wa wafanyakazi kwenye Serikali, mashirika ya watu binafsi na kadhalika, ni kwamba, wananchi wengi wenye umri wa kati ya miaka 35 -45 wanaachishwa kazi na kuambiwa kile kidogo walichochangia kwenye Mfuko wa Pensheni yao hawawezi kukipata mpaka wafikapo umri wa kustaafu wa miaka 55 au wataendeleza mchango wao wa pensheni pale watakapopata kazi au ajira nyingine na kwa wanawake wakipata *maternity leave benefits*, ndio kabisa hawarejeshewi michango ya pensheni.

Mheshimiwa Spika, sote tunajua uhaba na uchache wa kupata kazi. Hawa wananchi hawana matumaini ya kuajiriwa tena. Kilichobaki ni wao kujiajiri na kutafuta riziki yao upya. Kwa maana hiyo, wanahitaji fedha za kuanzisha ajira mpya ya kujiajiri na kadhalika na hivyo kuhitaji hizo fedha ndogo walizochangia kwenye Mfuko huo wa Pensheni. Vinginevyo hawa wananchi wanakuwa na hasira na kuona kwamba, Serikali hiyo hiyo ya Chama Cha Mapinduzi, inayohubiri kuondoa umaskini, kero na dhuluma zisizo za lazima, inamwekea ngumu mwananchi kupata haki yake ili aendeleze maisha yake na ya familia yake pale anapoachishwa kazi.

Mheshimiwa Spika, mwananchi ambaye hana uwezo wa kujitafutia ajira kwa visenti vyake alivyo navyo *NSSF*, kwa sababu viko benki, atajiingiza kwenye matatizo yasio ya lazima. Atakuwa na afya mbaya na hata pengine kujiingiza kwenye nambo ya ulevi wa pombe, madawa ya kulevya na hata zinaa na kuambukizwa na Ukimwi, hatimaye kufariki. Hizo fedha zilizoko *NSSF* nani atazitumia?

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kwamba, kama tunazungumzia suala zima la kumnasua mwananchi huyu, ku mwondolea kero mwananchi huyu, kumtendea haki mwananchi huyu na kadhalika, basi hiyo sheria au kipengele cha Mfuko wa *NSSF* kifanyiwe marekebisho haraka sana ili mwananchi yeyote yule anayeachishwa kazi kabla ya kufikia miaka 55, yaani kati ya miaka 35 hadi 50, basi apewe hicho kilichopo kwenye mchango wake na wa muajiri wake, ili fedha hizo zimsaidie kuanza maisha mapya kwa kujiajiri mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati kabisa, kipengele hicho kiondolewe kwa vile nina imani kwamba, Serikali haikuwa na lengo la kumpa kero wala kumnyanyasa au kumtesa huyu mwananchi, mpiga kura wake. Naomba sana Serikali itekeleze ombi hili la kurekebisha kipengele hicho mapema iwezekavyo kwenye Mkutano wa Bunge wa Oktaba, 2003.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

MHE. ANATORY K. CHOYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono bajeti hii, pamoja na kuipongeza Serikali kwa uamuzi wa busara wa kufuta kodi ya maendeleo. Baada ya hatua hii ya Serikali kufuta kodi sasa ni zamu ya wananchi kutumia muda huu kwa ajili ya kufanya kazi za kujiondolea umaskini.

Maana halisi ni kwamba, kwa sasa wananchi hawatahama majumbani, hawatakwepa Watendaji na kujificha ili kufidia pengo litakaloachwa wazi baada ya kufutwa kwa kodi, nashauri fidia ifuate idadi ya watu katika Halmashauri husika.

Katika hotuba ya bajeti ukurasa wa 75 napendekeza msamaha wa kodi ya vyombo na taasisi uendelee kutolewa kwani vyombo hivyo ni muhimu kwa wahisani pamoja na Wabunge. Ushauri huu nautoa kwa lengo la kutaka kuzuia mgongano unaoweza kujitokeza kati ya Serikali, Wabunge na Wahisani, wakati wa utekelezaji huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SHAMIM P. KHAN: Mheshimiwa Spika, naanza kuwapongeza Mawaziri wote wawili, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, kwa kutuletea bajeti nzuri, *down to earth*, itakayotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri kama ifuatavyo:-

1. Nashukuru suala la *gender budgeting* limeanza kujitokeza, lakini bado tunahitaji *dissegregated data*. Mikutano yote ya Kimataifa inadai hivyo (me na ke) - wakulima, *engineers, ICT*, walemavu na kadhalika.

2. Ruzuku kwa watu wenye ulemavu. Majuzi tu tulielezwa na Viongozi wa Chama Cha Viziwi Tanzania *(CHAVITA)*, kwamba wanapewa shilingi laki moja na nusu hadi laki mbili na nusu kwa mwaka; je, zinatosha pamoja na ufinyu wa bajeti?

3. *Irrigation* ni jibu sahihi la kuepukana na umaskini, njaa, maradhi na kadhalika, *a hungry man is an angry man*. Tuelekeze nguvu zetu hapo, twendeni kwa awamu. Kwa mfano, *TASAF* wamekisaidia kijiji kimoja cha Songea Vijijini hivi sasa. Walikuwa wamevuna magunia 10 ya mpunga kwa eka, sasa magunia 30.

4. Vyuo vya Maendeleo ya wananchi 58, mtufikirie vimeanza kuonyesha matumaini pamoja na ufinyu wa bajeti. Hivi sasa mkivitembelea mtashangaa. Baadhi ya Halmshauri za Miji na Wilaya husika zinasaidia. Lakini nahali ambapo hakuna vikao vya Bodi za Vyuo, sokomoko linaanza.

5. *Training Fond for Tanzania Women (TFTW)*, Mfuko huu uliokuwa unafadhiliwa na *Canadians* umesitishwa kama vile *HESAWA*. Ingawa tunashauriwa tutenge fedha katika bajeti zetu za kawaida, fedha hazitoshi, hivyo Serikali itawaelimisha lini wanawake? Hatuwezi kutegemea *NGOs only*.

6. Ninaipongeza Serikali kwa kufuta kodi ya maendeleo.

Mheshimiwa spika, mwisho, naunga mkono hoja zote mbili mia kwa mia.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili, kwa hotuba zao nzuri na za kina wakati wakiwasilisha bajeti ya mwaka 2003/2004. Hotuba zinaonyesha kwamba, ni shirikishi kwa vile zimezingatia sana masuala yanayowagusa wananchi wa kawaida katika maisha yao ya kila siku.

Kodi ya maendeleo ilikwishaonekana kuwa ni kero. Mbali na gharama kubwa zilizotumika katika ukusanyaji wa kodi, bado malengo yalikuwa hayafikiwi kwa vile wananchi wengi walikuwa wakikwepa kuilipa pamoja na kwamba wengine walikuwa na uwezo wa kuilipa, hii ilitokana na kwamba, madhumuni ya kodi hii yalikuwa hayaonekani, kwani wananchi walitarajia kuona shughuli za maendeleo zikifanyika katika maeneo yao. Badala yake fedha iliishia katika matumizi ya ofisini tu.

Kufutwa kwa kodi za baiskeli, ushuru wa mazao na kadhalika, kama vyanzo vya mapato ya Halmashauri, ni ukombozi kwa wananchi na bughudha nyingi zitapungua. Suala la ajira ya Watendaji wa Kata na Vijiji pia ni suala linalostahili pongezi kwa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Hii itapunguza mzigo mkubwa uliokuwa ukibebwa na Halmashauri za Wilaya.

Tumaini langu ni kwamba, Serikali itaweka viwango vya elimu vitavyomuwezesha mtu kuajiriwa kama Mtendaji wa Kata, Kijiji, lakini pia kuwapa mafunzo juu ya kazi zao na masharti ya kazi. Watendaji wa Kata shughuli zao ni pamoja na kulinda amani katika maeneo husika, kwa hiyo, ni lazima waishi katika maeneo yao ya kazi. Ni matumai kuwa watapewa maslahi ya kutosha ili waweze kuishi katika maeneo yao.

Ili kumuwezesha Mtendaji wa Kata/Kijiji kufanya kazi yake vizuri, ni muhimu sana kuwa na sehemu inayofaa kufanyia kazi. Sehemu nyingine Ofisi za Watendaji ni za kujibanza tu katika Ofisi za CCM, nyumba za watu binafsi na kadhalika. Nashauri Halmashauri nazo ziwe na mpango wa kujenga Ofisi za Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza kima cha chini cha pensheni ni jambo linalostahili pongezi kwa Serikali na Chama Cha Mapinduzi. Hata hivyo, inaelekea kwamba, Serikali imeziba masikio kwa pamba, inapuuzia malalamiko ya wastaafu waliochukua fedha yao kwa mkupuo, ambao badhi yao walilazimishwa kuchukua mkupuo kwa vile malipo yao ya pensheni yalikuwa madogo sana.

Wazee hawa wanaomba Serikali iwafikirie ili waweze nao kuendelea kulipwa pensheni kwa vile bado wanaendelea kuishi baada ya muda uliokuwa umekadiriwa wa miaka kumi na mbili na nusu au miaka kumi na tano.

Kama hoja ni kwamba, kwa mujibu wa sheria hawana haki ya kudai kulipwa, mimi naona hoja hii haina uzito. Wazee hawa kwanza si wengi, maana wengine wameshaaga dunia, lakini pia ni sehemu ya jamii ya Watanzania ambao walilitumikia Taifa kwa uaminifu sana. Naomba Mheshimiwa Waziri, unieleze kama suala hili hulijui na kama unalijua kwa nini unalipuza? Kama sheria ndiyo hoja, ni sheria ngapi zimerekebishwa ili kukidhi mahitaji ya wakati uliopo lakini pia kuondoa kero na malalamiko katika jamii. Wengi wa wazee hawa ni Waasisi wa CCM iliyoahidi hali za wazee! Sasa ni vipi Serikali ya CCM inaziba masikio juu ya kilio hiki?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naiunga mkono hoja.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo na ninaahidi kuwapa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, pia Manaibu Waziri wote na Watendaji Wakuu, waliosaidia kwa kiasi kikubwa, kusomwa kwa bajeti iliyofurahisha umma, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, Watanzania walio wengi walichoshwa na kero kubwa ya kodi ya maendeleo. Kufutwa kwake ni kufungua njia ya maendeleo kwani walio wengi walikuwa hawafanyi kazi kutokana na

tishio la kodi. Napenda nimhakikishie Waziri kuwa kutakuwa na maendeleo hasa kwa mazao ya kilimo kwani watalima bila woga na Watanzania wanao uwezo wa kulima na kupata ziada ya kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nitoe mchango wangu hasa juu ya ubinafsishaji. Shughuli ya ubinafsishaji ni nzuri na ndiyo inayoifanya bajeti iungwe mkono na wengi baada ya mashirika mengi kubinafishwa na kuanza kutoa faida badala ya hasara. Mimi naungana na Sera ya Chama chetu cha Mapinduzi, zoezi hili liendelee ila tunapotaka ufafanuzi Wizara iwe wazi kutoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kulinda viwanda na mashirika yaliyobinafsishwa, ni vyema Serikali iwalinde wote walionunua mashirika yetu, juu ya bidhaa toka nje, tuagize tu baada ya kuona bidhaa inayozalishwa hapa nchini haitoshelezi kwani walionunua mashirika hayo wanapata hasara ya watu kutoka nje kuingiza nchini bidhaa kwa njia zisizo halali.

Mheshimiwa Spika, mfano ni Kampuni ya Sigara wamekuwa wakilalamika juu ya uingizwaji wa sigara na kuua biashara za bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Vile vile viwanda vya sukari kama wanaweza kuzalisha sukari ya viwandani waruhusiwe ili wakulima wa miwa wapate bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni viwanda vya nguo navyo vilindwe ili kukuza zao la pamba, ambalo linataka kutoweka hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Ndugu Sanare, kwa kazi kubwa aliyoifanya *TRA* na ndiyo maana leo hii tumeweza kufuta kodi na pia baadhi ya sehemu kupata maendeleo, vile vile nimpongeze Ndugu Kitillya na Ndugu Luoga, kwa kuteuliwa na Rais, kwa kazi ambazo nina imani wataendeleza.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niunge mkono hotuba zote kwa asilimia mia moja na niahidi ushirikiano wa kufanikisha malengo yaliyolengwa. Ahsante sana.

MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja yenyewe. Ingawa imekwishaelezwa kasoro ya kutamka kwamba sio vyema kusema ile sehemu inayotolewa kwa SMZ kama ni kuisaidia Bajeti ya Serikali hiyo. Nami nashauri kwamba, tamko hilo lisijitokeze tena kwani fedha hizo hazikutengwa kutokana na ombi la Serikali husika, isipokuwa limetokana na ufuatiliaji wa kuweka uwiano wa kweli kwa Muungano wa Serikali zetu mbili.

Mchango wangu mwingine ni kuitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kusaidia kuondoa kasoro zinazoendelea hivi sasa kwa SMZ kuendelea kushuka kwa mapato yake, hasa yale yanayotokana na kodi ya *VAT* kwa Bandari ya Zanzibar. Kuipa SMZ mgao wake wa asilimia 4.5 hausaidii wananchi walio wengi. Fedha hizo ni kwa Serikali yenyewe tu, huku wananchi wanaendelea kuelemewa na umaskini, kutokana na kukosa kazi bandarini, pamoja na kuondolewa kwa viwanda ambavyo vilikuwa vinasaidia sana maisha ya watu, pamoja na kupunguza umaskini kwa jumla. Tatizo kubwa ambalo linaongeza pengo kwa Serikali zetu mbili ni suala la uchumi usio na uwiano na haionyeshi kama ipo nia ya kusaidia na kukuza uchumi wa nchi kwa jumla. Nashauri mkazo sasa uelekezwe huko kuliko kujifaharisha kwa mchango huu wa asilimia 4.5.

Wananchi wa Zanzibar walikuwa na viwanda mbalimbali vya Bakhresa, Magodoro, vitambaa, na kadhalika. Vyote sasa havipo. Ni mambo ya kuangaliwa sana. Serikali ya Muungano inayo nafasi nzuri ya kusaidia misingi kama hii kuwepo, kwani ikiwa na nguvu za kutosha wananchi wake watazidi kuelimika, kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano na Zanzibar kweli ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MHE. RHODA L. KAHATANO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao nzuri, zinazoleta matumaini mema kwa maendeleo ya nchi yetu. Hata hivyo, ninayo machache ya kuchangia.

Ninaipongeza Serikali na wananchi kwa kukua kwa uchumi na kushuka kwa upandaji bei hadi kufikia asilimia 4.3, ingawa sina hakika watu wa vijijini wamebadilisha vipi maisha yao toka kwenye umaskini uliokithiri kuwa na hali bora zaidi sasa.

Ninapenda kuzungumzia viwanda vidogo vidogo. Suala la kukuza viwanda vidogo vidogo kwa maendeleo ya Watanzania ni muhimu sana wakati huu ambao uwekezaji umepamba moto na hauna huruma. Sekta hii itiliwe mkazo. Fedha za kudhamini mikopo ya sekta ya watu wenye shughuli ndogo ndogo zidhibitiwe. Fedha hizi zitawasaidia wananchi kuondoa umaskini, kuendeleza viwanda vidogo vidogo, kujifunza kufanya biashara, kuweka akiba ya chakula na kadhalika. Udhibiti wa Mfuko huu ni muhimu sana. Fedha zisaidie wananchi katika mikoa yote wasije faidika watu wa mikoa maarufu tu au watu wachache wajanja kama ule Mfuko wa Pembejeo.

Sekta ya elimu ni muhimu sana kuleta maendeleo katika nchi yoyote ile. Ninaipongeza sana Serikali yetu kwa kujitahidi kuboresha madarasa na madawati kwa shule za msingi, bado wanafunzi ni wengi sana katika madarasa, kiasi ambacho walimu hawamudu kuwafundisha vizuri na hii inasababisha vijana wengi wanapomaliza darasa la saba kuwa hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu. Badala ya kuwa wasomi, ni tofauti na wenzao ambao hawakwenda shule hata kidogo.

Ninashauri watoto waandikwe wanaotosha darasa linaloweza kufundishika kulingana na madarasa yanayojengwa. Walimu waendelee kutiwa moyo wa kufundisha, waandaliwe vizuri vyuoni. Wakaguzi wapewe vitendea kazi. Hata kama fedha za kuongeza miaka 10 badala ya saba iliyoshauriwa na Wabunge wengi, naomba miaka ile miwili ya mwisho vijana wakaziwe kufundisha elimu ya ufundi. Iwe kama ilivyokuwa *Post Primary* iliyokufa kwa kukosa fedha. Wanafunzi walioendelea na ufundi baada ya darasa la saba wanasaidia sana vijijini kujenga nyumba, kutengeneza vifaa vya nyumbani (useremala), kuchoma vyuma na kutengeneza matangi ya maji. Kundi hili linaweza kujiunga na *VETA* na wanaobaki wakaweza kujiunga pamoja na kutumia Mfuko wa *SIDO.*

Nashukuru kwa kutilia mkazo kwenye elimu ya sekondari, kutenga fedha zaidi kwa lengo la kuwasaidia vijana wanaofaulu kujiunga na sekondari, ambao wazazi au walezi wao hawana uwezo.

Mheshimiwa Spika, naomba EWW isitupwe kabisa, ina mchango mkubwa kwa maendeleo ya vijiji vyetu. Fufua kisomo chenye manufaa kwa kupata fedha kidogo kuchapisha vitabu. Hawa ndio wazalishaji, watatoa malighafi kwa watu wenye elimu ya juu na wenye viwanda vikubwa.

Katika sera ya uwekezaji, naomba Serikali kwa makusudi mazima, itumie ardhi yetu kuwashirikisha wazawa kuwekeza na wageni. Mgeni asipewe ardhi kama hawa Watanzania wazawa. Wako wengine wanaoitwa wazawa ambao kukitokea mashaka kidogo ya usalama nchini hata Uchaguzi Mkuu tu wanaikana nchi. Ni wazawa lakini wanaweza kukimbia, mimi nasema wale wasio na pa kwenda, iwe mvua liwe jua wako hapa, hawa ndio wapiga kura wa sisi sote. Kumpa mtu mgeni ardhi ni mwiko. Nadhani benki uliyoisema, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, inawahudumia wawekezaji wananchi wasio na pa kwenda. Uwekezaji wa kilimo awepo Mtanzania mzawa.

Benki itakayoanzishwa iwe chombo kitakacholeta matumaini kwa watu wasiohesabika kwenye uwekezaji hali wao ndio wenye nchi. Hawa wakishirikishwa tunazidi kujenga nchi na kuzuia mambo ya kuja kugombea ardhi mbele ya safari. Hata wawekezaji wageni watakuwa na hakika na kazi zao kwamba zitadumu.

Kuwalipa Watendaji mishahara hadi vijijini, nadhani kazi itafanyika vizuri sasa. Kwa kuwa hata kodi imefutwa, wataweka nguvu zao kwenye miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Nawapongezeni.

Utaratibu wa *Cash Budgeting*, ni mzuri kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha kama ulivyosema mwenyewe. Naomba kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Fungu la Balozi zetu nje miezi iwe zaidi ya mitatu. Kwa kuwa wako mbali na nyumbani wanapata shida nyingi hata za makazi tu. Wakipewa kwa miezi sita kwa utaratibu utakaoweka, waweke kwenye akaunti kupata faida ili waweze kukopesha. Udhibiti ni muhimu sana hapa. Saidia Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba *P.A.Y.E.* iangaliwe upya, watumishi hawana kitu wasingang'anywe zaidi kile kidogo. Tusisababishe mianya ya toa kidogo upate huduma.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuwaongezea wastaafu shilingi 20,000/= toka shilingi 12,000/=, kutoa unafuu wa kodi kwa vitu vinavyoingizwa nchini, pamoja na kufurahia kwa kupunguza kodi ya *VAT* kwa Mashirika ya Dini, naomba Serikali iwafutie kodi watu wanaoendesha shule za binafsi, vifaa vya shule visitozwe kodi.

Mheshimiwa Spima, naunga mkono hoja zote mbili.

MHE. FRANK M. MUSSATI: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha na Mipango na Ubinafsishaji na wafanya kazi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri sana mliyoifanya mwaka 2002/2003, ambayo imesababisha uchumi wa Taifa letu kukua kwa kiasi kisichopungua asilimia 6.

Ni ukweli usiopingika kuwa kilimo bado ni uti wa mgongo wa uchumi wetu na hasa kwa maeneo ya vijijini. Lakini, pamoja na kutambua umuhimu wa kilimo, Serikali katika Bajeti yake ya 2003/2004, haijaeleza kwa uwazi mambo yafuatayo:-

(i) Itahamasisha vipi taasisi za fedha kuwasaidia wakulima na wavuvi wadogo kupata mikopo ya kuendeshea shughuli katika nyanja hizo hasa baada ya Serikali kujitoa katika shughuli za biashara;

(ii) Itawawezeshaje wakulima/wavuvi wadogo kupata pembejeo na zana za kazi kwa mfano, matrekta ya bei nafuu?; na

(iii) Itawasaidiaje wakulima, hususan, wakulima wa tangawizi katika Kata ya Kalela, Jimboni Kasulu Mashariki, kupata soko la tangawizi ambayo wamekuwa wakiilima kwa miaka mitatu mfululizo bila kupata mununuzi wa zao hilo?

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikihimiza uuzaji wa bidhaa nje ya nchi na usindikaji wa mazao ya kilimo lakini haijaweka mazingira ya kuwawezesha wananchi kufanya hivyo kwa mfano, Mkoani Kigoma, pamoja na kutangaza eneo hilo kuwa eneo la *EPZ*, bado Mkoa hauna umeme wa kuaminika na hivyo wawekezaji wa ndani na nje ya nchi hawavutiwi kuwekeza Mkaoni humo, pamoja na Mkoa kuwa na *potentiality* kubwa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima ichukue hatua za makusudi kusimamia uboreshaji wa haki ya miundombinu, hasa umeme, barabara za lami kati ya Bukoba na Kigoma na Kigoma na Tabora na uboreshaji wa Reli ya Kati - DSM/Kigoma, ili kuinua hali ya uchumi wa Mkoa huu na hivyo kuuwezesha Mkoa wa Kigoma kuchangia zaidi katika Pato la Taifa. Endapo miundombinu hiyo itawekwa na kuimarishwa au kuboreshwa, ni hakika hali ya kilimo, viwanda na uchumi kwa ujumla, itakuwa nzuri zaidi.

Pamoja na maoni yangu hayo, ninaunga mkono hoja za Wizara zote mbili kwa asilimia mia kwa mia. Ninawatakia kila la kheri.

MHE. MWANAIDI HASSAN MAKAME: Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kutoa shukrani zangu kwa kupata fursa hii ya kuchangia kwa maandishi. Mimi ninaziunga mkono hotuba hizi mia kwa mia.

Ninatoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Serikali kwa masuala yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuondoa kodi ya maendeleo, jambo ambalo lilikuwa ni kero kubwa kwa wananchi.

Pili, naipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa upendeleo katika ugawaji wa fedha kwa maeneo yanayolenga kupunguza umaskini hasa kilimo, elimu, afya, barabara na maji na yale yenye kuongeza kipato, hasa kwa njia ya ajira.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninawampongeza Mawaziri wote wawili, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, kwa pamoja na wataalam wao wote, kwa jinsi walivyotayarisha hatuba hizi vizuri.

MHE. MOSSY SULEIMANI MUSSA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuzipongeza Wizara zote mbili, kwa kutuwasilishia sisi Wabunge, kwa niaba ya wananchi, bajeti ambayo imekamilika na kuonekana kwamba, kweli imepangwa na wataalam wenye sifa zote za Mipango na Fedha. Lakini si hilo pekee, pia kuonekana kwamba, upo ushirikiano mzuri baina ya Wizara zote mbili.

Mheshimiwa Spika, katika demokrasia ya ushindani wa Vyama si mara nyingi Wapinzani kuunga mkono hoja ya Chama Tawala hata pakiwa na uzuri au ufanisi ulioonyeshwa, lakini Bajeti ya mwaka huu wa 2003/2004, imeungwa mkono hivyo imeonyesha wazi kwamba, Wizara hazikucheza bali kazi imefanyika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mramba na Mheshimiwa Kigoda, kama kweli watataka heshima ya bajeti hii na wao binafsi wabaki na sifa hizi zinazoendelea kupewa kwao, basi hoja ya kilimo cha umwagiliaji maji *(Irrigation Plan)*, kitekelezwe kama kilivyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nieleze wazi siri kubwa ya bajeti hii kupendwa na kupewa sifa na kila mwananchi ni kwa sababu imegusa mikopo kwa wakulima na wavuvi ambao ni asilimia 80 ya walengwa hivyo, naomba utekelezaji ufanane na maandiko.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hizi kwa kuwa zina wataalam wa kutosha na wenye sifa zote na kwa kuwa mianya ya ukwepaji kodi imeonekana, basi utumike utaratibu wa nguvu zote kuziba mianya hiyo kwani tutafaidika kuongeza mapato yetu ya ndani na hapo *automatically* uchumi wetu utapanda kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, wapo walipaji wazuri wa kodi walioandikishwa *TIN*, hivyo kila wakati wa bajeti tuwe tunapewa idadi yao kama wameongezeka au kushuka. Bajeti hii imegusa Watanzania wote kwani tume kuwa tunapokea simu kutoka Zanzibar za kuipongeza bajeti hii, kwa vile mgao wa asilimia 4.5 umeelezwa bayana kuipa nguvu bajeti ya Zanzibar.

Huu ni wakati wa vitendo na wala sio maneno baada ya mipango, mimi nashauri Waheshimiwa Wabunge wote, wapatiwe eka 200 za mashamba kila mmoja na wawezeshwe kuyaendeleza kisasa ili uwe mfano wa uzalishaji kwa wazawa na pia vijana wengi watapata ajira ndani ya mashamba hayo, sambamba na mikopo kwa wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, sitasahau kauli ya Balozi wa Japan, wakati anatuaga alisema: “Uchumi wa Tanzania utakua kwa kasi kama nguvu za Watanzania zitaelekezwa kwenye kilimo hasa cha kisasa”. Hivyo Watanzania tutimize wajibu wetu chini ya muongozo wa wataalam wa Wizara ya Fedha na Mpango.

Ushauri wangu mwingine ni kuondoa kodi kwenye *spear* zote za zana za kilimo, ili kutoa motisha kwa kuikuza sekta hiyo. Kwa upande wa uvuvi lazima uvuvi wa *deep sea* upewe kipaumbele, hivyo mikopo katika sekta hiyo iwe ya namna mbili, ule wa wavuvi wadogo wadogo na ule wa wavuvi wakubwa wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, umefika wakati kuongeza mapato yetu kwa kuboresha ufugaji tuondokane na ule wa kuswaga na twende kwenye kunenepesha ndani ya matunzo na tuuze nyama nje, kwani masoko yapo tena mengi hasa *Far East* na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza sana Ndugu Sanare, kwa ushupavu wake ambao upo wazi, kwa ushirikiano wake na watumishi wenzake, kwa kutufikisha hapa kimapato na najua anakokwenda atafanya vizuri pia, hivyo tunamtakia Mungu ampe uwezo zaidi. Pia namtakia kazi njema Kamishna mpya Ndugu Kitillya.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya, hasa wale wa Chama Cha Mapinduzi, kwa kuchaguliwa kwa kishindo na kuwa pamoja nasi Bungeni, ili kutekele za Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000. Hongera sana.

Pia nawapongeza Mawaziri wa Fedha Mheshimiwa Mramba na Mheshimiwa Kigoda wa Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba zao nzuri, zenye mwelekeo wa dhamira ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, bajeti na mipango ya mwaka huu kwa ujumla wake ni ya kukomboa wananchi walio wengi nchini, wakulima, wafanyakazi, wanafunzi, wastaafu na kadhalika. Hata hivyo, napenda kuchangia kwa lengo la kuboresha na kushauri au kutaka ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Kuhusu suala la utoaji wa huduma bure kwa wasiojiweza, utaratibu huu ulikuwepo lakini utekelezaji wake umekuwa haueleweki, kwa hiyo, ni mikakati gani imepangwa kwa saa ili isiwe kero kwa walengwa? Pia naomb a Serikali itoe ufafanuzi wa mikakati iliyoiandaa katika jitihada za kupunguza bei ya nishati hasa umeme ambao bado unaathiri uzalishaji viwandani na majumbani na kuwezesha matumizi ya teknolojia rahisi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuboresha maslahi ya wastaafu, lakini rai yangu ni kwamba, utaratibu wa malipo hayo ufanyike bila usumbufu kwa vile kwa muda mrefu urasimu wa utendaji wa Ofisi ya Hazina umekuwa ni mkubwa mno na ni kero sana kwa wastaafu.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na Serikali kuona umuhimu wa kutoa motisha kwa wananchi wanaotumia nguvu kazi zao katika kujiletea maendeleo yao. Lakini naomba kupata ufafanuzi kuhusu motisha husika itakuwa ni motisha gani?

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2003/2004, imeonyesha fedha zilizotengwa kwa ajili ya kulipa mafao kwa watakaopunguzwa kazi katika sekta mbalimbali. Rai yangu ni kuwa Serikali ihakikishe kuwa watu wenye ulemavu hawapunguzwi kazi kiholela tu, kwa vile ile Sheria ya Ajira kwa Walemavu bado inawalinda lakini utekeleza ji wake umekuwa ukipuuzwa na waajiri walio wengi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kusimamia mpango wa MMEM na kufanikisha ujenzi wa madarasa 15,991 nchini. Lakini kinachosikitisha ni kwamba, ingawa nilianza kuishauri Serikali umuhimu wa kujenga madarasa yanayozingatia matatizo maalum kwa watoto wenye ulemavu kabla ya kuanza kwa mpango wenyewe, lakini hilo halikuzingatiwa. Naamini kuwa kati ya madarasa yaliyojengwa hakuna hata moja lililozingatia rai niliyowahi kuitoa kwa Serikali. Sasa hili maana yake ni nini? Kwa msingi huo watoto wenye ulemavu watakuwa bado wanaendelea kusumbuka sana katika kuipata elimu hata ile ya msingi. Hivyo, nasisitiza rai hii ifanyiwe kazi kwa vile ni moja ya kero.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo naomba ufafanuzi wa *New Canadian Initiative,* mkakati huu unasema nini ndani yake? Kuhusu Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, mkataba unaotegemewa kusainiwa hapo baadaye tuwe waangalifu na kujaribu kukwepa matatizo (vipengele) kiuchumi vilivyosababisha kuvunjika kwa umoja huu mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache, naunga mkono hoja zote mbili ya Bajeti na Mipango ya Maendeleo. Ahsante.

MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ametamka kuwa umwagiliaji mdogo wa asili utaendelezwa. Amesema pia kuwa Serikali itakamilisha mpango wa kuanzisha Benki itakayohudumia wavuvi, wafugaji na wakulima wakubwa na wakati. Aidha, amesema itaanzisha Mfuko wa kuhudumia mifugo kuanzia Bajeti hii.

Maelezo haya yote ni mazuri na hasa pale aliposema sekta za uzalishaji, hasa kilimo ambacho kinaingiza zaidi ya asilimia hamsini ya Pato la Taifa na kubeba asilimia 80 ya Watanzania, bado ni dhaifu na kinahitaji mabadiliko ya haraka.

Mheshimiwa Spika, imetamkwa katika hotuba ya Waziri wa Fedha kuwa, ipo mipango ya kuendeleza umwagiliaji wa asili. Wizara ya Kilimo na Chakula katika *scheme* yake iliyo katika *program* ya utekelezaji wa kilimo cha umwagiliaji, wameweka *priority for selecting irrigation scheme*, ambayo inatoa kipaumbele katika mambo makubwa matatu:-

Kwanza, *presence of traditional irrigation; canals* na *Weirs* - Mabanio.

Pili, *dependency of the farmers on irrigation and scarcity of rain.*

Tatu, *adequacy of irrigation water.*

Mheshimiwa Spika, kimsingi mimi nakubaliana na *priority* zote hizo. Lakini inaonyesha *scheme* hii katika *program* zake za utekelezaji aidha, Wizara ya Kilimo na Chakula haijui vijiji vilivyo na vipaumbele walivyoweka, kwa kushindwa kutembelea maeneo yote ya nchi yetu yenye *priority* zote hizo wanazozitamka ili wawe katika hali ya kuelewa vizuri kuamua kuanza kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na kanda ipi.

Kwa mfano, watu wa Kijiji cha Rudewa Gongoni katika Wilaya ya Kilosa, *depend very much on irrigation* katika kilimo chao. Kijiji hiki kina uzoefu mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji. Ni wazi hawana mabanio ya kisasa lakini mabanio yao yanayotengenezwa *locally* yapo na yamekuwa yanatumika miaka yote. *There is very high adequate irrigation water*.

Eneo linaloweza kulimwa kwa kumwagilia ni kutoka hapo Kijiji cha Gongoni mpaka Mbigiri. Hili ni eneo kubwa sana. Jambo zuri zaidi umwagiliaji wa bonde hili unatumia *gravity* na sio *pumps* kama ilivyo sehemu nyingine.

Kwa maelezo haya, nashauri Waziri wa Fedha katika majumulisho yake, akubali kumshauri Waziri wa Kilimo na Chakula, kukubali kujumlisha Kijiji cha Rudewa Gongoni katika utekelezaji wa programu ya utekelezaji wa *selected areas* katika Bajeti ya mwaka huu wa 2003/2004, pamoja na *other selected areas because all basic irrigation functions like economic function, financial function and social function have already been started to be used.* Kwa kweli kijiji hiki cha Rudewa Gongoni kinastahili na kina sifa za kuwemo katika programu ya utekelezaji ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Fedha kwa kutamka katika Bajeti kuwa gharama ya kuchimba visima zimepunguzwa. Ingawa hakusema zimepunguzwa kwa asilimia ngapi, bado kauli yake imetia nguvu sana katika kilimo cha umwagiliaji.

Matumizi ya *Tube-wells* yanaonekana hayafai kutumika kwa sababu matumizi yake na uendeshaji wake yanaonekana ghali sana. Nchi kama India, Pakistan na nyinginezo, zenye *Extensive Irrigation Networks*, mahitaji ya maji yanayohitajika kwa kumwagilia hayatoshelezi kuwawezesha wakulima *to achieve the maximum intensity of land use. Irrigatable land already developed, lies fallow because of water shortage*. Kauli ya kutamka kupunguza gharama za uchimbaji visima mimi naipongeza sana.

Mheshimiwa Spika, katika nchi nyingi *rivers supplying surface water have a marked difference between maximum and minimum annual flow*. Katika hali hii nchi hizo hutumia *Tube-wells to augment basic surface water to supplement surface canal water.* Kwa sababu *most profitable cropping pattern is unlikely to have an even profile of water demand on the year and canal system is limited to cope with peaks.*

Mfumo wetu wa *Irrigation* unategemea kwa kiwango kikubwa kujaa kwa mito. Kwa kawaida mito hujaa wakati wa mvua za vuli au mvua za masika, kwa hiyo, kudhani kipindi cha mvua hizi ndicho kipindi cha kilimo cha umwagiliaji. Tutakuwa bado hatujakamilisha lengo la Taifa la kuwezesha

maendeleo ya kilimo chetu kutegemea *Irrigation*, kwa sababu mkulima hawezi kulima na kuvuna mara mbili au mara tatu kwa mwaka kwa sababu mito itakuwa kina chake kinapungua hivyo kukosesha maji ya kutosha kwa kulima mara tatu kwa mwaka.

Matumizi mengine ya *Tube-wells* ni kwamba, *Tube-wells can be sited adjacent to areas to be irrgated.* Pia uchimbaji wa *Tube-wells can be phased with demand*. Kwa njia hii *costly excess capacity in early years of development can largely be avoided.*

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo hoja ya kupunguza gharama za uchimbaji wa visima inatoa nguvu kubwa katika kilimo cha umwagiliaji. Kukataa kuanzisha *Tube-wells Irrigation System* katika nchi yetu kwa kisingizio cha sababu ya uchimbaji wa visima hivyo ni ghali mno, kwa tamko la Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hoja hiyo haina msingi. *South-East Asia* inahesabiwa ni miongoni mwa *Third World Countries* au nchi zinazoendelea. Lakini pamoja na idadi kubwa ya wananchi wao, bado haijasikika wakiomba chakula kutoka *FAO* au *World Bank* au Marekani.

Mafanikio yao katika kilimo yameletwa kwa kutumia maji yao kuendeleza uchumi wao na huko *Tube-wells* zipo karibu kila shamba.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja ya maelezo haya, napendekeza umshauri Waziri wa Fedha kwamba, Wizara ya Kilimo na Chakula katika mapendekezo Bajeti ya mwaka 2003/2004, iweke fungu la kuanzisha mfumo huu wa *Tube-wells Irrigation* hasa katika maeneo yaliyokuwa *designed* kwa kilimo cha umwagiliaji kwa njia ya *Surface Water Canal*. Tukiogopa gharama, nchi yetu tutashindwa kujitosheleza kwa chakula na ziada ya kuuza nchi za nje kuongeza Pato la Taifa.

MHE. MOHAMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa wote wale walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuzungumzia suala la biashara, ukweli Zanzibar kwa muda mrefu ni sehemu mojawapo yenye shughuli nyingi za biashara kiasi ambacho Afrika ya Mashariki yote inaelewa hilo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo wa utekelezaji wa kodi kati ya Zanzibar na Bara kwa sasa umekuwa mgumu zaidi hasa ukizingatia kuwa soko kubwa la bidhaa za Zanzibar liko Tanzania Bara na Commoro kwa asilimia ndogo. Tatizo zaidi linalotukabili ni usawa wa kodi kati ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, kwani leo hii kama bei za bidhaa zitakuwa sawa kati ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, si rahisi mtu kutoka Bara kwenda Visiwani kufuata bidhaa ambazo Tanzania Bara atazipata kwa bei ile ie ya Tanzania Visiwani halafu haishii hapo tu

Mheshimiwa Spika, baada ya mzigo kufika Bandarini Dar es Salaam unachekiwa tena na baadaye kulipia bidhaa zilizozidi *(Excess)*, hilo lote sio tatizo lakini tatizo linalokuja ni kuzuiliwa bidhaa kwa muda mrefu pale Bandarini hadi kusababisha baadhi ya mizigo kuibiwa na kusababisha hasara kubwa kwa mwenye mali, ukweli tunaoathirika zaidi ni wafanyabiashara wa Zanzibar. Kwa hiyo, tunachoomba uweko uwiano wa *rate* kati ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali ilitoa elimu ya kutosha kwa wananchi na hasa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amepita mikoa yote kuwataka wananchi kutumia vyandarua na kutia dawa ya ngao, lakini leo cha kusikitisha ni kwamba, wananchi wamepokea maagizo ya Serikali kwa kutumia vyandarua hasa wanawake wajawazito na watoto, ambao ndio waathirika wakuu wa malaria, leo hii kodi ya vyandarua imepanda kutoka 0% - 10%, hii ni sawa na kuwakusanya wananchi baada ya banda kujaa sasa tumewafungia ndani hawana pa kutokea, ningeliomba ushuru huu uondolewe ili kuwarahisishia wananchi wananunue kwa wingi vyandarua ili kujikinga na malaria ambayo ni adui mkubwa.

Mheshimiwa Spika, suala la pensheni nashukuru Serikali kwa kusikiliza vilio vya Waheshimiwa Wabunge, kwani huko tunakotoka kwenye Majimbo yetu, hicho ndio kilio cha wastaafu, lakini kwa kuwa limeonekana umuhimu wake, sasa tunachoomba ni utekelezaji wake ufanywe kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna hali inayoleta malalamiko mengi kwa wastaafu katika vikosi vyetu vya ulinzi na usalama, *gratuity and pension*. Watu hawa wote wawili huingia kazini siku moja na takriban hufanya kazi pamoja, kwa muda usiopungua miaka 20-30, lakini siku ya kuacha kazi huwa na tofauti ya kipato mwenye pensheni hupata pesa zaidi kuliko huyu mwingine, ningeomba Serikali iondoe mfumo huo na iweke aina moja tu ya malipo ya wastaafu wote kwa pamoja, kwani tofauti iko kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika:-

Mheshimiwa Spika, mimi siridhiki na ubinafsishaji wa mashirika kutokana na yafuatayo:-

(i) Kutokulipa mafao - *Timing Boom*;
(ii) Viwanda kusimama uzalishaji;
(iii) Wafanyakazi kuishitaki Serikali; na
(iv) Mitambo kuchakaa/kung'olewa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha, kuweka siku 15 za kulipia mafuta ya petroli, muda huu unafaa tu kwa bidhaa ya aina hiyo iliyoko *Bonded Ware Houses*, kwa mafuta ya Makampuni ya *CALTEX, OILCOM, GAPCO, TIOT* na kadhalika.

Napendekeza sasa kodi zilipwe kwa awamu tano. Kwa mapendekezo ambayo Wizara itapendekeza, vile vile kwa nini Serikali haiweki *flow meter* bandarini?

Mheshimiwa Spika, wenye viwanda nchini na wawekezaji wanalalamika sana juu ya bei ya umeme ambayo iko juu sana. Inakatisha tamaa wawekezaji. Kinachotakiwa ni utaratibu wa Serikali kuonyesha ratiba ya upunguzaji kwa awamu kisha itaje tarehe ya mwisho ya kupunguza umeme ili wawekezaji wavutiwe.

Mheshimiwa Spima, mishahara nchini, kima cha chini cha mshahara hakikutajwa. Tarehe ya mshahara ya Tanzania ni ipi tarehe 29 au 30 au 15?

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pensheni Serikali imefanya kazi nzuri sana kuongeza kiwango cha Sh. 20,000/= badala ya Sh. 10,000/=. Naomba waliolipwa kwa mkupuo walipwe ongezeko kwa kuondoa kiasi walichochukua au walipwe asilimia 50 ya kiwango cha chini cha Sh.20,000/=. Naomba sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, uanzishwe Mfuko wa Pensheni ya Madiwani, kidogo kidogo ili walipwe mapema na kwa ukamilifu.

MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango kidogo kuhusu mikopo. Katika hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha alitamka kwamba Serikali itakamilisha mpango wa kuanzisha Benki itakayohudumia wavuvi, wafugaji na wakulima wakubwa na wa kati. Pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitamka kuwa Serikali itaanzisha mfuko wa kuhudumia mifugo kuanzia Bajeti hii. Naunga mkono Bajeti ya Waziri wa Fedha kwa asilimia mia kwa mia. Hata hivyo naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kupata ufafanuzi wa tamko la Serikali kwamba mpango wa kuanzisha Benki itakayohudumia wavuvi, wafugaji na wakulima wakubwa na wa kati ukamilishaji wa utekelezaji wake utakamilika kuanzia Bajeti hii au utakamilika katika Bajeti zijazo?

Serikali ina watumishi wataalamu waliobobea katika fani mbalimbali na wengi wa wafanyakazi hasa wastaafu huwa hawana mtaji wa kujikwamua kwenye umasikini na pia wengi hawana dhamana ya kudumu, kwa hiyo kwao kupata mikopo kwa mfumo wa sasa haiwezekani.

Napendekeza Benki hii ya Wavuvi, wafugaji na wakulima ianzishe kutoa mikopo ambayo dhamana yake ni elimu ya mhusika pamoja na utumishi wa mhusika, utumishi katika kilimo, ufugaji na uvuvi. Ni jambo lililowazi kuwa elimu ya mfanyakazi, mkulima, mvuvi na mfugaji, Serikali inailipia kwa miaka mingi hadi kuipata elimu hiyo na kuwawezesha kufikia elimu ya juu ya Chuo Kikuu na Vyuo vingine Vikuu vya elimu za fani mbalimbali. Ni wazi kuwa elimu ambayo Serikali inalipia kwa kipindi cha miaka kadhaa haitumiki kikamilifu kujenga nchi yetu kwa ukosefu tu wa dhamana kwa wavuvi hao, wakulima na wafugaji wenye uzoefu mkubwa wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ukichukua gharama inayotumika na Serikali katika kujenga elimu na gharama zinazotumika na Serikali katika kuwawezesha wakulima na wafugaji na kulinganisha jinsi ambavyo elimu hiyo ina uzoefu huo wa wakulima na wafugaji usivyotumika kikamilifu kujenga nchi yetu kwa sababu tu ya ukosefu wa dhamana, utagundua gharama hiyo haiwezeshi nchi yetu kujengwa kitaalamu katika taaluma ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Hali hii inaifanya nchi yetu uchumi wake ukose kujengeka kitaalamu. Katika hoja ya uanzishwaji wa Benki ya wavuvi, wafugaji na wakulima naomba kupendekeza njia mbadala za utoaji wa mikopo kwa wakulima, wavuvi na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa kabla ya mtu hajakopeshwa na Taasisi za fedha, kigezo kikubwa kinachohitajika ili mwombaji huyo akopeshwe lazima wawe na dhamana ama ya nyumba iliyojengwa kwa gharama kubwa au awe na shamba lenye mazao ya kudumu na Hati Miliki. Taasisi za fedha zote *(Banks)* utaratibu huo ndio wanaoupa kipaumbele kabla ya mtu hajastahili kufikiriwa kupata mkopo.

Mheshimiwa Spika, naomba kufahamishwa kwamba huo ndio utaratibu utakaotumika na Benki hiyo ya wavuvi, wakulima na wafugaji katika kutoa mikopo yao kwa wavuvi, wakulima na wafugaji? Kama watatumia utaratibu huu, nashawishika kuamini nchi yetu haiwezi kupata maendeleo ya kilimo kikubwa na kidogo cha kitaalamu endelevu. Kwa ajili hii, nampongeza Waziri wa Fedha kwa kuwezesha kuwa na Benki ya wavuvi, wafugaji na wakulima. Napendekeza tuwe na mfumo mpya wa kutumia kwa ajili ya kukopesha wakulima, wavuvi na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametamka kwamba Serikali itaboresha kumbukumbu za wastaafu na amesema Serikali inafanya haya kwa kuthamini mchango mkubwa wa wastaafu wake wakati walipolitumikia Taifa. Inakubalika Serikali ina watumishi wataalamu waliobobea katika fani ya kilimo, uvuvi na ufugaji na fani nyingine. Kwa ajili hii, napendekeza Serikali ikubali kuwaruhusu wataalamu wa kilimo na mifugo ambao wako tayari kuingia kwenye kilimo na mifugo cha kibiashara, yaani waliokubali kuingia katika *Business Agriculture and Livestock* wawezeshwe kupewa mikopo ya kuendeshea shughuli hizo za kilimo, uvuvi na ufugaji na pia kabla ya kuacha kazi zao wale waliokuwa katika ajira walipwe haki zao ili wakazalishe na wale wataalamu walioacha kazi kabla ya mfumo huu wawezeshwe kupewa mikopo kuendeleza kilimo, uvuvi na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, napendekeza uwezeshaji wa kukopesha dhamana iwe elimu ya kazi zao na kazi walizoziacha. Elimu ya kilimo na ufugaji pamoja na elimu za fani nyingine zozote ni dhamana kubwa sana kwa maendeleo ya Taifa. Kwa kutumia misingi hiyo, Serikali itoe *guarantee* kwa wasomi hao na wakulima wenye uzoefu na wafugaji wenye uzoefu pamoja na wavuvi wenye uzoefu, elimu zao na uzoefu wao uwe ndio *collateral* za kupata mikopo hiyo. Serikali za Vijiji zihusishwe zaidi katika kuthibitisha uwezo na uzoefu wa wakulima wakubwa na wakulima wa kati, wafugaji na wavuvi. Mfumo wa dhamana ya aina hii utawezesha vijana wetu walio mashuleni, walio katika Taasisi za Elimu na walio Chuo Kikuu kuongeza bidii ya masomo yao wakiamini katika maisha yao elimu na uzoefu wa kazi katika maisha yao ni dhamana ya kupata mikopo. Mafunzo na uzoefu wao utafanya maendeleo ya Taifa letu kuwa endelevu.

Mikopo itakayotolewa, dhamana yake iwe kazi zao watakazoziacha na viwango vya elimu zao pamoja na uzoefu wao katika kilimo, ufugaji na uvuvi. Hakuna njia nyingine ya kuthamini elimu ila kuwezesha elimu kuleta maendeleo katika Taifa. Hivyo, elimu itakapokuwa ni dhamana ya kupata mikopo, kilimo bora kitapanuka na kuongezeka pamoja na kuongezeka mifugo bora na uvuvi bora ambapo mapato yake yataongeza kwa asilimia kubwa sana *export crops* na hivyo kuongezea Taifa mapato ya fedha za

kigeni. Katika utekelezaji, Serikali itabidi itoe masharti ya uzalishaji kwa shabaha ya kukidhi malengo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, wakulima wakubwa na Wadogo Wadogo na wafugaji pamoja na wavuvi wapewe mikopo ya masharti nafuu. Uzoefu wao katika kilimo, ufugaji wao na uvuvi wao ndio utumike kuwa dhamana ya kupata mikopo. Hata kama ardhi haina *lease* isichukuliwe kuwa ni kigezo cha dhamana. Serikali za Vijiji zitumike kuthibitisha uwezo wa wakulima wakubwa na wakulima wadogo wadogo, wafugaji na wavuvi kufikiria kutoa wastani unaostahili kukopeshwa ili kuwawezesha kulima kilimo bora na ufugaji bora ulio endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Taasisi za Fedha zinahitaji mikopo itolewe kwa wakulima wakubwa na wakulima wadogo wadogo, wafugaji na wavuvi kwa masharti ardhi lazima ziwe na lease, nina mashaka mfumo huu wa ukopeshaji ukiachwa uendelee hatimaye itatokea ardhi yote kuwa mali ya Benki hiyo.

Serikali inaweza kuwa na mashaka juu ya utekelezaji wa utaratibu huu, napendekeza hasa juu ya utaratibu wa ukopeshaji namna Taasisi ninayopendekeza hasa juu ya utaratibu wa ukopeshjaji na namna Taasisi za Fedha zitakavyopata fedha za kujiendesha. Napendekeza Serikali itoe fungu kuwezesha Benki hii ya wavuvi, wakulima wakubwa na wa kati na wafugaji, pia Serikali itoe *guarantee* kwa wote watakaoomba mikopo. Kwa njia hii, Benki itapata fungu la kujiendesha.

Kwa kuwa ukopeshaji wa Benki kipaumbele chao ni dhamana *(collateral)*, napendekeza ukopeshaji wake *(collateral)* iwe elimu na uzoefu wa mwombaji katika kilimo, uvuvi na ufugaji. Mfumo huu unainua ubora wa kilimo chetu na mifugo yetu na kuongeza pato la Taifa. Kwa mfano, wataalamu wa Kituo cha Utafiti cha Minazi na Mazao mengine wakikubali kuacha kazi zao kwa makubaliano watalipwa haki zao kwa kutumia taratibu zilizopo, elimu yao ya utafiti na uzoefu uchukuliwe kuwa ndio collateral ya kukopeshwa na Serikali pia iwe *guarantor* kwa wakopeshwaji hao kwa Taasisi za Fedha pamoja na Benki ya wakulima, wavuvi na wafugaji.

Watafiti na wasomi wengine katika Taasisi mbalimbali watahamasika sana na kwa njia hii matokeo ya utafiti wao utapanua na kuwezesha upatikanaji wa mazao yaliyo bora na kwa wingi katika muda mfupi. Kwa njia hii kilimo chetu kitatoa mazao bora na kuwezesha kushindana katika masoko kwa kutumia mfumo huu wa utandawazi katika soko la Afrika ya Mashariki na Soko la Dunia.

Kwa kufanya hivyo pia Serikali itakuwa imewezesha mambo yafuatayo baada ya kupatiwa raslimali kwa njia ya mikopo hiyo, uzalishaji utaongezeka kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. Hii ina maana kipato cha Taifa kitaongezeka na bei za bidhaa zitapungua kwa wananchi kwa mazao ya kilimo na bidhaa zake pia za wafugaji pamoja na bidhaa zao.

Kinachohitajika hapo ni kwa Serikali iwe na usimamizi ulio na uadilifu na madhubuti katika utekelezaji katika suala hili. Pia Benki itoe muda wa miaka minne kwa wakulima, miaka saba kwa wafugaji na miezi miwili kwa wavuvi na kuanza kurudisha mikopo kwa riba ya asilimia tatu.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nizungumzie suala la kuunda wakala wa kuendeleza kilimo.

Ingawa Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema katika hotuba yake ya Bajeti kwamba kilimo kinachangia zaidi ya asilimia hamsini ya pato la Taifa na kubeba asimilia 80 ya Watanzania, bado kilimo chetu ni dhaifu na kinahitaji mabadiliko ya haraka. Pia Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji akiwasilisha Bajeti ya Wizara yake Bungeni kwa upande wa ukuaji kisekta *(sector growth)* katika mwaka 2002 alisema Sekta ya Kilimo ilikua kwa asilimia tano ikiwa ni pungufu kidogo ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.5 mwaka 2001, bila shaka ukuaji wa Sekta hii ya Kilimo mwaka 2003 itakuwa chini zaidi. Hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipotamka ndani ya hotuba ya Bajeti yake kuwa kilimo chetu ni dhaifu na kinahitaji mabadiliko ya haraka alitoa ujumbe muhimu sana kwa viongozi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshauri Waziri wa Fedha akubali kuwa mabadiliko ya haraka ambayo yanastahili kuchukuliwa sasa ni kutunga sheria ya kuundwa kwa wakala wa kusimamia uendelezaji wa kilimo. Kwa kuwa Wizara ya Kilimo na Chakula kwa miaka mingi imekuwa inajishughulisha na sera, hivyo kwa kipindi cha miaka mingi imekosa muda wa kutosha kujidhatiti kusimamia kilimo nchini. Napendekeza Serikali ikubali kutunga sheria itakayoanzisha Wakala wa Kilimo itakayowajibika kiutendaji kwa Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Wakala hii itakuwa kuwawezesha na kuwasaidia wakulima kuweka mikakati ya kuwasaidia kuongeza bei ya mazao yao na kuwahimiza kwa kuwapa moyo wa kujenga tabia ya kubadilisha aina ya mazao ya kilimo chao kwa kuzingatia *concept* ya *crop development life cycle* na pia kuwawezesha kuendeleza *wider range of products, interests and skills in order to be more successful or reduce risks.* Ni wakati muafaka kwa hivi sasa kuunda chombo maalum cha utendaji wa kilimo kwa sababu kilimo ni muhimili wa uchumi wa Taifa letu. Kama ilivyojitokeza, Wizara nyingi ambazo kwa sasa zimekwishaanzishwa Wakala kwa mfano Wizara ya Ujenzi imeweza kutunga sheria ya kuunda *Tanroads* ambapo viongozi wote wa Mikoa pamoja na viongozi wote wa Wilaya ni Wajumbe wa Bodi, hivyo kuwezesha kusimamia kikamilifu ujenzi wa barabara za Taifa na barabara za Mikoa kwa ufanisi mkubwa sana. Matokeo ya kazi nzuri inayofanywa na *Tanroads* chini ya usimamizi wa Wizara ya Ujenzi yamejenga matumaini makubwa ya ufanisi wa utekelezaji wa sera za Wizara ya Ujenzi katika Taifa letu. Kimuundo, karibu Wakurugenzi Wakuu wa *Tanroads* zote katika Mikoa yote ya Tanzania Bara pamoja na Wakurugenzi wa Kanda wote walikuwa waajiriwa wa Wizara ya Ujenzi.

Kwa mfano, utekelezaji mzuri wa *Tanroads* maana iwapo Wizara ya Kilimo na Chakula itakuwa na Sheria ya Kuunda Wakala, *Tanzania Agricultural Agency (TAA)* ni dhahiri kilimo kitasimamiwa kikamilifu kuanzia ngazi ya Mkoa hadi Kijiji kwa sababu viongozi katika Bodi ya Wakala ya Mkoa watahusishwa na kuwezeshwa kusimamia uendelezaji wa kilimo chetu nchini. Nasema hivyo kwa sababu kwa kuiga muundo wa Tanroads viongozi wote wa Mkoa na Wilaya watakuwa Wakurugenzi wa Bodi hiyo.

Kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana kupitia *Tanroads*, imewezesha Wizara ya ujenzi kufanikiwa kwa ufanisi mkubwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kwa kuwa kilimo bado ni dhaifu na kinahitaji mabadiliko ya haraka kwa sababu asilimia hamsini ya pato la Taifa inachangiwa na kilimo kinabeba asilimia 80 ya Watanzania na kwa kuzingatia mafanikio ya utekelezaji wa Wizara ya Ujenzi yaliyosababishwa na wakala wake Tanroads, Serikali imetenga Shilingi bilioni 126 katika Bajeti ya Wizara ya Ujenzi mwaka 2003/2004.

Kwa ajili hii, napenda kumshauri Waziri wa Fedha akubali Serikali itunge Sheria ya kuunda Wakala wa Sekta ya Kilimo yaani *Tanzania Agricultural Agency (TAA).* Wakala wa Sekta ya Kilimo bado itawajibika kwa Wizara ya Kilimo na Chakula kama ilivyo hivi sasa Tanroads Wakala wa Sekta ya Barabara inawajibika kwa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, inawezekana hoja ya kutunga sheria ya kuunda wakala ingeanzishwa na Wizara ya Kilimo na Chakula lakini kwa kuwa katika hotuba ya Waziri wa Fedha amesema kilimo chetu ni dhaifu bado sijakosea kutoa mchango wangu kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, iwapo Sheria ya Kuunda Wakala itatungwa, *this move will push income to new heights.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha ametoa msamaha wa kodi ya *VAT* kwa hoja kwamba shughuli za uchimbaji wa madini una shughuli nyingi tofauti, *Tanzanite* ni miongoni mwa madini aliyoyatolea mfano.

Mheshimiwa Spika, mimi kimsingi nakubaliana na uamuzi wake. Lakini nahitaji maelezo zaidi kwa nini *VAT* kwa mazao ya Tumbaku na Miwa yasipatiwe msamaha wa kodi ya *VAT?*

Mheshimiwa Spika, mimi naelewa ukichukua pato linalopatikana kutoka katika Sekta ya Madini katika kipindi cha muda mfupi ni mkubwa sana ukilinganisha na mapato yanayopatikana kutoka mazao ya tumbaku na miwa katika kipindi hicho cha muda huo mfupi. Naelewa pia Sekta ya Madini yanahitaji utoaji

wa uwekezaji mkubwa ukilinganishwa na zao la Tumbaku na Miwa. Naelewa pia ukitoa *VAT* katika zao la miwa na zao la tumbaku utakaribisha msululu wa maombi wa kutolewa kodi hiyo ya *VAT*. Lakini ni vizuri zaidi ikalinganishwa pato la fedha za kigeni linaloingizwa namazao haya mawili ikilinganishwa na mazao hayo mengine. Pia ni vizuri zaidi ikaeleweka ushindani wa kimasoko unaopata zao la miwa na zao la tumbaku ikilinganishwa na haya mazao mengine, baada ya kupata jawabu ndipo hoja ya kulinganisha mazao ya miwa na tumbaku na mazao mengine ikatumika katika kutoa kodi ya *VAT*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hoja hizo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anieleze kama madini katika nchi yetu ni endelevu. Aidha, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anieleze kimazingira madini yanayochimbwa ambayo sasa yanafutiwa kodi ya *VAT*, ardhi hiyo inayochimbwa madini itakuwa na matumizi gani endelevu katika kuendeleza pato na uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anieleze katika ushindani wa madini kama *Tanzanite*, Almasi na Dhahabu katika soko la Dunia yana ushindani wa asilimia ngapi? Aidha, kwa kuwa alitoa mfano wake wa madini ya *Tanzanite* naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anieleze madini haya yana ushindani gani katika Soko la Dunia, hasa tukielewa madini haya yanapatikana Tanzania tu.

Hoja kwamba wanatumia uwekezaji wenye thamani kubwa, si dhana nzuri kwa sababu mashamba ya miwa ya Kilombero yana dhana yenye thamani kubwa sana na mashamba ya Mtibwa hivi sasa yanajengwa Milling Machine yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 36. Kwa hiyo kutoa kodi ya *VAT* kwa kisingizio wawekezaji wa madini wanaleta mtaji mkubwa na mitambo mikubwa, si sahihi kwa sababu ukichukua uwekezaji wa viwanda vya tumbaku vya Morogoro utagundua ni thamani kubwa sana ya mabilioni ya Dola za Kimarekani zimetumika kuwekezwa katika nchi yetu kwa ajili ya ku-*process* mazao endelevu katika mapato ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, *theory of marketing* inatufundisha mikakati ya kuwezesha wazalishaji kama vile kuwafutia kodi inatokana na ushindani wa *products* katika soko. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anieleze kama hayo madini aliyotolea mfano yanapata *competition* katika soko la Dunia.

Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anieleze kama Wizara yake imekwishafanya *Environment Damage Assessment* kwa hayo madini ambayo sasa anayafutia kodi ya *VAT* na anieleze ni mikakati gani itakayotumiwa kurudisha hali ya mazingira kurudishiwa kama ilivyokuwa kabla ya kuchimbwa hayo madini.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anieleze ajira ya maeneo ya madini yana ukubwa wa asilimia ngapi ikilinganisha na idadi ya wakulima wa tumbaku na miwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, zao la miwa ni chakula. Mheshimiwa Waziri wa Fedha amefuta karibu kodi zote za mazao ya wakulima. Huo uamuzi naukubali kwa sababu utatia chachu kwa wakulima wazidishe kilimo chao. Zao la miwa ingawa pia linalimwa na viwanda vinakua, karibu asilimia 60 ya sukari inatoka na wakulima wadogo wadogo wa miwa.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha miwa ni endelevu kwa sababu hakina *environmental damage*. Kila mwaka kitaendelea kulimwa mpaka mwisho wa dunia. Zao hili la miwa lina mashindano makubwa ya soko katika soko la Afrika Mashariki, Afrika na nchi za Ulaya. Kwa hiyo, kilimo hiki cha miwa kinapambana na Wafanyabiashara ambao katika nchi zao wanapata ruzuku *(subsidy)* ya kulima miwa na wanapata ruzuku pia ya kutafuta masoko ya kuuza mazao yao? Katika nchi yetu, wakulima wa miwa hawapati ruzuku ya kulima, mbolea wala ruzuku ya kutafuta masoko ya mazao yao. Kwa kweli wana *Market Competition* nzito sana.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, karibu asilimia 45 ya sukari katika nchi yetu inatokana na miwa inayolimwa na wakulima wadogo wadogo wa miwa. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze msingi wa kutowafutia kodi ya *VAT* wakulima wa miwa. Uamuzi huo umejengeka na hoja zipi hasa akielewa *Sugar Industry* inahusisha wakulima wadogo wadogo wengi katika kilimo cha miwa ambao nina hakika

kama kodi ya *VAT* ingefutwa ingewaongezea kipato na hivyo kuongeza upandaji na kuendeleza utunzaji wa miwa.

Mheshimiwa Spika, *Sugar Industry* inapata ushindani mkubwa wa watu waliopewa vibali vya kuagiza *White Industrial Sugar*. Hao wanaoomba wanatumia hoja ya kutengeneza *biscuits* na vitu vingine lakini ukweli ni kwamba kiasi wanachokiagiza ni kikubwa mno kuliko *demand*. Hivyo wanatumia upenyo huo kuwauzia wananchi kwa bei poa. Hii *White Industrial Sugar* inatoka katika nchi ambazo zinatoa *heavy subsidies* Kwa wakulima wao na kwa watafutaji wa masoko ya hiyo *white sugar*. Hivyo, wanashiriki kupunguza bei ya sukari katika masoko na hivyo kuongeza ushindaji mkubwa kwa *Sugar Industry* yetu hata humu humu ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, namshauri Waziri wa Fedha afute kodi ya *VAT* kwa wakulima wa miwa.

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha afute kodi ya *VAT* kwa wakulima wa tumbaku. Kilimo hiki karibu asilimia mia kwa mia kinalimwa na wakulima wadogo wadogo. Katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema atatoa msaada wa mbolea kwa baadhi ya Mikoa, lakini katika orodha yake sikuona Mikoa hiyo maarufu kwa kilimo cha tumbaku kama vile Tabora na kadhalika. Kama hatafuta kodi ya *VAT*, wakulima wa tumbaku wa Mkoa wa Ruvuma watapata bei kubwa kwa kilo moja ya tumbaku kuliko wakulima wa Mkoa wa Tabora. Kisiasa uamuzi huu si mzuri kwa sababu utaongeza nguvu za uchumi kwa Mkoa mmoja na kupunguza nguvu za uchumi kwa Mkoa mwingine. Kwa ajili hii, napendekeza waongeze kipato chao na pia wawe washindani wazuri katika soko la tumbaku.

Mheshimiwa Spika, naelewa Mikoa hiyo inayopewa misaada ya mbolea ina historia ya kuitwa big five kwa maana ya kilimo cha mahindi. Dhana hii kwa maoni yangu sasa imepitwa na wakati kwa sababu ipo Mikoa mingi yenye sifa za kuzalisha mahindi kama vile Mkoa wa Morogoro, Kigoma, haimo katika orodha ya kupewa msaada wa mbolea na Serikali. Hoja zangu zote zinasisitiza kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atoe kodi ya *VAT* kwa zao la miwa na tumbaku, kwa sababu mazao haya yana ushindani mkubwa wa kimasoko duniani.

MHE. ESHA H. STIMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kuidhinisha Bajeti nzuri ya mwaka 2003/04.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil P. Mramba kwa kuiwasilisha hotuba ya fedha ya mwaka 2003/2004 kwa makini mbele ya Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hali kadhalika Mheshimiwa Kigoda kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Bajeti ya mwaka huu 2003/2004 imeelekeza mafanikio kwa wananchi kwa asilimia kubwa. Mimi kwa furaha kubwa naunga mkono mia kwa mia. Kwa hiyo, nachangia vipengele vichache au kuomba kuviboresha kama ifuatavyo:-

Nashukuru kwa nyongeza ya pensheni kufikia hadi kima cha chini kuwa Sh.20,000/=. Lakini mimi nina ombi la baadaye kwamba kwa mwaka 2004/2005 sheria ibadilike, malipo yafanyike awamu tatu badala ya mbili ili wastaafu waweze kutatua matatizo yao kwa vipindi vya miezi mitatu. Yaani Januari - Machi, Aprili walipwe, Mei - Julai, Agosti alipwe, Septemba - Novemba, Desemba walipwe. Marekebisho hayo yataongezea wananchi upendo kwa Serikali yao, kama ilivyo kwa Bajeti hii 2003/2004

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo wa ushuru wa forodha, hakika tumefarijika kwa mapunguzo ya ushuru kwa baadhi ya bidhaa, lakini bado naomba marekebisho yafanyike kwa baadhi ya bidhaa hizo kama zifuatazo: Dawa ya mbu ya kuchoma, kiwango kibaki cha sasa cha asilimia kumi badala ya 15, mafuta aina ya *Petroleum Jelly* kiwango kiwe asilimia kumi badala ya 15 na *Chassis* za mabasi, kiwango kiwe asilimia tano badala ya kuwa asilimia zero. Kwa sababu wananchi watakuwa na mawazo mabaya kuwa Serikali inapendelea matajiri. Kwa hiyo, kuwepo na ushuru walau kidogo kama asilimia tano. Hali kadhalika ushuru wa dawa za mbu za kuchoma na matufa ya *Petroleum Jelly* ndio yanatumiwa sana na wananchi wa hali ya chini. Sasa ushuru ukipanda na bei ya kuuzia itapanda na kuwapa kero wananchi wa

kawaida. Kwa hiyo, naomba ushuru upunguzwe kama nilivyopendekeza hapo juu na kupandisha maeneo mengine kama vinywaji vikali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu ushuru wa leseni za magari, *VAT*, kodi ya mapato kwa biashara ya magari. Katika Bajeti hii sijaona mahali palipozungumziwa kusamehewa au kupunguza kodi/ushuru kwa biashara za magari ya abiria kwa mfano gari likipata ajali ya kushindwa kufanya biashara yake kodi haifutwi au kupunguzwa. Analipia *TLB* (njia ya safari za gari) gari likipata ajali fedha hairejeshwi na anapohitaji tena *TLB* anatozwa tena gharama za leseni bila kujali kuwa muda wake ulikuwa bado haujaisha na alipata ajali. Hali kadhalika *VAT* ilivyokadiriwa inabaki vile vile. Hali hii inawanyima haki wafanyabiashara wa magari. Naomba yafanyike mabadiliko ya kupunguziwa ushuru.

Mheshimiwa Spika, niseme kwa niaba ya wapiga kura wangu Mkoani Shinyanga kwamba wanaishukuru sana Serikali kwa kufuta kodi mbalimbali ikiwepo kodi ya maendeleo ambayo ilikuwa kero kubwa kwa waume zao kukamatwa na kuwafanya washindwe kushiriki mikutano ya hadhara, mbio za mwenge, sherehe na sikukuu za Taifa na kadhalika kwa kuhofu kukamatwa wanapoenda na kurudi kwenye shughuli hizo muhimu.

Mfano mkubwa umejitokeza katika mbio za Mwenge za mwaka huu 2003, wanaume wengi wameshiriki katika mbio za mwenge kuliko miaka ya nyuma. Hakika miaka ya nyuma ni wanawake pekee walikuwa wanashiriki kwa wingi kuliko wanaume.

Mheshimiwa Spika, pamoja namango mengi mazuri yaliyopo katika Bajeti hii ya mwaka 2003/04 bado sijaona mikakati ya makusudi ya kupiga vita Ukimwi hapa nchini ugonjwa ambao unapunguza nguvu za uzalishaji kwa wananchi wengi kukosa nguvu na hatimaye kufariki kwa wingi. Kwa hayo machache narudia tena kusema naunga mkono hoja hii ya Bajeti ya mwaka huu 2003/2004 mia kwa mia.

MHE. REMIDIUS E. KISSASSI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kusema naunga mkono Bajeti hii na ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri sana. Pamoja na hayo, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile makusanyo yetuya ndani ya nchi ni madogo ukilinganisha na nchi jirani, napendekeza kiwango cha *VAT (20%)* kiangaliwe kwa makini, kipunguzwe ili kuchochea *consumption* kwa kupunguza kodi hiyo na nyingine. Bado Tanzania tuna kodi kubwa mno. Hata kodi katika bidhaa za mafuta bado ni kubwa na nyingine si za lazima, hivyo kusababisha gharama za mafuta kuwa juu. *Fuel Oil (IDO)* ipunguzwe ili tupunguze gharama za uzalishaji viwandani na hata bei za umeme zitapungua hivyo vitu vyetu vitakuwa *competitive.*

Kwa vile tumeshakubali kuwa umeme ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya jamii na kama tumeweza kuendesha kodi kwa vifaa na mitambo ya kuchimba visima, basi vivyo hivyo kwa mitambo ya kuzalishia umeme, *transformers* na waya nzito ili kupunguza gharama za kuvuta umeme. Hivi sasa ni *very discouraging*. Ni muhimu kutumia *EPZs* zetu kusukuma maendeleo haraka hasa kwa kuziweka katika *corridors* zetu nne yaani Mtwara, Dar es Salaam, Tanga na ya Zanzibar kama mkakati mahsusi.

Benki zetu na za binafsi zipewe masharti ya kufungua/kuwekeza katika Wilaya mbalimbali kama *Social Obligation* ya kufanya biashara Tanzania na sio wawekeze Dar es Salaam tu. Mifuko ya kusaidia vijana, wanawake, mikopo nafuu, pembejeo na kadhalika iwekwe *strategically* katika Benki hizo ili iwe motisha kwao kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, suala la *Trade Harmonization v/s Tax Harmonization* liangaliwe kwa undani sana ili biashara zinazopitia Zanzibar zisiuwawe. Mkakati wa makusudi ufanywe ili *flow* ya biashara katika Bandari zetu ziwe *complementary* na si vinginevyo. Ni vizuri ziwepo *tax incentives* kwa kupitisha mizigo katika Bandari za Zanzibar ili kuwepo harakati *(activities)* za kiuchumi.

Kwa vile mengi yamesemwa, ninaomba kusema tena naiunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. PETER KABISA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mawaziri wote wawili, Mhe. Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao zote mbili za Bajeti ya mwaka wa fedha ujao 2003/2004. Ni Bajeti nzuri ambayo imepokelewa na wananchi wa Jimbo la Kinondoni kwa kuridhishwa japo wangependa unafuu zaidi.

Kabla sijasahau, naomba kwanza basi niwapongeze Wabunge wanne wapya wa CCM Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga wa Jimbo la Kilombero, Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi wa Jimbo la Bukoba Vijijini, Mheshimiwa Edward Nziriye Ndeka wa Jimbo la Kigoma Kusini na Mheshimiwa Sumri Abdallah Salum Mohamed wa Jimbo la Mpanda Magharibi na Waheshimiwa Wabunge wote wa *CUF* wa Majimbo ya Pemba. Katika kuchangia hoja ya Bajeti, nimeridhishwa sana pamoja na wananchi wa Jimbo la Kinondoni kwa Serikali kuifuta kodi ya maendeleo. Hii ilikuwa ni mojawapo ya kodi zilizowabughudhi na kuwaudhi sana wananchi. Tunaishukuru Serikali kwa hilo.

Pia tunashukuru kwa Serikali kufuta kodi 52 kutoka kodi 60 ambazo zilikuwa pia ni kero kwa wananchi. Tunategemea kwamba utekelezaji wake utakuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuishukuru Serikali kwa kupunguza hizo kodi, kweli inasikitisha kwamba Serikali haioni umuhimu nambari wani wa kufuta kodi ya dawa ya ngao na malighafi ya vyandarua. Naiomba Serikali ifute kodi hizo hii imhamasishe mwananchi kununua na kutumia dawa hiyo ya ngao pamoja na vyandarua ili kupunguza na kukomesha ugonjwa wa Malaria na vifo kwa wananchi walio wengi. Kutokana na ongezeko hilo, Serikali ipunguze gharama za madawa ya malaria. Serikali ikiweka hiyo kodi, wananchi wengi watashindwa kuhamasika na kununua hizo dawa na vyandarua. Naomba kodi hizo ziondolewe. Nimefurahi kusikia Serikali imetenga fedha za kusaidia kulipia watoto ambao wanafaulu kwenda Shule za Sekondari za Serikali lakini wazazi wao hawana uwezo wa kugharamia elimu yao. Naomba pia kwamba watoto wenye vipaji na uwezo mzuri wanaoingia Shule za *Private* pia wasaidiwe kusomeshwa pindi ijulikanapo kwamba wazazi wao wamefariki au hawana uwezo. Tusibague kati ya watoto wa Shule za Serikali na za binafsi. Tuwasaidie wale wote wenye vipaji na uwezo. Naomba sana hili lichunguzwe na kukubalika.

Mheshimiwa Spika, kwa vile sasa kumekuwa na huu mpango safi sana wa MMEM ni dhahiri kwamba baada ya miaka saba au sita hivi wengi sana watafaulu mitihani yao ya Darasa la Saba kuingia *Form One* na kuendelea. Je, Serikali inaonaje kuanzia sasa kwa awamu kuanza kuhamasisha, kupitia Halmashauri wananchi kujenga Shule za Sekondari kwenye kila Kata ili wakati ukifika tuwe tayari kuwapokea watoto hawa?
Kumekuwa na malamiko kutoka kwa baadhi ya walemavu kwamba kama Serikali haijazingatia mapungufu yaliyopo kwenye kuwaendeleza walemavu kwa mfano wasioona, vifaa vya kusomea na kuandikia *braille* havitoshelezi, hata kidogo. Naiomba Serikali kulitazama eneo hili kwa makini sana na kwa haraka inayostahili wasaidiwe kwenye jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana (kuhusu nishati) bei ya umeme tuliafikiana baada ya mjadala mkali sana kwamba wananchi wote Watapata unit 100 za kwanza kwa karibu Sh. 25/= kwa unit na zitakazofuata zitakuwa kwenye Sh.90 kwa unit moja. Sasa hivi ahadi hiyo haipo. Serikali imeukana utaratibu huo, badala yake ni *unit 50* (na sio 100) unazopewa za unit zaidi ya hapo unalipia zaidi ya Sh.95/= kwa *unit* moja. Isitoshe kwa watumiaji kidogo sana wa hizo *unit*, akiwa na Sh.5,000/= anapata umeme mdogo sana kwa sababu ya *VAT*.

Naomba Serikali ilitazame tena suala hili. Lazima turudi kwenye makubaliano yetu ya kwanza, 100 *unit at an economic price of Tshs. 25/= per unit.* Kuna suala zima la mikopo na misaada mbalimbali kwa wazee. Kwenye Bajeti ya 2001/2002 niliamb iwa palikuwa na *technicalities* ambazo zilikuwa hazijakamilishwa. Hii ni Bajeti ya tatu tangu ahadi ya 2000/2001. Je, hiyo mikopo ya wazee itatolewa mwaka huu wa fedha 2003/04? Naomba majibu.

Kuhusu tatizo sugu la maji safi na salama kwenye Jimbo langu, naomba Serikali, tena naiomba sana, tena sana kwa kuipigia magoti, inihakikishie kwamba maombi yangu yaliyopo Serikalini watayahimiza na

kuhakikisha kwamba hao wanaoikodisha *DAWASA* watatupa kipaumbele wanakinondoni kwa kutupatia maji safi na salama kama nilivyoomba kwenye maombi yangu mbalimbali *DAWASA* na Serikalini.

Serikali itakamilisha uongezaji wa mabomba kutoka bomba la 8" lililoishia Shule ya Mwanyanyamala Kisiwani na kulifikisha maeneo mawili ya Mchangani na Mwanayamala Kisiwani *proper* kwa gharama ya Shilingi milioni 25.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwamba swali la ajira kwa vijana limezungumziwa kijuu juu tu. Hili ni tatizo la Kitaifa si kama malaria au Ukimwi. Lakini ni jambo zito mno. Lazima tupate suluhu vijana tunawafanya nini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Bajeti kuwa *rural friendly* kwa maana ya ajira ya kilimo kwa watoto wetu, bado hatujazungumzia jinsi ya kuwahamasisha waje Vijijini, vivutio ni nini? Wale ambao wameonja *City life* pamoja na matatizo yake ni wachache watakaorudi Vijijini. Naomba Serikali itamke nini itafanya kuondokana na hili *time bomb* - ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Ndugu Harry Kitilya kuwa *Commissioner General* wa *TRA* na Ndugu Luoga kuwa Makamu wake. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuungana na Waheshimiwa wenzangu kuunga mkono hoja hii mia kwa mia hasa baada ya kupata maelezo au majibu ya hayo machache niliyoyaulizia. Nashukuru sana.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi naanza kusema kwamba naunga mkono hoja zote mbili ya Waziri wa Fedha na ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa majibu ya baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kwa Wizara ya Fedha.

SPIKA: Wazalendo kwa maana ya raia?

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Raia wa Tanzania.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwenyewe, majibu.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mapato ya Kodi, haibagui raia wala asiye raia. Inalipwa pale mtu anapopatia mapato yake. Kwa hiyo, hatuna takwimu hizo kwa sasa hivi kwa sababu hatuzihitaji. Tunahitaji kujua tu ni Wakurugenzi wangapi ambao tumetaja kwenye Jimbo letu na ndiyo hao nawalipa hiyo asilimia 26 ya *Withholding Tax*.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, kabla sijaendelea na shughuli nyingine kama kawaida kuna matangazo. Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, alipokuwa akijibu swali hapa alisema, ameshinikizwa, amesukumwa na muuliza swali, ili aweze kutoa taarifa, ametoa majibu ambayo pengine asingeyatoa ni kwamba amesukumwa.

Sasa na mimi leo asubuhi nimesukumwa, nimeshinikizwa niwatambulishe Watanzania ambao kwa kawaida wanakuwa kwenye *Gallery* yetu, ambao kwa kawaida huwa hatuwatambulishi, Watanzania ni haki yao kuja kwenye *Gallery* kusikiliza majadiliano ya Bunge. Kwa hiyo, huwa siwatambulishi. Lakini leo nimeshinikizwa. *(Kicheko/Makofi)*

Niwatambulishe walioko kwenye *Gallery* ya Spika, *diplomatically*. Basi kutokana na shinikizo hilo napenda kusema kwamba walioko huko ni *Miss Tanzania* wa mwaka 2002, pamoja na warembo, nikikutaja usimame, pamoja na warembo wa Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma pamoja na Maafisa wa Kamati ambayo inaandaa mashindano ya *Miss Tanzania*. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya shinikizo sasa natangaza kikao cha Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athumani Janguo, ameomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 20 Juni, 2003 saa 4 asubuhi au mara baada ya kipindi cha maswali katika Kumbi zetu za Kamati. Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper.*

Nikianza na hoja ya mwanzo kuhusu nyongeza kwa Wizara ya Kilimo na Chakula. Inaonekana kama shilingi bilioni 6 ambayo ni ndogo ukilinganisha na nyongeza ya kukusanya fedha, *The Accountant General,* Elimu na kadhalika. Hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa katika fedha ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Fedha na Matumizi Maalum yenye jumla ya shilingi bilioni 56.376 ambayo yaliainishwa katika hotuba yetu ya Bajeti ya Waziri wa Fedha ukurasa wa 78 na kwa upande Fungu la 23 la Mhasibu Mkuu wa Serikali, nyongeza kubwa imetokana na matumizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, malipo ya *Bank Charges* ya shilingi bilioni 9 kwa ajili ya huduma za Benki kwa Serikali. Ya pili, ni *Treasury Voucher System,* shilingi bilioni 31 kwa ajili ya kusimamia misamaha ya kodi. Tatu malipo ya Bima ya watumishi wa Serikali ya shilingi bilioni 6.6. Nne, mafunzo ya Wahasibu ya *In Service* kutoka Wizara, Idara, Mikoa na Halmashauri yenye njumla ya shilingi bilioni 1.92. Tano, uimarishaji na upanuzi wa *Integrated Finance Management System,* shilingi bilioni 5.5 na mwisho Kutathmini Mali ya Serikali ambayo ilikuwa na jumla ya shilingi milioni 700.

Hivyo, nyongeza kubwa katika Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ni kwa ajili ya Matumizi Maalum ya jumla shilingi bilioni 54.72 au asilimia 87.6 na wala siyo matumizi ya kuendesha Idara. Kuhusu nyongeza halisi ya fedha za Bajeti kwa kilimo, ukweli ni kwamba kilimo kwa upana wake kimepewa shilingi bilioni 151 mwaka 2003/2004 kulinganisha na shilingi bilioni 95 ya mwaka 2002/2003. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 56 na siyo shilingi bilioni 6 kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Wizara ya Kilimo na Chakula peke yake imetengewa shilingi 54 bilioni ukulinganisha na shilingi 33 bilioni ya mwaka 2002/2003. Ongezeko la bilioni 21. Barabara Vijijini zimetengewa shilingi bilioni 29 kutoka shilingi bilioni 8.6 ya mwaka 2002/2003. Fedha nyingine kwa ajili ya kusukuma kilimo ni pamoja na shilingi bilioni 12 zilizotengwa chini ya Halmashauri za Wilaya, shilingi bilioni 13 kwa ajili ya kudhamini mikopo kutoka Benki za Biashara kwa ajili ya ununuzi wa mazao. Zote hizi kwa njia moja au nyingine zinachangia katika kilimo. Kuhusu mgao wa asilimia 4.5 kwa misaada kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ulikuwa kiasi gani kwa mwaka 2002/2003 na umeonyeshwa wapi?

Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mbunge wa Utaani, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mbunge wa Mlandege, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Viti Maalum, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mbunge wa Vitongoji, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe na Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mbunge wa Magomeni. *(Makofi)*

Mgao wa asilimia 4 ya mapato ya misaada toka nje umekuwa ukitengwa katika Bajeti ya Serikali kila mwaka. Fedha hizi hazitolewi nje ya utaratibu wa Bajeti ya Serikali. Aidha, *SMZ* imekuwa ikipata gawio kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Katika mwaka 2002/2003 kiasi kilichotengwa kwa *SMZ* kwa madhumuni hayo ni jumla ya shilingi bilioni 9,297 milioni. Kwa mwaka 2003/2004 mgao wa SMZ ni shilingi bilioni 10,298 milioni. Fedha hizi zimeidhinishwa na kuonyeshwa katika kitabu cha Makadirio *Volume II,* ambayo ni *Estimates of Expenditure Consolidated Funds Services, Section One and Supply Votes* ya *Ministerial* Fungu linalohusika ni 31, *Vice President's Office, Sub-Vote 2001* Kasma 280600, *Transfer and Subsidy Other Labels of Government,* ukurasa wa 49. *(Makofi)*

Ruzuku na gawio kwa *SMZ* imekuwa kama ifuatavyo:-

Kwa mwaka kuanzia mwaka wa 1994/95 mpaka mwaka 2001/02. Kwa ruzuku kwa miaka ya 1994/95 mpaka mwaka 1998/99 ilikuwa shilingi bilioni 22,907,900 na mwaka wa 1999/2000 ilikuwa bilioni 1,699.600. Mwaka 2000/2001 bilioni 12,147 milioni na mwaka 2001/2002 ilikuwa bilioni 8,804 milioni. Jumla ni bilioni 45,558.500.

Gawio kwa *BOT,* kwa mwaka 1994/95 *SMZ* ilipata shilingi milioni 553.2. Mwaka 1995/96 milioni 630.2. Mwaka 1996/97 milioni 147.9. Mwaka 1997/98 milioni 393,700,000. Mwaka 98/99 milioni 51 laki moja. Mwaka 1999/2000 milioni 482.3. Mwaka 2000/2001 milioni 543.1 na mwaka 2001/2002 milioni 360. Jumla bilioni 2,891.1. Kwa hiyo, jumla yote *SMZ* fedha walizopewa kwa kipindi hicho, ruzuku pamoja na gawio ni shilingi bilioni 48,449.6.

Kuhusu *SMZ* ilifaidikaje katika *HIPC*. Waheshimiwa Wabunge natumai mmesikiliza hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Zanzibar amelielezea wazi kwamba wamepata misamaha yote iliyohusu, ambayo ilihusikana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ilichukua dhamana pamoja na Serikali ya Zanzibar, mikopo yote ilichukuliwa dhamana imelipwa kwa mpango wa *HIPC*. Kwa hivyo, wananufaika vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya maendeleo kwamba imejaa posho na *Employment Allowance,* hoja ambayo ililetwa na Mheshimiwa Philip Marmo, Mbunge wa Mbulu.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha mfumo wa Bajeti ya Serikali, Hazina imekuwa inachukua hatua mbalimbali. Ni miaka mitatu sasa tangu Serikali imeanza kutumia utaratibu mpya wa kupanga Kasma za matumizi katika vikundi maalum.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ambao unaitwa *Government Finance Statistics* ni wa Kimataifa, unatumiwa pia na nchi nyingine za *SADC*. Mpangilio huu wa *Government Finance Statistics* unakusanya *(classification)* yaani Kasma za matumizi katika vikundi vya kiuchumi yaani *economic cluster's* ambavyo vina Kasma za matumizi yanayofanana, vikundi muhimu ni kama vile *Personal Emoluments, Employment Allowance, goods and services, current transfers, etc.*

Kwa utaratibu wa mpangilio, matumizi yote ambayo watumishi hulipwa kwa kazi maalum au stahili zao huonyeshwa katika kifungu hiki. Matumizi yanayohusika ni kama vile *Perdiem, Extra Duty Allowance, Utilities, Constituency Allowance, Tickets.* Kwa hiyo basi, matumizi yanayolipwa chini ya kifungu hiki siyo tu posho za hivi hivi. Bali ni *OC* ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mpaka sasa utaratibu huu wa *GFS* umekuwa ukitumika katika Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Hatua hii pia tulichukua kwa mwaka 2003/2004, pia ilichanganua miradi ya maendeleo kwa mfumo huu wa *GFS*. Lengo ni kuwa na mfumo mmoja katika Bajeti ambapo itaisaidia kuimarisha matumizi ya *Integrated Finance Management System* ili kutathmini Bajeti yetu yaani kuangalia *impact old the Budget* na *integration* na kulinganisha na Bajeti ya nchi moja na nchi nyingine.

Kutokana na kutumia mpangilio huu wa *GFS,* Waheshimiwa Wabunge wataona kwamba Kasma nyingi ndogo ndogo ambazo zamani hazikuonyeshwa sasa zinaonekana wazi wazi. Ni matumaini yangu kuwa uwazi wa kiasi hiki utasaidia pia Wabunge kuelewa matumizi katika miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Ieleweke wazi kwamba miradi ya maendeleo pia hujumlisha matumizi ya Semina, Warsha, Usafiri, matumizi ya magari kutegemea na mradi wa namna gani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendeshaji wa *Commodity Import Support.* Hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki. Napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba tumepokea mapendekezo ya Mheshimiwa Mgana Msindai na tutayazingatia na baadaye tutakuja na jibu ambalo nina hakika itakuwa ni muafaka kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Kuhusu matatizo ya Pensheni, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia, hii inaonyesha umuhimu katika jamii yetu na kwa Wastaafu. Waliochangia ni Mheshimiwa Mgana Msindai, Iramba Mashariki, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mbunge wa Amani, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, Mheshimiwa Monica Mbega,

Mbunge wa Iringa Mjini, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo na Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza. Hawa wote wamechangia aidha, kwa kuongea au kwa maandishi. *(Makofi)*

Serikali inatarajia kiwango cha pensheni kwa wastaafu wote, kuongezeka. Kima cha chini ambacho kwa sasa kitakuwa shilingi 20,077/= na utaratibu wa malipo wa miezi sita unaendelea. Sheria ya Pensheni haihitaji kubadilishwa kutokana na kwamba wastaafu wote sasa watakuwa wanapata kiwango ambacho hakiruhusu kulipwa kwa mkupuo.

Mheshimiwa Spika, Serikali italifanyia kazi ombi na kilio cha wastaafu ambao walichukua mkupuo miaka ya nyuma na mpaka sasa bado wako hai. Hawa idadi yao ni 33,700. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie kwanza *Financial Implications* za watu hawa. Lakini Serikali inalifikiria na natumaini baada ya muda si mrefu itakuja na jibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Hazina Ndogo zimeimarishwa ili zianze kutoa huduma za wastaafu kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005 ili wastaafu wasiwe wanapata taabu kufuatia mafao yao Dar es Salaam siku zote. Hivi sasa tumeshaboresha Masjala ya Kumbukumbu za Wastaafu waliopo Wizara ya Fedha na tunatarajia kuweka kumbukumbu zote kwenye kompyuta ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa. Tumetoa mwongozo kwa waajiri wote kuhusu kumbukumbu zinazohitajika ili kupunguza muda wa kulipa wafanyakazi wanapostaafu kutoka miezi mitatu hadi mwezi mmoja. Tumetuma maofisa mbalimbali Mikoani ili kufuatia hoja za Ukaguzi za miaka ya nyuma ili kuweza kuwalipa wale ambao hawajalipwa toka wamestaafu. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Serikali yaani *PSPF* kutasaidia kwa kiwango kikubwa kutatua matatizo ya wastaafu hapo siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu misaada ya mchele, mbolea na matrekta kutoka Japan. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zabuni ya mchele ilitolewa na Bodi ya Zabuni kwa kuzingatia ushindani, Sheria, Kanuni na taratibu za *Tender*. Hata hivyo, kufuatia kutenguliwa kwa Zabuni hiyo na Wizara ya Kilimo na Chakula, Mzabuni aliyeshinda, hakuridhika na hivyo alifungua kesi Mahakama Kuu Dar es Salaam. Kufuatia Mzabuni huyo kushinda kesi hiyo hivi karibuni, mchele huo sasa utaondolewa Bandarini mara moja.

Kuhusu hoja ya Bodi za Zabuni za Halmashauri ziwe huru na wazi badala ya Kamati za Halmashauri kuwa zimegeuzwa kuwa Bodi ya Zabuni. Hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho. Hili ni eneo mojawapo kati ya yale yatakayofanyiwa kazi na marekebisho kama ilivyoelezwa kwenye Ibara ya 43 ya Hotuba ya Waziri wa Fedha. Katika marekebisho hayo Serikali inakusudia kuhuisha Kisheria, Kanuni za ununuzi za Halmashauri na zile za Serikali Kuu. Katika suala la kutenganisha kazi za utendaji na zile za usimamizi, Madiwani ni Wasimamizi, hivyo siyo sahihi kuwa kwenye Bodi ya Zabuni za Wilaya. Aidha, kwa kuwa Halmashauri Kuu ya *Tender* mpya, *Central Tender Board* itabaki na jukumu la usimamizi na udhibiti wa Bodi za Zabuni pamoja na zile za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, alizungumzia juu ya Sheria za Manunuzi. Alitaka kujua ni vipi *Public Procurement Act* na Kanuni zake zilisababisha Wizara, Idara na Taasisi zingine au Asasi nyingine kushindwa kutumia fedha zilizoidhinishwa katika Bajeti ya 2002/2003 kwa asilimia 45. Sheria na Kanuni mpya za Ununuzi zinataka ununuzi Serikalini ufanyike kitaalam kwa misingi ya uwazi, usawa, ushindani na kisheria ili Serikali ipate thamani bora ya fedha zake. Upungufu katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni uko katika sehemu mbili, upungufu wa kiutendaji na ule wa sheria na kanuni kama ifuatavyo:-

Kwanza, ukosefu wa wataalam mahsusi wenye elimu na ujuzi wa manunuzi ya *Procurement Experts*. Hali hiyo imesababisha kushindwa kutafsiri zile Sheria na kanuni kwa usahihi na hivyo kusababisha ucheleweshaji katika uwagizaji na upatikanaji wa vifaa na huduma hadi mwaka wa fedha uliposita, ulipoisha. Pili, ujuzi mdogo wa waombaji wa zabuni wa taratibu na mfumo mpya wa zabuni zilizokuwepo. Baadhi ya waombaji wa zabuni ama hawakujaza vizuri *bidding documents* ipasavyo au

hawakuambatanisha nyaraka zinazostahili. Hali ambayo ilisababisha wengi wao kuonekana siyo *responsive*. *Tender* nyingi ama zilirudiwa upya au zilichukua muda mrefu kwenye uchambuzi na upatikanaji wa *no objection* kutoka kwa Wahisani. Tatu, ukosefu wa *Standard Billing Documents* na *contracts/agreements* jambo lililosababisha uondoaji wa *tender* kuchukua muda mrefu.

Nne, ukosefu wa *Procurement Plans (Thresholars)* kwenye hizo Wizara, Idara na Asasi na mwisho viwango vidogo, walivyokasimiwa Maofisa Wahasibu, Wakuu wa Idara na Taasisi kwa manunuzi ya dharura. Aidha, Bodi za Zabuni za Wizara, Mikoa na Wilaya nazo zilipewa viwango vidogo. Hali hii inahitaji *tender* nyingi zifanyiwe maamuzi na *Central Tender Board*. Kutokana na ukosefu huo, Wizara inakusudia kuifanyia marekebisho Sheria ya Ununuzi na Kanuni zake ili kuongeza uwajibikaji na kuimarisha uwezo wa watekelezaji kama inavyosema Ibara ya 43 ya hotuba ya Waziri wa Fedha ya Bajeti.

Kuhusu Mashirika ya Hifadhi ya Jamii kuwajengea nyumba wanachama. Imesema je, Mashirika ya Hifadhi ya Jamii, kama *PPF, NSSF, PF, LAPF* na kadhalika, yana mpango au mikakati gani ya kuwajengea nyumba wanachama wao? Hoja ambayo ililetwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali. Mifuko mbalimbali ilianzishwa hapa nchini kwa madhumuni ya kukusanya michango ya wafanyakazi katika mashirika ya umma, makampuni binafsi na watumishi wa Serikali. Mifuko hiyo, ni pamoja na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF)* na *Local Government Provident Fund (LAPF)*. Mifuko hii huwekeza michango ya wanachama wake katika vitega uchumi mbalimbali, kwa lengo la kupata faida na hivyo kutunisha na kuongeza thamani ya mafao yatakayolipwa wanachama hao baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nieleze kuwa mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma, unao mpango wa kujenga nyumba za gharama nafuu kwa wanachama wake ili utekeleze majukumu yake ya kimsingi na kisheria ambayo ni kuhakikisha mstaafu mwanachama anaishi maisha yanayokaribiana na yale aliyokuwa akiishi akiwa kazini yaani kabla ya kustaafu. Mwanachama anayechangia atauziwa kwa pesa taslimu au kukopeshwa kwa masharti nafuu. Katika kufanikisha azma hiyo, uongozi wa *PPF* umefanya mazungumzo na Mamlaka za Miji za Kibaha, Mwanza na Dar es Salaam ambapo maeneo yanaandaliwa kwa ajili ya shughuli hizo katika miji yote hiyo mitatu. Maandalizi hayo ya kupatiwa maeneo yanategemea kukamilika wakati wowote ili taratibu za ujenzi ziweze kuanza.

Mheshimiwa Spik,a kwa upande wa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma *(PPF)* na kwa kuzingatia michango ya mfuko huu, mikakati ya muda mfupi na muda mrefu imewekwa na kuwekeza michango ya wanachama wake kwa lengo la kutunisha mafao yao pindi wanapostaafu. Kama mkakati wa muda mrefu, mfuko umewekeza kwenye dhamana za mabenki, hasa yale yanayotoa mikopo ya ujenzi kwa kushirikiana na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii kama vile Benki ya Azania. Mkakati wa muda mrefu ni kujenga nyumba za gharama nafuu ambazo zitauzwa kwa wanachama wake au kwa pesa taslimu au kwa njia ya mkopo mwanachama ataweza kupata mkopo wa fedha kwa masharti nafuu ya kujengea nyumba yake mwenyewe kutegemea na matokeo ya utafiti ambao itaanza baada ya mfuko kukamilisha shughuli za maandalizi ya kuanza kulipa mfuko na mafao Julai, 2004.

Kuhusu usitishaji wa mafao ya kila mwezi yaani *Monthly Pension* kwa mwanachama walio chini ya umri wa uzee yaani miaka 55. Hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni. Mifuko ya pensheni duniani pote inazo kanuni na taratibu za utoaji mafao kwa wanachama wake wanapoondoka katika ajira. Aidha, Kanuni na taratibu hizi zinaongoza, masuala ya uandikishaji wa wanachama, ukusanyaji wa michango na uwekezaji. Mafao ya uzeeni kwa wanachama ndiyo nguzo muhimu ya uanzishwaji wa mifuko ya pensheni, nguzo nyingine ni pale mwanachama anapougua au anapofariki dunia na kuwaacha wategemezi. Mafao ya uzeeni mahali popote duniani hutolewa kwa mwanachama aliyefikisha umri wa uzee. Sheria iliyoanzisha Mfuko wa *PPF* ilirekebishwa ili kuwezesha utaratibu wa utoaji wa mafao ya uzeeni ya kila mwezi kuendeana na kanuni na taratibu zinazotumika kuhusiana na mafao hayo. Kutokana na marekebisho hayo, wanachama wanaoondoka katika ajira kabla ya kufikisha umri wa uzee ambayo ni miaka 55 wanapewa sehemu ya mkupuo ya mafao ya uzeeni na mafao ya uzeeni ya kila mwezi *(monthly pension)* yanatolewa wanapofikisha umri wa uzee. Huu ndiyo utaratibu unaotumika katika mifuko yote ya pensheni. Aidha, urekebishaji huu wa Sheria unauwezesha mfuko kuweza kuboresha mafao kwa wazee au pia kuanzisha mafao mengine yanayoendana na mahitaji

halisi katika jamii. Katika marekebisho haya *PPF* imeweza kuanzisha mafao ya elimu, watoto wa wanachama endapo mwanachama atafariki dunia akiwa katika ajira.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Bodi ya Wadhamini wa *PPF*, uongozi na wafanyakazi wote kwa ujumla, kwa jinsi walivyoweza kuanzisha mafao haya muhimu kwa wanachama wake. Jambo ambalo ni muhimu kwa sasa ni elimu kwa wanachama na wananchi wote kwa ujumla juu ya taratibu na kanuni za pensheni. *PPF* imekuwa mstari wa mbele katika kuwaelimisha wanachama na wadau wengine juu ya kanuni na taratibu za pensheni. Mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge kwamba *PPF* iliendesha semina hata kwetu sisi Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni mwaka jana mwezi Juni. Semina hizo zimekuwa zinaendelea kutolewa na *PPF* katika sehemu mbalimbali ikiwa ni pamoja na wanachama ambao wataanza kupata mafao hayo ya uzeeni ya kila mwezi watakapo- fikisha umri unaostahili baada ya kuondoka katika ajira kabla ya kufikisha umri huo. Ni vema elimu hii tuliyoipata na tutakayoendelea kuipata tuitumie katika kuwasaidia wananchi wengine pia. Aidha, nichukue nafasi hii kusisitiza kwamba Serikali kama mojawapo ya wadau katika mifuki ya pensheni itashirikiana na uongozi wa mifuko hii ili kuhakikisha kwamba wanachama wanapata mafao yao wanayostahili kwa mujibu wa kanuni na taratibu za uendeshaji wa mifuko ya pensheni kama zinavyoelekezwa katika sheria zilizoanzisha mifuko hiyo ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa mafao mengine yanayoigusa jamii kama haya ya elimu yaliyoanzishwa na *PPF*.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

SPIKA: Kabla hatujaendelea, nimeombwa kutangaza Kikao cha Wabunge wote wa CCM asubuhi hii mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge, Wabunge wote wa CCM.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu kwenye hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, waliochaguliwa hivi karibuni na wameungana na sisi katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwapongeze Ndugu Kitillya kwa kuteuliwa kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na Ndugu Luoga, kuwa Naibu Kamishna Mkuu, naamini kwamba wataongeza pale alipoishia Ndugu Sanare na kwamba ufanisi utaongezeka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango ambayo wameitoa, imekuwa ya manufaa makubwa na imetusaidia Serikali kuona mahali gani tunahitaji kuparekebisha. Wananchi wa Jimbo langu la Magu wameipokea Bajeti hii kwa faraja kubwa na wana matumaini kwamba utekelezaji wa Bajeti hii utakuwa wa makini kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Jimbo la Magu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nianze kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucas Selelii, alitoa hoja kwamba, makusanyo yanayotokana na ushuru wa forodha yameshuka. Ni kweli kwamba thamani ya bidhaa zinazoingizwa nchini imeongezeka ukilinganisha na mwaka 2001/2002. Hali kadhalika, kodi iliyokusanywa inaonekana kuwa ni kidogo ukilinganisha na thamani ya bidhaa zilizoingizwa. Hii inatokana na ukweli kwamba idadi ya wawekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji yaani *Tanzania Investment Centre* na wale wa Madini wameongezeka kwa kuwekeza katika sekta mbalimbali hapa nchini. Hata hivyo, bidhaa zilizoingizwa na wawekezaji hao, zilihesabiwa kama bidhaa za mitaji yaani *capital goods* na hazikutozwa kodi.

Bidhaa hizo ni pamoja na mashine na mitambo mbalimbali yenye thamani kubwa. Pamoja na wawekezaji hao kuna misamaha mingine ya kodi inayotolewa kwa mashirika ya hiyari na yale yasiyo ya Kiserikali yaani *NGOs*, mashirika ya dini, miradi inayofadhiliwa na Serikali za nje kama ya ujenzi wa barabara na kadhalika, watu binafsi, mashirika ya umma na wafanyakazi mbalimbali. Bidhaa zote hizo zina thamani kubwa lakini hazilipiwi kodi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa William Kusila na Mheshimiwa Suleiman Sadiq, walitoa hoja juu ya mabadiliko ya viwango vya ushuru wa forodha kwenye matairi ya magari. Serikali imeamua kupunguza ushuru wa forodha kwa matairi ya *Radial* kutoka asilimia 15 hadi asilimia 10, kwa lengo la kupunguza gharama za usafirishaji wa mizigo na abiria wa masafa marefu. Kwa kuzingatia kuwa barabara zetu ziko katika hali mbaya, hivyo ni matairi ya aina ya *Radial* pekee yanayoweza kuhimili safari hizo pasipo kupasuka ovyo na kusababisha ajali zinazoleta maafa makubwa na uharibifu wa mali. Serikali inatoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 matairi ya aina ya *nylon*, *VAT* ya asilimia 20 na ushuru wa muda yaani *Suspended Duty* wa asilimia 40.

Matairi ya aina hii ndiyo yale ambayo yanatengenezwa na Kiwanda chetu cha *General Tyre Limited* cha Arusha. Lengo la uamuzi huu ni kulinda kiwanda hiki ambacho kinatoa ajira kwa wananchi na kinachangia mapato ya Serikali kwa kodi mbalimbali. Kwa msingi huo, wasafirishaji wadogo wadogo ambao wanatumia matairi ya aina ya *nylon*, wanashauriwa kutumia matairi yanayotengenezwa nchini ambayo ni madhubuti na yana ubora unaokubalika Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja juu ya kodi katika dawa za mbu na vyandarua. Waliotoa hoja hii ni Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalfan, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Benson Mpesya na Mheshimiwa *Capt*. Theodos Kasapira.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004, Mheshimiwa Waziri alipendekeza kufanya marekebisho kadhaa katika mfumo wa ushuru wa forodha. Kati ya marekebisho hayo, Mheshimiwa Waziri alipendekeza kuongeza ushuru wa forodha kwa dawa za mbu zinazoagizwa kutoka nje kutoka kiwango cha asilimia 10 hadi 15 na kuanza kutoza ushuru wa forodha kwa vyandarua vinavyoagizwa kutoka nje kwa kiwango cha asilimia 10 ukilinganisha na kiwango cha sasa cha asilimia zero.

Mheshimiwa Spika, sera ya Serikali kwa bidhaa hizi pamoja na madawa ya binadamu na ya kuua wadudu imekuwa ni kutotozwa kabisa kodi au kutoza viwango vya chini ili kuzifanya zipatikane kwa urahisi na kwa bei nafuu zaidi ambazo wananchi watazimudu. Aidha, bidhaa hizi zimekuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi kwa kuwa uzalishaji wake hapa nchini umekuwa hautoshelezi mahitaji halisi au kutozalishwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, mtazamo wa sera hii ni wa muda tu hadi hapo uwezo wetu wa uzalishaji hapa nchini utakapoongezeka. Kwa kuwa hakuna kiwanda cha kuzalisha dawa za vyandarua kama NGAO, msamaha wa kodi unaotolewa kwa dawa hiyo utaendelea kama ilivyo kwa pembejeo za kilimo na uvuvi. Nasisitiza kwamba hakuna mpango kwa sasa, napenda nirudie sehemu hiyo. Kwa kuwa hakuna kiwanda cha kuzalisha dawa za vyandarua kama NGAO, msamaha wa kodi unatolewa kwa dawa hiyo hivi sasa utaendelea kama ilivyo kwa pembejeo za kilimo na uvuvi. Napenda kusisitiza kwamba hakuna mpango kwa sasa wa kutoza kodi dawa ya ngao, pembejeo za kilimo wala vifaa vya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua inayopendekezwa na Serikali ya kuongeza kidogo ushuru wa forodha kwa vyandarua na dawa za mbu inalenga kujenga uwezo wa uzalishaji, kuongeza ajira na kuweka hali ya ushindani wa haki na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Kulingana na takwimu zilizopo kwa mwaka wa fedha 2001/2002 vyandarua vya thamani ya shilingi milioni 11,310,803 viliagizwa toka nje. Serikali ilikusanya ushuru wa shilingi milioni 1,131,080.30, kiasi hiki ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji ya ndani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lekule Laizer, alitoa hoja kwamba mitambo ya kutengeneza barabara inayoingizwa nchini kwa muda isitozwe kodi. Mashine, vifaa na mitambo ambavyo vinaingizwa nchini kwa muda kwa ajili ya ujenzi wa barabara vilikuwa vinatozwa ushuru wa forodha wa asilimia 5 kwa mwezi kwa mujibu wa *Government Notice*, Nambari 133 ya mwaka 1996. Hata hivyo, hivi sasa mashine, vifaa na mitambo hiyo haitozwi tena ushuru wa forodha na kodi ya ongezeko la thamani kwa mujibu wa Sheria ya kodi hizo wakati vinapoingizwa nchini kwa sababu hivi sasa vipo kwenye kundi la bidhaa za

mtaji yaani *capital goods*. Kutokana na kupitwa na wakati *GN* nambari 133 ya mwaka 1996 ni moja ya *GNs* ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha atazifuta mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja inayohusu ada ya asilimia 5 kwa vifaa vya wawindaji wakubwa. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Stephen Kazi. Asilimia 5 iliyoondolewa kwenye bunduki na vifaa vya uwindaji si ada bali ni ushuru wa forodha kwa vifaa vya aina hiyo. Tangazo la Serikali Na. 133 la mwaka 95 liliweka ushuru wa asilimia 5 kwa mwezi kwenye vifaa hivyo, vifaa hivyo vina ushuru wa asilimia 25.

Kwa hiyo, kuweka asilimia 25 kwa mwezi ina maana baada ya miezi mitano mwingizaji atakuwa analipa zaidi ya kiwango cha juu cha vifaa hivyo ambavyo si sahihi. Pia utaratibu wa kuingiza vifaa kwa muda yaani *temporary importation* hauhitaji kulipa ushuru bali kuweka dhamana endapo vifaa hivyo vitapotea. Kwa vile wawindaji wa kitalii huja kwa muda na ili kuhamasisha uwindaji wa kitalii unaoleta fedha nyingi za kigeni, Serikali imeona utaratibu wa kawaida ulio kwenye Sheria Mama ya *Temporary Importation* uendelee kutumika.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja juu ya misamaha ya kodi na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga. Lengo la kutoa msamaha wa kodi kwa magari ya watumishi wa Serikali na ili wayatumie katika shughuli za kikazi yaani *official duties* na si biashara, endapo mtumishi anafanya biashara ni wazi kuwa anajiweza hivyo hana sababu ya kuomba msamaha wa kodi. Kwa mtumishi ambaye ana gari lenye msamaha wa kodi anaruhusiwa kulisajiri kama *taxi* mara baada ya kulipa kodi alizosamehewa awali na kufanya biashara yake kama wanavyofanya wafanyabiashara wengine. Dhana ya kuinua hali ya maisha ya watumishi kwa njia ya misamaha ya kodi si nzuri, nia ya Serikali ni kuinua hali ya maisha ya watumishi wake, kwa kuwaongezea mishahara na mafao mengine kila mara hali ya uchumi inaporuhusu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, alitoa hoja kwamba kufutwa kwa kodi kwa Taasisi mbalimbali kwa magari yenye uwezo wa *CC 3,000* linatia shaka kwa wenye magari ya mkonga.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa magari kwa ajili ya kuweka viwango vya ushuru wa forodha, inategemea uwezo wa kubeba abiria yaani *sitting capacity*. Magari ambayo yamependekezwa msamaha wake usitolewe kwa *engine* zenye uwezo wa *CC 3,000* ni yale yanayochukua abiria tisa ikiwa ni pamoja na dreva. Magari yenye mkonga ambayo Mheshimiwa Mbunge anayazungumzia na ambayo huhimili vishindo vya porini, ni yale yenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 10. Magari haya yanajulikana zaidi kama *hardtop* na yana milango mitatu. Haya hayamo katika utaratibu uliotajwa na hivyo yataendelea kupata msamaha wa kodi kama hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ernest Mabina, alitoa hoja kwa nini Kitengo cha Kukagua Magari kisiwe cha ndani ya nchi badala ya kutumia kampuni ya nje. Sheria za nchi zinaipa mamlaka Shirika la Viwango Tanzania yaani *TBS*, kukagua na kuridhia kuingia nchini bidhaa zote ambazo zinatakiwa kuthibitishwa ubora wake kabla ya kuingizwa nchini ikiwa ni pamoja na magari yaliyotumika. Ili kudhibiti na kuhakikisha kuwa magari mabovu ambayo hayafai kutembea barabarani hayaingii nchini, Serikali iliamua kuingia makubaliano na Kampuni ya Japan ya *Automobile Appraisal Institute* ili kuthibitisha ubora na uwezo wa kutembea barabarani yaani *road worthness* wa magari hayo kabla hayajaletwa nchini.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inasaidia kuepusha gharama kwa mwagizaji ambaye endapo gari hilo lingekaguliwa hapa nchini na kuonekana halifai, fedha aliyotumia mwagizaji huyo ingepotea bure. Kwa kukagua magari nje ya nchi kunamwezesha mwagizaji kununua gari lingine ikiwa alilotaka kulileta nchini litaonekana halifai na hivyo kutoingia hasara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Christopher Wegga, alitoa hoja kwa nini sukari ya hapa ndani haipati soko, sukari inaingia kiholela na kwa nini mianya ya rushwa haizibwi? Serikali imekuwa inachukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kulinda viwanda vya ndani kutokana na ushindani usio sawa wa bidhaa toka nje. Ulinzi huo unatolewa pia kwa wazalishaji wa sukari.

Huko nyuma kulikuwa na uingizaji holela wa sukari ambao ulisababisha viwanda vya ndani kuyumba, Serikali ilichukua hatua za kuzuia uingizaji wa sukari kwa kuwapa vibali waagizaji wa sukari kwa matumizi ya viwandani, vibali hivyo vimetolewa kwa tangazo la Serikali na vinaonyesha mahitaji ya kila mwagizaji kwa kipindi fulani kutokana na ushauri wa Bodi ya Sukari. Hii ni kutokana na ukweli kwamba viwanda vyetu havizalishi sukari ya viwandani. Serikali kupitia *TRA* inaendelea kupambana na wale wote wanaoingiza sukari kwa magendo. Serikali inawaomba na kuwashauri wazalishaji wa sukari kufungua vituo vya usambazaji katika Mikoa ambako hawana vituo.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba wafanyabiashara wengi wamekimbilia Mombasa kwa vile Kampuni ya *ICS* inaleta kero kwa kukadiria thamani kubwa ya mizigo inayoingia Dar es Salaam tofauti na thamani halisi ya bidhaa hizo. Pia wafanyabiashara wa Zanzibar wanapata usumbufu mkubwa kwa mizigo inayotoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam. Walitoa hoja hii ni Mheshimiwa Issa Mohamed Salim na Mheshimiwa Job Ndugai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Ukaguzi wa Bidhaa kabla hazijaingizwa nchini yaani *Pre-Shipment Inspection* unaotekelezwa na *COTECNA*. Unatoa fursa kwa Serikali kuteua Mkaguzi yaani *Auditor* ambaye kwa sasa ni *ICS*, kukagua utendaji wa *COTECNA*, ukaguzi huu ni kuhusu jinsi bidhaa zilivyoainishwa, zilivyohakikiwa ubora, uwingi wake na pia thamani yake. Mamlaka ya Mapato Tanzania imepata malalamiko kama Waheshimiwa Wabunge wanavyoeleza na hivyo kulazimika kuchukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwaeleza *ICS* kuzingatia masharti ya mkataba huu na kufuata taratibu za uthamini wa mizigo kama zilivyopitishwa na Bunge hili Tukufu mwaka 2001 bila kusababisha bughudha na kero kwa wafanyabiashara.

Aidha, majadiliano ya mara kwa mara baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA), COTECNA* na *ICS* yameonyesha mwelekeo wa kupunguza bughudha na kero hizi. Hata hivyo, Serikali imeweka utaratibu wa kuachana na ukaguzi wa mizigo nje ya nchi yaani *PSI* na kuanza utaratibu wa kukagua bidhaa baada ya kufika nchini yaani *destination inspection.* Utaratibu huu utakwenda sambamba na matumizi ya mitambo ya ukaguzi yaani *Container Scanners* za kukagua bidhaa yote ndani ya makasha yaani ndani ya *container*.

Katika kuimarisha na kuboresha utaratibu huu, Serikali inatarajia kuacha matumizi ya mtandao wa kompyuta ulioko sasa wa *ASCUDOR* 2.7 wenye mapungufu mengi kiutekelezaji na kuanza kutumia *ASCUDOR* ++ ambayo ina taratibu za kiforodha za kisasa kama *Computerize Risk Management System* pamoja na uwekaji wa kumbukumbu za uthamini mahiri wa bidhaa yaani *transaction price data base*. Hatua hizo zinalenga na zina nia ya kujenga uwezo wa watumishi wa *TRA* na mawakala wa forodha kwa kufanya mafunzo ili kuwezesha ufanisi mzuri zaidi. Pia Serikali inakusudia kuoanisha *Computer Systems* za mamlaka ya mapato na zile za mawakala au wafanyabiashara ili waweze kuwasilisha nyaraka na kadhia kwa njia ya mtandao toka Maofisini kwao bila kulazimika kuwakilisha kadhia au nyaraka hizo Ofisi za *TRA. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kero wanazopata wafanyabiashara wa Zanzibar kwa mizigo inayotoka Zanzibar kupitia Bandari ya Dar es Saalam ni kuwa, kuna baadhi ya taratibu za kiforodha na kuna aina fulani za kodi ambazo hazitozwi kwa mizigo inayopitia Zanzibar.

Kwa mfano, mizigo inayoingizwa Tanzania Bara yenye thamani zaidi ya dola za Kimarekani 5,000 zinapitia utaratibu wa ukaguzi wa nje ya nchi yaani *Pre-shipment Inspection*, utaratibu ambao hauko Zanzibar. Mwingizaji hutakiwa kulipa gharama ya asilimia 1.2 ya thamani ya mzigo huo. Pia kuna baadhi ya bidhaa ambazo hazitozwi ushuru wa ziada yaani *suspended duty* zinapoingizwa Zanzibar. Ili kuwa na ushindani wa haki bidhaa hizo zinapoletwa Tanzania Bara hutakiwa kulipia gharama za ukaguzi na ushuru wa ziada endapo haukulipwa Zanzibar. Kwa bidhaa zile ambazo hazina matatizo niliyoyaainisha hapo juu, hazitozwi kodi yoyote ziingiapo Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, alitoa hoja inayohusu kusamehe kodi ya mapato Mfuko wa Mazao kwa Mkoa wa Kagera, *Kagera Farmers Trust Fund.* Mfuko huu hauna sifa za kupewa msamaha wa kodi ya mapato kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 14 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973. Awali mfuko huu uliombwa kusamehewa kodi ya mapato kwa misingi ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, inasaidia katika kuondoa umaskini wa wananchi wa Muleba, Bukoba Vijijini na Mjini. Pili, lengo lake ni kutoa huduma kwa wakulima katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mfuko huo hayaendani na masharti yaliyomo katika Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 kwa sababu zifuatazo:

Moja, *Kagera Farmers Trust Fund* haijishughulishi tu na kutoa huduma bali inakopesha na kupata riba kutoka *Kagera Cooperative Union.* Kisheria riba inatozwa kodi.

Pili, Mheshimiwa Spika, Mfuko huu pia huwekeza fedha zilizopatikana kama viingilio, ada za wanachama ama michango ya hiyari katika vitenga uchumi mbalimbali na mwisho kutoa zawadi au mikopo kutoka katika mapato yatokanayo na amana za mfuko kwa yule anayewahudumia wakulima.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja na Mheshimiwa Athumani Janguo ya utozaji ada ya Ukurugenzi, swali ambalo limejibiwa leo hii. Kwa mujibu wa Sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 1973, utozaji wa kodi ya mapato hufanyika pale mlipa kodi anapopata mapato, mapato yanayotozwa kodi ya mapato ni yale yanayotokana na ajira, biashara na mengineyo. Kimsingi mapato anayopata Mkurugenzi ambaye sio mfanyakazi wa kudumu wa Taasisi husika yaani *Non full-time Director* kama ada ya Ukurugenzi yalikuwa yanatozwa kodi chini ya mfumo wa kodi ya ajira yaani *Employment Tax.*

Kwa vile ulipaji wa kodi kwenye ada hizo haukuwa unafanyika kwa hiyari: napenda kurudia, kwa vile ulipaji wa kodi kwenye ada hizo haukuwa unafanyika kwa hiyari na ukwepaji ulikuwa mkubwa, Serikali iliamua kuifanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Mapato ili kutoza kodi kwenye mapato hayo kwa mfumo wa zuio yaani withholding. Lengo ni kuziba mianya ya ukwepaji kodi katika eneo hili na kuleta usawa katika utozaji wa kodi ya mapato. Mfumo huu hauongezi mzigo wowote bali unaleta usawa katika utozaji wa kodi ya mapato kwani baadhi ya wastaafu hao wengine ni wafanyabiashara au wamejiajiri na wanatozwa kodi ya mapato.

Mheshimiwa Ponsiano Nyami, alitoa hoja kwamba makadirio yanayofanywa na *TRA* kwa wafanyabiashara katika Mikoa ya Mbeya na Rukwa ni makubwa. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato *TRA* hutoza kodi kwa mujibu wa Sheria za kodi wanazozisimamia, kila Sheria ya kodi imeeleza misingi na taratibu za makadirio na namna ambavyo kodi husika italipwa. Aidha, Sheria hizo zinaeleza aina ya kumbukumbu na taarifa ambazo walipa kodi hutakiwa kuzionyesha kwa wakadiriaji wa kodi ili zitumike kama msingi wa makadirio ya kodi husika. Hatuna ushahidi wowote wa kuonyesha kuwa misingi ya Kisheria inakiukwa katika Mikoa ya Mbeya na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Rufaa za Kodi ya mwaka 2000 pia imebainisha haki na utaratibu wa walilipa kodi kupinga makadirio yenye mapungufu. Sheria hiyo hivi sasa inafanya kazi na taarifa zilizotufikia zinaonyesha kwamba rufaa nyingi zimeishashughulikiwa na Bodi na Baraza la Kodi ambavyo ni vyombo vilivyoanzishwa chini ya Sheria hiyo.

Hata hivyo, bado lipo tatizo la walipa kodi wengi kutokutunza kumbukumbu sahihi za biashara zao ama kwa kutokupenda kufanya hivyo au kwa kukosa utaalam. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali imerekebisha viwango vya kodi kwa wafanyabiashara wadogo. Aidha, *TRA* imeendelea kuhimiza kuweka wazi viwango na vigezo vya makadirio ikiwa ni pamoja na kuonyesha viwango vya kodi ya mapato kwenye mbao za matangazo ofisini.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye maswali yaliyoulizwa, kwenye eneo la mfumo wa kodi ya ongezeko la thamani yaani *VAT.* Ilitolewa hoja kwamba kiwango cha *VAT* cha asilimia 20 kishushwe kama nchi jirani zilivyofanya. Waliotoa hoja hii ni Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Remidius Kissassi na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro.

Mheshimiwa Spika, tangu Tanzania ianzishe kodi ya *VAT* mnamo mwaka 1998 kiwango chake kimebakia kuwa asilimia 20. Kiwango hiki kinaipatia Serikali mapato mazuri ikilinganishwa na yale yaliyokuwa yanapatikana chini ya mfumo wa kodi ya mauzo ambayo ilifutwa tarehe 1 Julai, 1998. Endapo

Serikali itashusha kiwango hiki cha *VAT* na kuzingatia pendekezo letu la kuondoa baadhi ya kodi za Serikali za Mitaa, ikiwemo na kodi ya maendeleo, italazimika kutafuta vianzio vingine vya mapato kwa ajili ya kuziba pengo litakalojitokeza. Pamoja na ukweli kwamba nchi jirani ya Kenya imeshusha kiwango cha *VAT* kutoka asilimia 18 hadi asilimia 16, ni vema tukazingatia yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, moja, Tanzania inakusanya asilimia 12.5 tu ya pato la Taifa tofauti na Kenya inayokusanya asilimia 25 ya Pato la Taifa. Pili, viwango vya kodi nyingine kwa mfano ushuru wa bidhaa ni vikubwa nchini Kenya ukilinganisha na vile vinavyotozwa Tanzania. Kenya imeweka viwango hivyo vikubwa ili kufidia kiwango kidogo cha *VAT* wanachotoza. Kwa mfano, bia, sigara, soda na kadhalika Kenya wanatoza viwango vikubwa zaidi. Endapo Serikali itashusha kiwango cha *VAT* basi itabidi kupandisha viwango vya kodi nyingi ili kufidia pengo litakalojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Edson Halinga, alizungumzia juu ya *VAT* kwenye maji, umeme na simu. Maji hayatozwi *VAT* hata mamlaka za maji safi na majitaka hazilipi *VAT* kwa baadhi na au huduma zinazopata kwa ajili ya kuendeleza majukumu waliyopewa. Umeme na simu hutozwa *VAT*. Ni vizuri kuzingatia kwamba *VAT* ni kodi inayotozwa kwa mtumiaji wa bidhaa ya huduma. Kadri matumizi yanavyoongezeka ndivyo mlaji anavyolipa kodi kubwa, ni vema wananchi wakaelimishwa na wakalielewa suala hili la kubana matumizi kwenye umeme na simu ili wasilipe *VAT* kubwa.

Mheshimiwa John Singo, alitoa hoja juu ya msamaha wa *VAT* kwa magari ya Wabunge. Utakumbuka Mheshimiwa Spika ya kwamba, Bunge lako Tukufu la Bajeti 2001/2002 lilifuta unafuu wa *VAT* kwa Serikali na Taasisi zake, kwa hivi sasa Mheshimiwa Rais analipa *VAT* kwenye manunuzi, bidhaa na huduma, hata Serikali na Taasisi zake sasa zinalipa *VAT* na pia watumishi wa Serikali nao hulipa *VAT* wanaponunua magari yao. Kutokana na maelezo hayo niliyoyatoa hapo juu ikiwa ni pamoja na suala la usawa kwenye mfumo mzima wa kodi, ni busara kwa Waheshimiwa Wabunge kulipa *VAT* kwenye magari yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, alitoa hoja inayohusu Vyama vya Msingi kwamba havijarejeshewa *VAT* inayolipwa na wakulima wakati wa kusafirisha, kusindika na kwenye vifungashio vya mazao ya kuuza nje. Wakulima wanaouza mazao nchi za nje ili kurejeshewa kodi ya *VAT* wanayolipa, wanapaswa kupitia Vyama vya Msingi, Vyama vya Ushirika na vyombo vingine vya wakulima vilivyosajiliwa na *TRA*. Kodi inayorejeshwa ni ile inayolipwa kwenye ukoboaji, usindikaji wa mazao, gharama za usafiri hadi kwenye minada na huduma za bandarini. Takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba Vyama vya Wakulima vya *Kilimanjaro Native Cooperative Union 1984 Limited*, *Kagera Cooperative Union 1990 Limited* na *SHIRECU 1984 Limited* vimerejeshewa kodi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, *Kilimanjaro Native Cooperative Union* imerejeshewa shilingi milioni 42,017,883.40 tarehe 23 Julai, 2002 na nambari ya hundi ni 713421, *Kagera Cooperative Union 1990 Limited* imelipwa kama marejesho ya *VAT*, shilingi milioni 37,764,961.22 tarehe 16 Agosti, 2002, nambari ya hundi ni 713469 na *SHIRECU* ililipwa tarehe 4 Oktoba, 2002 shilingi milioni 49,366,838 na nambari ya hundi ni 713601.

Kwa hiyo, tangazo ama msamaha wa kodi kwa wakulima kwa kodi hiyo ya *VAT* imeshaanza kutekelezwa lakini kinachosisitizwa ni kwamba ili uweze kurejeshewa ni lazima uwe umesajiliwa na *TRA*. Kwa hiyo, wakulima wanasajiliwa kwa kupitia vyama vyao hivi vya ushirika ama *associations* nyingine ili waweze kurudishiwa kodi hiyo ya *VAT* kupitia vyombo hivi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, alitoa hoja ya kuondolewa *VAT* kwa zao la miwa na tumbaku. Mazao yote ya kilimo ambayo hayajasindikwa yana msamaha wa *VAT*. Msamaha huo umewekwa wazi chini ya kipengele cha kwanza, kipengele kidogo cha tano kwenye jedwali la pili la Sheria ya *VAT* ya mwaka 1997. Miwa na tumbaku ni miongoni mwa mazao yaliyoorodheshwa katika kipengele hicho na hivyo hayatozwi *VAT*. Pamoja na kusamehewa *VAT* pembejeo za kilimo zina msamaha wa *VAT* kwa mujibu wa vipengele Na. 2 na 13 vya jedwali la pili la Sheria ya *VAT* ya mwaka 1997. Namshauri Mheshimiwa Mbunge aipitie kwa makini Sheria hii ya *VAT*.

Mheshimiwa Spika, sasa nitajielekeza kwenye kodi nyingine, moja, kuhusu *Property Tax*, hoja ya Mheshimiwa Ponsiano Nyami, ambapo anasema itazamwe upya. Kodi ya Majengo na mali nyingine *(Property Tax)* inasimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kodi hii ambayo ni chanzo kizuri na muhimu cha mapato ya Mamlaka hizo haikusanywi kikamilifu ikilinganishwa na wingi wa wamilikaji wa majengo na mashamba katika maeneo mengi. Kwa vile Serikali imefuta Kodi ya Maendeleo, ni vema sasa Mamlaka husika zikaimarisha mikakati ya kukusanya kodi hii pamoja na wigo wake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, ametoa hoja ya Ushuru wa Bandari Ziwa Victoria, vyombo vya usafiri majini vilivyosajiliwa kama vivuko, ni kweli kuwa abiria wake hawatozwi Ushuru wa Huduma za Bandari *(Port Service Charge)* wakati meli au boti ambazo hazitofautiani na vyombo vile vinavyotoa huduma ya abiria kati ya Dar es Salaam na Zanzibar abiria wake hutozwa ushuru huo. Serikali inalifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Abdula Lutavi, alitoa hoja kuongeza makusanyo ya mapato yasiyokuwa ya kodi...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

SPIKA: Malizia Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, kulikuwa na masuala mbalimbali ambayo yametolewa kuhusu mambo ya fedha, noti bandia, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, alitoa hoja kuhusu udhibiti wa noti bandia na masuala mengine mbalimbali yanayohusu sekta ya fedha. Benki Kuu imetoa jarida linaloitwa *Monetary Policy Statement* la Juni 2003. Kijarida hiki kimeeleza mambo yote yanayohusu fedha, kuhusu *interest rate, inflation*, mikopo, *bank supervision* na kadhalika.

Nashauri Waheshimiwa Wabunge tukisome kijarida hiki kwa sababu kinatoa maelezo ya kina kwa utekelezaji wa sera za fedha mwaka uliopita na mwaka huu tunaokwenda, matarajio katika vigezo na viashiria mbalimbali vikoje. Kwa hiyo, naomba tukisome kijarida hiki itatupunguzia sana maswali pamoja na kuwaelimisha wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini jinsi hoja zilivyokuwa nyingi ndio maana nimechukua muda mrefu kuyaeleza, yale ambayo tumebakiza Mheshimiwa Waziri wa Fedha atayamalizia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukupongeza wewe kwa kutuongoza vizuri katika Bunge hili, tunakupongeza sana, ahsante sana. Vile vile niwapongeze Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wetu kwa kutuongoza vizuri katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Katibu Mkuu wangu Ndugu Enos Bukuku na wafanyakazi wote wa Mipango na Asasi zake, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliochangia katika hoja ya mipango ni wengi na ninashukuru karibu wote walisema safari hii mipango na Bajeti ni ya matumaini. Naomba nichukue fursa hii kuwatambua nao ni Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kwa niaba ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Irenius Ngwatura, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Getrude Mongella, Mheshimiwa Ramadhan Khalfan, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila,

Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo na Mheshimiwa Jumanne Nguli. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa *Capt*. Theodos Kasapira, Mheshimiwa Abdula Lutavi, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Issa Mohamed Salim, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Kidawa Saleh, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Mwanamkuu Kombo, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Dr. Talala Mbise na Mheshimiwa Frank Magoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda niwatambue waliochangia kwa maandishi, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Profesa Mark Mandosya, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Omar Ramadhani Mapuri, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mheshimiwa Sijamini Mohammed Shaame, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Mossy Mussa, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Iddi Simba, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya na Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote hawa, tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo mazuri ya mpango na Bajeti yetu katika kipindi hiki kusema kweli yametokana na ushirikiano mzuri kati ya Serikali na Bunge katika kuweka mambo sawasawa. Nazishukuru sana Kamati zote za Bunge ambazo zimeboresha mipango yetu pamoja na Bajeti yetu. Namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Njelu Kasaka, kwa ushauri ambao alitupa ili kuboresha hotuba yetu ya mipango ya mwaka huu. Nadhani kwa Bajeti hii, sisi Waheshimiwa Wabunge tunajishauri kwamba tukitoka hapa twende Majimboni tukaitekeleze ili tuweze kuiboresha zaidi na kupata mafanikio zaidi kwa mwaka ujao. Huu ni mpango shirikishi unaotekelezeka na wenye matumaini.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza, nimekaa Bungeni kwa kipindi cha miaka saba, hatujapata mchango wa kuboresha hotuba zetu mzuri zaidi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kama uliotokea safari hii. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile katika kipindi chote cha miaka saba hata siku moja nilikuwa sijaona Wabunge kutoka Upinzani kusema wanaunga mkono hoja. Lakini yote ambayo wametuandikia kwa kweli wengi wamesema wanaunga mkono hoja. Kama jana alivyosema Mheshimiwa Frank Magoba, hatuzungumzii itikadi, tunazungumzia suala la kuleta maendeleo katika Taifa letu. Kwa hiyo, nafurahishwa na kauli ya Mheshimiwa Semindu Pawa, jana aliposema atakayekataa hotuba hii maana yake anataka wananchi wetu tusiwafutie kodi, tusiwawekee mazingira bora, nitashangaa nani hataki kura tena mwaka 2005. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chama legelege huzaa Serikali legelege, nadhani kwa mipango na Bajeti hii tunakubaliana wazi kwamba Chama cha Mapinduzi ni Chama imara na ni Chama ambacho kitaendelea kutawala kwa sababu ni Chama ambacho kimezalisha Serikali imara. Naomba tumpongeze sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa uongozi wake bora kama Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi na chini ya uongozi wake Tanzania sasa tuko katika ramani ya ulimwengu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo langu la Handeni na wao wanashukuru sana. Kama alivyosema Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Benson Mpesya na Waheshimiwa Wabunge kutoka Mwanza kwamba watu walikesha kwa kufurahi, hata watu wa Jimbo langu la Handeni wamefurahishwa sana na Bajeti hii na wamenipigia simu wakasema ingekuwa hili ndio Bunge la mwisho kuelekea kwenye uchaguzi wa Majimbo, wana CCM wote tungepita bila kupingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wananchi vijijini wanataka matokeo na sio nadharia. Tukasaidiane nao tulete matokeo mazuri katika kipindi kijacho katika kutekeleza mpango wetu kutokana na bajeti iliyoletwa.

Mheshimiwa Spika, tumepokea michango mingi sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ambayo ilikuwa na mantinki. Mingi ya michango hiyo ilikuwa inagusia zaidi uchumi jumla na mengine yalikuwa yanagusia zaidi kisekta. Sasa nitajaribu kugusia tu maeneo kadhaa ambayo ni ya uchumi jumla na nina hakika kabisa kwamba yale ya kisekta kwa sababu bado Wizara zetu hazijaleta bajeti zao, yatajibiwa vizuri sana kwa umakini na kwa ufanisi zaidi. Nina hakika kwamba masuala ya kisekta yatakapojibiwa na haya ambayo tunayatoa kwa ajili ya uchumi mkuu, tutakuwa tumeshajibu hoja nyingi za Waheshimiwa Wabunge. Lakini napenda kuwahakikishia kwamba Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji tutajibu hoja zote na ni hoja za siku nne siwezi kuzijibu zote peke yangu ni nyingi sana, tutazijibu zile na tutatoa vijarida na tutafikisha kwa kila Mheshimiwa Mbunge ili aweze kuziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimsingi, katika hoja ya mipango jambo kubwa lililojitokeza kwa Waheshimiwa Wabunge lilikuwa ni kwamba, ndio, tunasema uchumi jumla unakua lakini sasa uchumi huu jumla kukua kwake utawezaje kuboresha maisha ya wananchi vijijini? Hilo ndilo lilikuwa suala la msingi kwa Wabunge wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia kukua kwa Pato la Taifa tumefikia asilimia 6.2, tumezungumzia kuteremka kwa mfumuko wa bei tumefikia karibu asilimia 4.2 hivi, tumezungumzia kuongezeka kwa fedha zetu za kigeni kwamba sasa tunaweza kuagiza bidhaa kutoka nje kwa zaidi ya kipindi cha miezi mitano na zaidi, tumezungumzia suala la kuongeza uwiano kati ya mapato na Pato letu la Taifa. Yote haya ni masuala ambayo kwa kweli yamejiweka vizuri kwa maana ya kuzungumzia viashirio vya uchumi mkuu katika harakati za kupunguza umaskini. Sasa tunajiuliza mafanikio haya yatawafikiaje wananchi kule vijijini?

Mheshimiwa Spika, napenda kumuunga mkono Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Vijijini nafikiri.

MBUNGE FULANI: Mbeya Mjini.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mbeya Mjini, aliposema mafanikio ya uchumi jumla kuwafikia wananchi sio kwa Serikali kubeba makontena ya mafanikio na kuyapeleka kijijini, nadhani jana alisema hivyo na nakubaliana naye sana. Suala la msingi ni kwa Serikali kuendelea kujenga mazingira mazuri kuhakikisha kwamba kuna *trickle down effect* ya yale mafanikio ya uchumi jumla kwenda kwenye uchumi wa kaya.

Mheshimiwa Spika, moja ya mifano iliyojitokeza katika Bajeti yetu hii na mipango yetu na najua Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana kwanza Serikali imefuta Kodi ya Maendeleo ambayo tulisema ilikuwa kero kubwa sana. Serikali imepunguza kodi ya wafanyabiashara ndogo ndogo, Serikali ilifuta ada za shule, Serikali imeanza kutoa pembejeo katika kilimo kwa Mikoa iliyotajwa, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu na mawasiliano na tunapozungumzia miundombinu hapa tunazungumzia miundombinu laini, migumu na ile ya kitaasisi, Serikali imeendelea kuandaa mfuko wa

vijana na akina mama ambao utawasaidia katika shughuli zao, Serikali imepunguza kodi ya wavuvi, Serikali imeanzisha mfuko wa kuendeleza wafugaji, Serikali imeimarisha *credit guarantee scheme* kwa wana ushirika katika kununua mazao yao, Serikali imeongeza pensheni, Serikali inaandaa utaratibu wa ardhi kuwa na thamani ili iwe dhamana ya kupata mikopo na Watanzania wote tunayo ardhi, Serikali inaendelea kusomesha watoto yatima na wasiojiweza, Serikali inaendelea na mkakati wa kupunguza umaskini yaani kuboresha huduma za elimu, maji, afya, barabara vijijini, ajira na mapato, Serikali ina mikakati karibu miwili, mitatu ya kuendeleza kilimo tuna *agricultural sector development programme* ambao nia yake ni kuboresha pembejeo, masoko, ugani na utafiti katika kilimo vile vile tuna mkakati wa maendeleo vijijini. Zaidi ya hapo, tuna mpango kamambe wa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji maji ambacho Waheshimiwa Wabunge wengi walisisitiza kwamba tukifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imedhamiria kabisa kuendeleza kilimo hiki cha umwagiliaji. Uchunguzi umeshafanyika na umebainisha kuwa kuna hekta 29.4mil zinazofaa kuendelezwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Kati ya hizo hekta 2.3 milioni zina fursa kubwa, hekta 4.5 milioni zina fursa ya wastani na zilizobaki hekta 22.3 milioni zina fursa ndogo. Katika mpango huu, kila Wilaya imeshahimizwa kuandaa mipango yake ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na kipaumbele kimewekwa katika kufufua na kuboresha miundo mbinu, skimu za asili za umwagiliaji za wakulima wadogo na miradi mipya ya gharama ndogo ambayo wakulima watachangia nguvu na gharama ya uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, ni wazi kabisa kwamba sasa hivi Serikali inajikita katika eneo la kuona kwamba mafaniko haya tunayopata kwenye uchumi jumla yanawafikiaje wananchi. Lakini ni lazima Waheshimiwa Wabunge tukumbuke kwamba taratibu zote hizi huu ni mchakato hatuwezi kusema inaweza kuchukua mwezi mmoja lakini huko nyuma tulikotoka na tunakoelekea sasa hivi, nina hakika kwamba hili tutaliendeleza vizuri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tunaliwekea mkazo bado tunafikiria suala la kukubali kwamba sasa sekta binafsi ndio itakuwa mhimili wa uchumi wetu. Hili tumeshakubaliana na Serikali imeshachukua hatua mbalimbali. Serikali imeanzisha *Tanzania National Business Council*, Serikali imeanzisha *Tanzania Private Sector Development Foundation*, Serikali imekuwa ikifanya vikao mbalimbali na sekta binafsi ili kuiruhusu kutoa mchango wake katika uwezeshaji wa kuwekeza vema katika nchi yetu.

Kwa hiyo, la msingi ni kwamba wananchi, sekta binafsi na Serikali kila mwenye uwezo wa kufanya kazi ni vizuri tukafanya kazi kwa sababu tumeshaelewa hakuna njiapanda lazima tufanye kazi ili tuweze kukuza uchumi wetu. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaahidi kuendelea na zoezi hili la kuboresha uchumi na itazingatia sana ushauri kama tulivyofanya safari hii unaotoka katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali kupitia mpango na Bajeti hii, tumesema kwamba ni kupunguza umaskini. Kama nilivyosema, tunapozungumzia umaskini kama alivyosema Mheshimiwa Anne Makinda, inabidi tuangalie umaskini wa kipato. Tunapozungumzia huduma za jamii tunazungumzia taratibu za kupunguza umaskini usio na kipato. Mara nyingi nimekuwa nikisema tunapotafsiri nini maana ya umaskini, umaskini sio kukosa fedha tu mfukoni nimesema pale ambapo wananchi hawapati huduma nzuri za afya pana umaskini, pale ambapo hawapati maji vizuri ni umaskini, lakini vile vile suala la ajira na *income generation* ni masuala ambayo yatasaidia sana katika kupunguza umaskini usio wa kipato.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kama alivyosema Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Hamisi Nguli na Mheshimiwa Athumani Janguo, kinachobakia sasa ni nidhamu na uwajibikaji katika utendaji wetu katika shughuli zetu ili tuweze kuinua uchumi wetu kwa kiwango kikubwa. Wako Waheshimiwa Wabunge waliokuwa na wasiwasi kwamba katika hizi *projection* zetu za kukua kwa kasi ya uchumi tutawezaje kufikia dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Dira ile ya maendeleo kwa kweli inatuwekea kiwango cha 8% lakini nina hakika kwa hatua ambazo tumechukua sasa hivi na sote tukienda kufanya kazi kwa bidii viwango vyetu vya uchumi vitakuwa kwa kiwango kikubwa tu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la uchumi jumla ambalo lilikuwa limeulizwa na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Hamisi Nguli na Mheshimiwa Aridi Uledi, kwamba kama

tunazungumzia uchumi unakua inakuwaje tunasema thamani yetu ya fedha inashuka? Hili ni swali ambalo limeulizwa hapa ndani. Niseme kwamba tunazungumzia mambo mawili tofauti.

Tunapozungumzia kukua kwa Pato la Taifa *(Gross Domestic Product)* tunazungumzia viwango vya uzalishaji wetu humu ndani na tunapozungumzia kupungua kwa thamani ya fedha tunalinganisha fedha yetu mahusiano yake na fedha nyingine au sarafu nyingine. Sasa tunaelewa kwamba sarafu yetu tumeiweka sana kwenye Dola. Vimetokea vita vya Iraq vimeleta matatizo, sasa hivi nchi za Ulaya *(European Union)* zimeungana *Euro* yao ikawa na nguvu zaidi kuliko Dola sasa hilo lazima liwe na athari fulani katika thamani yetu ya shilingi. Lakini kama nilivyosema ufumbuzi wa tatizo hili kwa kweli ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa za kuuza nje, tukazane na suala zima la kuongeza thamani ya bidhaa zetu kwa *agro-processing* ili tuweze kujiweka katika hali nzuri. Misaada ambayo tumepata, lazima tuseme wazi, kama ya *HIPC* na ile *ODA* imesaidia sana kuiweka shilingi katika hali nzuri ama sivyo ingeshuka sana. Sasa mtu ataweza kusema kwamba tunapata fedha za kigeni ambazo sio zetu hapana ni zetu kwa sababu mwanzoni tulikuwa hatupati kabisa fedha hizi. Sasa hivi fedha hizi tunazipata kwa sababu ya utaratibu mzuri wa urekebishaji wa uchumi wetu katika nyanja za uchumi, kifedha na katika nyanja za kufanya kazi kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuzungumzia suala moja ambalo limezungumziwa hapa na hili ni suala la baadhi ya miradi ambayo hatukuitaja kwenye Bajeti. Naelewa wazi kwamba mradi wa *Mtwara Corrido*r hatukuutaja, lakini kazi inaendelea. Sasa hivi utafiti wa kupeleka umeme kutoka Mufindi mpaka kule Mchuchuma umeanza kufanyiwa kazi, tumeambiwa hapa na Waziri wa Ujenzi kwamba hata ile barabara upembuzi yakinifu uko katika *process* ya kuanza. Kwa hiyo, sio kwamba tumenyamaza tu ni kwamba kuna kazi inafanyika.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tunalifanyia kazi ni suala la ubinafsishaji. Nimefurahi sana nitakuwa namtajataja sana lakini Mheshimiwa Benson Mpesya, alinifurahisha sana pamoja na Mheshimiwa Venance Mwamoto, walisema kwamba kama tukishaamua kuingilia zoezi la kisera basi twendeni tuingilie zoezi hilo la kisera.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba hakuna mtu au nchi yeyote duniani inayoweza kufanya zoezi lolote lile likawa ni *hundred percent*. Ndio maana tunasema kwenye zoezi la ubinafsishaji kuna mafanikio sisi tunakubali kama Serikali lakini vile vile tunakubali kwamba yapo mapungufu.

Mheshimiwa Spika, lakini mafanikio yapo tunaweza kuyataja, Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati ya Uwekezaji walitembelea baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa. Kiwanda cha Mtibwa kilikuwa kinawalipa wakulima wadogo wadogo wanaopanda miwi shilingi milioni 300 kabla hakijabinafsishwa baada ya kubinafsishwa Kiwanda cha Mtibwa kinawalipa shilingi bilioni 1.3. Hilo ni ongezeko na ni mafanikio.

Kiwanda cha Kagera kilikuwa na wafanyakazi nadhani 120 tu sasa hivi kimeongeza ajira na kiwanda kile hata kabla ya kufanya kazi hakikuweza kuzalisha zaidi ya 10% ya uwezo wake. Sasa iko mifano mingi mingine mnaifahamu Viwanda vya Bia kuongezeka kwa kodi Serikalini, sasa hivi tunasafirisha nje nyaya za umeme, sasa hivi tuna saruji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nije yale yanayowagusa wakulima. Waheshimiwa Wabunge wote watakumbuka na hili bado nalirudia na nalizungumza mara kwa mara, ilifika wakati hata chumvi tunapinga foleni, tulifika wakati hata sukari likuwa lazima tuweke foleni, ilifika wakati tunatafuta nguo za kuvaa lakini urekebishaji ulipoanza kufanyika pamoja na ubinafsishaji bidhaa hizi sasa zimeanza kupatikana.

Sasa wakati tunapozungumzia suala la ubinafsishaji ni kweli lina mafanikio lakini vile vile mapungufu yapo. Kama nilivyosema mwanzoni haitawezekana hata kidogo, nakumbuka wakati ule wa zamani watu wengine waliingizwa kwenye uhujumu kwa sababu ya kukutwa na galoni moja ya mafuta kwa sababu kulikuwa hakuna bidhaa wengine waliwe kwa uhujumu kwa kukutwa na maboksi ya *Colgate* kwa sababu ya huduma ya bidhaa katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Eliachim Simpasa, alipokuwa anazungumza hapa alisema sasa hivi tunalalamika kuhusu suala la ubinafsishaji lakini lazima tuangalie suala la ubinafsishaji lilianzaje. Tulikuwa na mashirika zaidi ya 400 yakafikia *capacity utilization* ya chini ya 25% na ndio tukajikuta tunapiga hizo foleni hizo ndio tukawa tunazungumzia masuala mengi ya ulanguzi.

Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi alisema hapa kwamba hili suala la ulanguzi kulizungumzia lazima tuli-*categorize* kwa sababu kuna watu wanawasaidia wakulima sisi tunawaita walanguzi lakini hii *concept* ya ulanguzi tuliipata wakati ule, ulanguzi, magendo, kwa sababu ya uhaba. Lakini nafikiri yote haya sasa kabla ya zoezi la ubinafsishaji lenyewe kuanza karibu viwanda 70-80 vilifungwa kabisa.

Tulikuwa tunazungumzia *KILITEX* na *SUNGURATEX*, ni magofu. Sasa hivi sekta ya nguo kile kiwanda cha *NIDA* tu kitaajiri watu zaidi ya elfu tatu na *production* imepanda. Kwa hiyo, nasema kwamba, zoezi la ubinafsishaji mimi sisemi kwamba *hundred percent* ni zoezi timilifu, yapo mapungufu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge waliotembelea viwanda hivi kwani walitupa ushauri kwamba, ni lazima tuangalie tutawawezesha vipi wale wawekezaji hasa Watanzania katika kuondokana na matatizo ambayo wanayapata ya kuanzisha viwanda hivyo. Serikali italiangalia hilo. Haja yetu hatutaki kuona viwanda vilivyolala kwa sababu *opportunity cost* ya kulaza viwanda hivi na wakati tuna shida kubwa ya kuongeza uchumi wetu inatubidi tuchukue taratibu za kuvifanya viwanda hivi vifanye kazi. Kuna viwanda vingine vilikuwa na teknolojia ya mwaka 1960. Nilitembelea Kiwanda cha *Ubungo Spinning Mill*, niliambiwa kwamba, mashine zilizokuwepo pale zilikuwa zinatoa mita nne za kitambaa kwa saa moja. Teknolojia ya sasa mashine hizo zinatoa mita kumi na tano kwa saa moja. Sasa inawezekana kabisa tukawa tunazungumzia tu suala la kufanya kazi, tukasahau suala la teknolojia, *management* na ujuzi. Ndiyo maana tukasema kwamba, ipo haja ya kusaidia taratibu za kuwa na *bankable proposals* lakini vile vile ni jinsi gani wawekezaji hawa watafikia huduma za mikopo.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba tunazungumza sana kuhusu kutoridhika katika ubinafsishaji kwa maana ya kuzungumzia watu kutopata mafao yao, lakini sote tunaelewa kwamba Serikali katika kila kiwanda ilichobinafsisha imekwishalipa mapato na mafao ya kisheria. Mara nyingi mafao haya ya Pensheni na *PPF* ni matatizo yale yale ya nyuma kwamba wakati ule *management* za viwanda hivi ilikuwa inakata fedha za wafanyakazi wale ili wazifikishe kwenye vyombo vya pensheni, lakini fedha hizo zilikuwa haziendi. Sasa Serikali inachukua jukumu, lakini hayo ni mambo ambayo inabidi kama Serikali au Wabunge, tuyapime kwamba bado yanatokana na *inefficiency* iliyojitokeza wakati ule tulipokuwa na mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Mwaga, aliuliza swali moja zuri sana na alisema kwamba, sasa jamani hizi *data* zilizotolewa kwenye kitabu cha bajeti inawezekana kabisa zikawa ni za kiini macho. Kwamba labda vile viwanda vilivyouzwa kwa Watanzania thamani yake ni nini? Mimi nadhani hilo lilikuwa ni swali zuri.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni, 2003 thamani ya mashirika yaliyouzwa kwa bei ya mauzo kwa wageni, asilimia mia moja yalikuwa na thamani ya shilingi bilioni ishirini na tisa nukta nane. Mashirika yaliyouzwa kwa Watanzania asilimia mia moja yalikuwa ni shilingi bilioni sitini na tatu nukta tano. Sasa na mashirika yaliyouzwa kwa ubia kwa maana ubia wa Serikali na wawekezaji wa nje yalikuwa ni shilingi bilioni mia nne na saba. Lakini vile vile katika baadhi ya mashirika haya ambayo yamewekezwa na wawekezaji kutoka nje yameshafungua utaratibu mzuri tu wa hisa, tunayo *Dar es Salaam Stock Exchange*, wananchi sasa wananunua hisa, wapo wananchi Watanzania sasa hivi zaidi ya elfu sitini wamenunua hisa katika Kampuni za Sementi, Bia na Sigara. Kwa hiyo, ni vigumu sana kusema kwamba, yale mashirika waliyopata Watanzania labda ni yale mashirika uchwara tu. Nadhani tuzungumzie tatizo lililopo pale ambapo ni tatizo la kuona ni jinsi gani watasaidiwa hawa wawekezaji Watanzania ili kupambana na matatizo wanayoyakuta katika kuendesha viwanda hivi.

Mheshimiwa Spika, tunayo orodha ya mashirika yaliyobinafsishwa kwa Watanzania, tumeuza mashirika kwa wafanyakazi chini ya utaratibu wa *MEBO* na tumesaidia katika kuwezesha Watanzania kupata mashirika haya, kwa mfano, KAURU na *Mbeya RETCO*, kodi zimepunguzwa ili kuwauzia wale wahusika. Kuna ushirikishwaji mzuri unafanyika. Katika kipindi hiki cha bajeti tulipata takwimu kutoka

kwa Mheshimiwa Shellukindo za Kiwanda cha Chai cha Luponde, ambacho *investment business plan* yao ilikuwa ni 1.5 *billion shillings.* Sasa hivi wamefika 1.59 *billion shillings.* Sasa tunayo mifano mingi tu na *in fact* wale walionunua hisa ni wananchi karibu themanini elfu.

Mheshimiwa Spika, lingine lililozungumzwa kwa ujumla wake na Waheshimiwa Wabunge wengi tu ni kwamba, sasa umefika wakati wa *PSRC* kufanyiwa tathmini. Hili limezungumzwa na Wabunge wengi tu. Mimi kama Waziri mwenye dhamana ya Mipango na Ubinafsishaji, sina tatizo na hilo. Nakubali kwamba *PSRC* ifanyiwe tathmini kwa sababu haiwezekani kitu kifanye kazi kwa muda halafu kisifanyiwe tathmini, basi tathmini hiyo ifanyike. Ila tu ninachotaka kusisitiza, tunachotaka kukifuata ni utaratibu wa kisheria uliopitishwa na Bunge lako hili Tukufu lililozaa *Public Corporation Act, 1992*, ambayo ilirekebishwa mwaka 1993 na 1999. Naomba katika Sheria hii tuangalie kifungu cha 21(3) cha Sheria hiyo. Kwa hiyo, mimi nasema kwa kweli sina tatizo lolote la kukataa *PSRC* isifanyiwe tathmini.

Mheshimiwa Spika, katika ufuatiliaji wa baadhi ya mashirika, napenda kutoa ahadi kwamba, Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, tutafanya kazi karibu sana na sekta husika ili kuhakikisha kwamba, yale mashirika au makampuni ambayo sekta husika inabidi iyasimamie yaliyokwishabinafsishwa, tunafanya kazi kwa pamoja ili kuondoa baadhi ya matatizo yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, *sector dominant* ni sekta za kilimo, utalii, viwanda na biashara. Sasa hivi Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa sababu Serikali imeshasema kwamba mashamba yote ya mifugo kama alivyozungumza hapa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, ubinafsishaji wake utasimamiwa na Wizara ya Maji na Mifugo kwa *ranches* zile. Pia katika sekta ya madini tutahakikisha kwamba, tunafanya kazi kwa karibu sana ili kupunguza haya matatizo ambayo Waheshimiwa Wabunge mmetupa na ya kuboresha utendaji katika zoezi la ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia kwa ujumla ni suala la uwekezaji ambalo limezungumziwa katika kikao chetu hiki kwa ujumla wake. Mimi nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba, Tanzania hatuwezi tukaishi *in isolation*, tukawa ni nchi tu hatukaribishi *foreign direct investment* tukasema tutawekeza wenyewe, tumeshaweka mazingira mazuri kupitia *Tanzania Investment Centre*. Saa nyingine nakaa najiuliza Mheshimiwa Mbunge mmoja alitoa mfano wa Uarabuni na mafuta, sijui alikuwa nani, samahani jina nimelisahau. Lakini nilitaka kumwuliza Makampuni yale yanayoendesha mafuta kule Uarabuni ni mangapi ya Kiarabu? Nilitaka kumwuliza hilo. Sasa sijui *TEACO* ni la Uarabuni, *BP Shell* la wapi, *CALTEX* ni la wapi na kadhalika na kadhalika. Sasa hiyo inatueleza kwamba, kwa kweli hatuwezi kuishi *in isolation. (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilipata bahati ya kwenda Angola ambako wanazalisha mafuta mengi sana, kampuni zote ni hizi hizi. Kwa hiyo, nilikuwa nasema hatuwezi kuishi *in isolation*. Sasa hivi tuna uwekezaji katika sekta ya madini, nilipokuwa Waziri wa Nishati na Madini nilipata bahati ya kusafiri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, niliwachukua Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa tukaenda Ghana na Australia, kuangalia migodi. Kule tulikwenda kuangalia migodi iliyokuwa na umri wa miaka mia, tulikwenda Ubuwasi na wapi. Kule Australia tulikwenda Mji mmoja wa Calbul nafikiri kitu kama hicho, ile migodi ni ya miaka mia. Sisi migodi yetu ni miaka minne sasa baada ya kufanyiwa kazi kubwa sana na *STAMICO* na *STAMICO* sijui ilifikia wapi. Kwa hiyo, ninachojaribu kukisema ni kwamba, tutajaribu kuboresha mazingira yetu ya uwekezaji, tutajaribu kuhakikisha kwamba, uwekezaji unaongeza Pato letu la Taifa, unaimarisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na kuzungumzia masuala ya uwekezaji, napenda kuyapongeza sana baadhi ya haya makampuni ya madini ambayo yapo. Nayapongeza sana kwa sababu kuna maeneo mengine wamejenga barabara, hospitali, nyumba na kwa kweli wala siyo kwa masharti. Wale ni wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kulizungumzia ni suala la Ukimwi. Wote tumelizungumza kwamba, sasa hivi ni janga kubwa na lile linaathiri sana uchumi kwa ujumla. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tutakapokwenda katika maeneo yetu tuendelee kulipigia kelele zaidi suala la Ukimwi, kwa sababu suala la Ukimwi linavunja nguvu kazi. Sasa na mipango mizuri hii na bajeti nzuri ya kuwawezesha wakulima wetu Vijijini ni bora sasa tukawa na moja la wakulima wetu Vijijini kufanya kazi

kwa bidii ili kukuza Pato letu la Taifa ambalo limeshaanza kukua vizuri na ambalo vile vile linaandamana na ukuaji mzuri wa kisekta katika sekta zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tutajitahidi vile vile kuboresha mipango ili mipango yetu iweze kukidhi haja lakini nadhani mare kebisho tunayotakiwa kuyafanya ni marekebisho ambayo si makubwa sana. Tukiangalia ukuaji wa Pato la Taifa kwa asilimia sita nukta mbili kwa Tanzania ukilinganisha na ukuaji wa wastani wa Pato la Taifa kwa Afrika na tukiangalia nchi zinazotuzunguka majirani zetu, nadhani Tanzania tumefanya vizuri, isipokuwa tunahitaji tu kuongeza jitihada, huo ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzoni, hotuba yangu ya mipango iligusia sana maeneo ya uchumi jumla. Nimesema maeneo yale ya kisekta yatajibiwa na sekta husika. Lakini kabla sijamaliza napenda kurudia tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia na kuboresha hotuba yetu na mipango yetu. Napenda kuwahakikishieni kwamba, baada ya kuchukua ushauri ambao tumeupata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na baada ya kukubaliana kwa mihadi nini tukafanye katika Majimbo yetu, nina hakika Mwenyezi Mungu akijalia, katika bajeti ijayo tutaanza kuona viwango vikubwa vya ukuaji wa uchumi na vile vile viwango vikubwa vya kukua katika sekta zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa kadri utaratibu wetu wa Kanuni ulivyo, hoja zinaweza kujadiliwa pamoja, lakini ni lazima kila hoja itaamuliwa peke yake. Kwa hiyo, jioni tutaamua hoja ya kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali. Lakini hoja ya Waziri aliyewasilisha taarifa ya hali ya uchumi kama inavyoonekana kwenye *Order Paper,* ilikuwa ni kwamba, Bunge lijadili na hatimaye likubali kuridhia Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2002 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2003/2004. Sasa nitawahoji tuone kama Bunge linakubali kuridhia taarifa iliyowasilishwa Bungeni.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2002 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2003/2004 ilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Kama nilivyoeleza jana kuhusu ratiba ya leo, sasa nitasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni ili tumsikilize Mheshimiwa Waziri wa Fedha, akihitimisha hoja yake ikifuatiwa na upigaji kura wa kuita jina moja baada ya jingine. Ni matakwa ya Katiba na matakwa mengine ya Katiba kwa maamuzi yote ni kwamba, lazima tuwe na kiwango cha *quorum.* Ibara ya 94(1) inasema kiwango cha Kikao cha Bunge ni nusu ya Wabunge wote. Kwa hiyo, tujitahidi mahudhurio yetu kama yalivyo sasa yaendelee kuwa hivyo hivyo wakati wa mchana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha nimeshatangaza kikao cha Wabunge wote wa Chama Tawala. Sasa nimeombwa nitangaze kikao cha Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani na wao wakutane mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge, wenyewe wanajua watakapokutana. Lakini Wabunge wa CCM watakutana humu ndani. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 5.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)
(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili na hasa mjadala huu wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2003/2004, kwa uwezo mkubwa na kwa nidhamu ya hali ya juu. *(Makofi)*

Ningependa vilevile kutambua mchango wa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Akukweti na Wenyeviti wanaosaidiana na wewe, Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Eliachim Simpasa, kwenu nyote nawashukuru sana. *(Makofi)*

Ningependa vilevile kutambua mchango wa Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii. Kwanza kabisa, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine waliochangia kwa kuzungumza ni Waheshimiwa Wabunge wafuatao: Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Diodorus Kamala, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Edson Mbeyale Halinga, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Ramadhani Khalfan, Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Isaac Cheyo.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mheshimiwa Abdula Lutavi, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Thadeus Luoga, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Jumanne Hamisi Nguli, Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Mheshimiwa Monica Mbega.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mheshimiwa Frank Magoba na Mheshimiwa Zahor Juma Khamis. Kwa wote hawa ambao nimewataja tu kwa kuokoa muda nikaacha kutaja vyeo vyao vingine vya ziada, nawashukuru sana kwa michango yenu mizuri na nitaizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Jacob Shibiliti na Mheshimiwa Prof.Mark Mwandosya.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Dr. Maua

Daftari, Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Ali Sheha Mussa, Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali na Mheshimiwa Semindu Pawa. Kwa wote hao na pengine wengine ambao kwa bahati mbaya labda nimewasahau, nawashukuru sana na nitazingatia michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa mchango wao mkubwa wakati tulipokutana kabla ya Bunge rasmi kuanza kule Dar es Salaam na hata baada ya Bunge rasmi kuanza, michango yao nimeithamini na nimeizingatia katika bajeti hii, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea niseme kwamba, nimesikiliza kwa makini sana mawazo na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na kwa sababu toka mwanzo nilikuwa nikisema kwamba, Bajeti hii inatokana na mchango wa kila aina ya watu, pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Napenda kuthibitisha tena usikivu wangu huo na usikivu wa Serikali yenu ya Chama cha Mapinduzi kwa Waheshimiwa Wabunge wenzake na uthibitisho wa usikivu huo mnisikilize kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imesikiliza kwa makini na kutafakari hoja za Waheshimiwa Wabunge, ambazo zimegusia maeneo mengi sana. Serikali imejitahidi kutoa maelezo kuhusu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na maelezo hayo kwa kuzingatia uzito wa hoja zilizotolewa katika baadhi ya maeneo, Serikali imeamua kufanya marekebisho yafuatayo:-

Kwanza, Ushuru wa Forodha kwa dawa za mbu za kuchoma kutoka nje. Serikali ilipendekeza kuongeza Ushuru wa Forodha kwa dawa za mbu za kuchoma zilizoagizwa kutoka nje kutoka asilimia 10 ya sasa hadi asilimia 15, kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani ambavyo vinatumia Pareto ya Tanzania kutengeneza dawa za mbu za kuchoma. Kwa kuzingatia mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge, ushuru huo sasa utabaki katika kiwango cha sasa cha asilimia 10, *no change. (Makofi)*

Pili, nyenzo za kutengeneza vyandarua imebainika kwamba, nyenzo muhimu zinazotumika kutengeneza vyandarua ni nyuzi ambazo zinatumiwa pia na viwanda vingine vya nguo, siyo rahisi kutofautisha nyuzi zinazotumiwa na viwanda vya kutengeneza vyandarua na zile zinazotumiwa kutengeneza bidhaa nyingine za nguo. Ili kusaidia viwanda vinavyotengeneza vyandarua humu nchini, viwanda hivyo vitatakiwa kuwasilisha Hazina mahitaji yao na mchanganuo wa nyenzo za msingi wanazohitaji kama malighafi ili zipewe unafuu wa kodi kwa kutumia Tangazo la Serikali, yaani *Government Notice (GN).* Aidha, nieleze kwamba, dawa ya ngao ya kuweka kwenye vyandarua haitozwi kodi yoyote. Hatua hii ina maana ya kupunguza sana ushuru kwenye vyandarua vya mbu. *(Makofi)*

Tatu, kodi kwenye madawa ya binadamu. Hivi sasa madawa ya Kifua Kikuu, Malaria, UKIMWI hayana kodi yoyote. Dawa nyingine zote zinazotoka nje zinalipa Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 na zimesamehewa *VAT*. Ushuru huo wa asilimia 10 umewekwa ili angalau kusaidia viwanda vya ndani visife, kutokana na ushindani kutoka dawa za nje. Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa kupatikana kwa dawa za kuokoa maisha ya watu kwa wingi na kwa bei nafuu, orodha ya dawa zitakazosamehewa kodi itaongezwa ili kusiwe tena na visingizio vya ukosefu wa dawa katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati za Serikali. Dawa tunazozizungumzia hasa ni zile *Essential Drugs*, ambazo zinasambazwa hadi vijijini kwenye Zahanati na kadhalika. *(Makofi)*

Nne, ushuru wa bidhaa *(Excise Tax)* kwenye matumizi ya simu za mkononi unabaki asilimia 5 kama ilivyokuwa tangu Julai, 2002. *(Makofi)*

Tano, ushuru wa ngozi ghafi, Serikali ilianzisha Mfuko tuliouita *Livestock Development Fund* katika bajeti hii ili Mfuko huo uweze kuwa na manufaa katika kipindi cha muda mfupi. Serikali sasa imeona ni vyema kuongeza ushuru kutoka asilimia 15, niliyokuwa nimependekeza hadi asilimia 20 kwa ngozi hizo. Lengo ni kuzuia ngozi hizi zisisafirishwe ovyo nje ili zitumike kwenye viwanda vyetu vya ndani kuzalisha ngozi ambayo imekwishasindikwa. *(Makofi)*

Sita, udhibiti wa ukwepaji wa kodi ya mafuta ya petroli. Baada ya kutafakari hoja za Waheshimiwa Wabunge na mawasilisho mapya kutoka kwenye kampuni za mafuta, Serikali imeona ni bora muda ule wa kulipa uliokuwa uwe ni siku 15 sasa usogezwe uwe ni siku 30, toka tarehe ya kuingiza mafuta hadi atakapolipa ni siku 30 badala ya siku 15. *(Makofi)*

Saba, msamaha wa *VAT* kwa *sub-contractors* wa uchimbaji wa madini. Kwa kuzingatia hoja za Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Sekta ya Madini, hatua iliyokuwa imependekezwa sasa inasitishwa, hawa *sub-contractors* wataendelea kulipa *VAT* kama kawaida. Kwa hiyo, uamuzi huu wa Serikali utazingatiwa katika *Finance Bill* ambayo imewasilishwa pamoja kama sehemu ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze sasa kwa bahati mbaya muda ni mfupi na sitapata muda, lakini nitajitahidi kujibu kwa mafungu badala ya hoja moja moja kwa sababu ya kuzingatia muda. Hoja ya kwanza, ilikuwa ile tofauti baina ya Mikoa katika kutoa mgao wa fedha kwenye miradi mbalimbali na kwenye shughuli za maendeleo. Ninachoweza kusema tu ni kwamba, mwaka huu nilijitahidi kufanya mambo ambayo nilifikiri yangesaidia. Lakini ukweli inavyoonekana mambo yangu hayakusaidia sana. Kwa hiyo, lalamiko limebaki pale pale. Sasa nitakachofanya mwaka huu wa fedha nitapeleka washauri kwenye Mikoa hiyo ili waweze kutupa *formula* ya namna ya kugawa fedha za maendeleo kwenye Mikoa yote ya Tanzania, kwa uwiano unaofanana bila kuathiri maendeleo ambayo yapo tayari. Kama kwenye Mkoa fulani kuna shule 10 na Mkoa mwingine kuna shule 3, hatuwezi kufunga zile shule 10 kusubiri wenye shule 3, tutaendelea lakini lazima uwepo uwiano wa dhahiri kati ya fedha zinazotumika kwa miradi iliyoko na kwa miradi mipya ili kuleta uwiano unaoridhisha zaidi kuliko ulioko sasa. Sasa hii kazi nitaifanya mwaka huu wa fedha na ingawa sikuwa nimeipangia, lakini nitatafuta fedha. *(Makofi)*

La pili, udhibiti wa bajeti, nakubaliana kabisa na hoja kwamba, ni lazima tudhibiti bajeti ya maendeleo na ya matumizi ya kawaida. Ndiyo maana tumenunua kwa gharama kubwa ule mtandao wa kompyuta tunaouita *IFINZI* kwa kifupi, ambao ndiyo umemletea sifa Mama Blandina Nyoni hapa, ndiyo wenyewe huo. Waheshimiwa Wabunge, nirudie lile ambalo nilikuwa nimewaeleza Kamati ya Fedha na Uchumi. Tanzania sasa imekuwa ni kisiwa katika nchi hizi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Tanzania ni kisiwa, watu wanakuja hapa kujifunza jinsi ya kuendesha mtandao ule wa Mhasibu Mkuu wa Serikali uliofanywa Dar es Salaam. Wanakuja Mawaziri na wataalam kutoka Afrika ya Magharibi, Afrika ya Kusini, Afrika ya Kati. Mimi mwenyewe mwaka 2002, nikifuatana na Katibu wangu Mkuu, Ndugu Ngumbullu, wakati ule, tulikwenda London kuhutubia Jumuiya ya Madola yote juu ya jambo hili. Hivi sasa tunavyozungumza, kila siku tunaalikwa kwenye mikutano mingi ya wafadhili kueleza jinsi tunavyofanya sisi hapa Tanzania. Lakini kama nilivyosema hapa, sisi Tanzania hatujakamilisha sasa tunasogea Mikoani na Wilayani. Kwa hiyo, huku tunafanya na huku tunafundisha sisi siyo wachoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Cash Budget* kuna waliokuwa wanalalamika sasa hii *Cash Budget* inarudisha maendeleo nyuma. *Cash Budget* inaongeza nidhamu kwa sababu kama wewe unajua una shilingi 10/= tu mfukoni mwako, huwezi kufanya kazi ya shilingi 20/= utafanya kazi ya shilingi 10/= na hii ndiyo imetufikisha hapa tulipo kwamba, tunatumia kile tu tunachokusanya. Ndiyo maana ni muhimu sana kuliangazia macho Shirika la *TRA*, kwa sababu wakiteremka kidogo tu katika ukusanyaji, basi tumekwisha na ndiyo maana nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, waliokuwa wanalisifu Shirika hilo na hasa kiongozi wake Mkuu ambaye sasa amehamishwa, Ndugu Sanare, kwa kazi nzuri aliyoifanya kwenye Shirika hili. Mimi nimekwishawaapisha hawa wapya, nimewaapisha kienyeji maana sina madaraka ya kuwaapisha hawa. Nimekwishawaambia mimi ninao mwaka huu lazima waongeze hiyo bilioni 100 ielekee kwenye bilioni 200. Makusanyo angalau wafike bilioni 150 kama Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa alivyosema na wale wamesema tunakubali na tutafanya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna waliokuwa wanazungumzia habari za ruzuku ya pembejeo. Mimi ni mtu wa siku nyingi kidogo msinione hivi, ni mtu wa siku nyingi kidogo. Hii nchi naifahamu sana na kuna Mkoa mmoja naufahamu sana, unaitwa Mbeya, nimekaa kule nikaogelea nikitazama mbele sioni, nikitazama nyuma sioni, nikazinduka tu lakini nikafanya utundu nikafanikisha mambo. Katika kilimo katika Mkoa ule jambo moja muhimu nililojifunza ni mbolea na ndilo naweza nikaandika hata *Ph.D.* leo.

Mbolea ndiyo jambo la kwanza kabisa kwenye Mikoa ya Kusini Magharibi kwa sababu udongo wao bila mbolea hauzalishi kitu, ndiyo ukweli. *(Kicheko)*

La pili, *inputs, Agro- Chemicals* na la tatu ni vitu kama umwagiliaji. Kwa hiyo, mimi najua kabisa kwamba, ni vitu gani ambavyo leo unaweza ukafanya na wakati wa kuvuna ukapata mavuno mengi. Ni vitu gani? Hakikisha umeweka mbolea, hakikisha umenyunyizia madawa, hakikisha una soko, hakikisha Vyama vya Ushirika vinafanya kazi na wanunuzi wengine na vitu chungu nzima ambavyo Mheshimiwa Charles Keenja, atafafanua. Kwa uzoefu wangu wa miaka 5 kama Mkuu wa Mkoa, nilifanya vitu hivyo nikaliona hili, nimefanya na kuona matokeo. Nimeona nianze pale ambapo nilikuwa kwa sababu napafahamu pale siwezi kufanya kosa.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Mbeya na mimi ni mwana-Mbeya pia, naomba msiniangushe bwana. Tutakwenda taratibu, mpango huu siyo wa bajeti hii, tutaendelea nao na tutaendelea kusikiliza na wengine. Nasikia Morogoro wanataka vitu fulani kwa ajili ya mpunga sawa, wengine wanataka vitu fulani kwa ajili ya zao lingine sawa, lakini lazima tuanze mahali. Kisha nikasema hii tabu, sasa hivi nimesikia kuna kesi ya mchele kule Bandarini, ni upuuzi gani, kule Mbarali kuna mchele, kule Morogoro kuna mchele, Shinyanga, Dodoma, kila mahali. Lakini Serikali nzima mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waheshimiwa Mawaziri wote wale, tunahangaika mpaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunahangaika na mchele wa kupewa, hiki ni kitu gani hasa. Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo maana nikasema zao moja la biashara na zao moja la chakula, la chakula ondoa aibu, hii habari ya kwenda kuhemea chakula lazima tuachane nayo, hakuna kuhemea, tuhemee ndani ya nchi yetu, lakini tusihemee Japan, tusihemee Thailand. Kwa hiyo, ni lipi zao lifuatalo? Ni mpunga, lakini hata sasa hivi kwenye bajeti hii inawezekana, kwa sababu nimesema chagueni huko mniambie mpunga ndiyo zao letu sawa, wengine waseme ni mtama sawa, wengine waseme ni mahindi sawa, wengine ndizi sawa na wengine muhogo sawa, yote sawa. Lakini uamuzi ni wenu kisha mkishirikiana na Mheshimiwa Charles Keenja na watu wake mnasema aah uamuzi ndiyo huu. Moja tunalotaka kufanya a, b, c d, mimi nimeshakubaliana na Waziri wa Kilimo na Chakula, hakuna kupeleka fedha mahali pasipokuwa na uamuzi na mpango wa wananchi wenyewe pale walipo, mimi sitapeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini msiniombe tena nifikishe vijijini, maana nimesikia akisema sasa Bwana Basil Mramba, mbona mambo haya, mimi siwezi kufikisha vijijini, sana sana nimefika Wilayani nimeenda mbali sana, nimetoka Taifani nikaenda Mkoani, nimefika Wilayani fedha naziweka pale, sasa amueni nyie mtumie huko na msimamie maana mimi siwezi kwenda zaidi ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hili wala siyo la utani wala siyo la kudumu na kama nilivyosema wiki iliyopita, wala hakuna cha mfadhili hapa ni uamuzi wetu sisi huku nyumbani hakuna cha mfadhili, wala *IMF* wala hakuna anayetunyima. Ni sisi wenyewe kufanya mambo tunavyotaka. Kwa hiyo, lile la kusema zao moja la biashara na zao moja la chakula haikuwa kwamba ukatafute zao jipya, hapana. Pale pale ulipo kama wewe una kahawa ufanye nini kahawa yako sasa ikuletee pato, kama wewe una mahindi ufanye nini mahindi yakuletee pato, sikusema tafuta zao jipya *no*, aanza hapo ulipo. Kwa sababu ukianza mwanzo wa msimu, mwisho wa msimu una kitu, una fedha na una chakula, ndivyo nilivyosema, lakini uamuzi ni wenu. Hii ya fidia ya pembejeo tuna ushirikiano mkubwa na Wizara ya Kilimo na Chakula, tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula na Viongozi Mkoani na Wilayani kufanikisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja aliniuliza ile fedha ya mwaka 2002 iko wapi? Sasa mimi ninachojua nimeshaitoa, nilikoipeleka najua, nimeipeleka kwenye Wizara ya Ushirika na Masoko, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, *Regional Administration*, barabara za vijijini, Halmashauri za Wilaya na kadhalika mpaka kufidia baadhi ya Vyama vya Msingi vilivyokwenda kukopa fedha benki, kuvidhamini ili viweze kuuza pamba, viweze kuuza kahawa, viweze kuuza mazao mengine, nimefanya yote hayo. Jumla ya shilingi bilioni 94.6 nimezipeleka huko. Mwaka 2002 sikusema ni kilimo tu, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, nilisema ni kilimo na vile vinavyoendana na kilimo, maana kilimo bila soko hujaenda ndiyo Wizara ya Ushirika na Masoko, kilimo bila mtu wa kutawala kule kwa hiyo, kuna mtu wa kutawala kule, kilimo ni pamoja na mifugo, kilimo ni

pamoja na mambo mengine. Kwa hiyo, sikusema zote shilingi bilioni 94.6 zinakwenda kwenye kitu kilimo, kilimo *in the broader sense of* kilimo, kuna maana pana ya kilimo. Nafahamu maana ya kilimo ni kilimo kama tunavyokijua sisi watu wa kawaida na vingine ambavyo vinajulikana kitaalam tutaelewana mbele ya safari. Lakini fedha zimekwishakwenda shilingi bilioni 94.6.

Mheshimiwa Spika, sasa kama ndiyo hivyo na sasa tunazungumza habari za *Development Bank*, wanasema mbona benki tunayo tayari, nasema ndiyo. Lakini benki hiyo siyo hiyo, Benki ya *NMB* itaendelea kuwa *NMB*, benki ile ni ya *Micro-Finace*, vitu vidogo vidogo, kuna kilimo kidogo kidogo, uvuvi mdogo mdogo hii itakuwa huko. Mimi nazungumza habari za Benki kubwa hapa siyo benki ndogo ndogo. Benki ndogo ndogo zitakuwepo na zitaendelea kukopeshwa na benki kubwa tunazihitaji. Ukitaka kilimo kiibuke na tulime kwa wingi na tuondokane na shida zote katika kilimo lazima kuwa na Benki kubwa ya kudhamini kilimo. Kwa tafsiri ndogo sana uwe na kitu kama *East African Development Bank* ya Tanzania, kwa ajili ya miradi ya kilimo, ya viwanda, ya barabara na za aina mbalimbali. Nazungumzia juu ya *Development Bank not Commercial Bank, not Micro-Finance Bank, a Development Bank*. Sasa hiyo ndiyo tunaendelea nayo, tukifika zile tarehe tutaamua juu ya hilo kama ndiyo sawa, kama siyo sawa. Baadaye nitaleta taarifa hapa. Lakini *Micro-Finance Bank* inabaki pale pale, kwa nia ile ile ya kuendeleza ihudumie mtu mdogo inabaki pale pale. Kuna waliokuwa wanasema sasa hii *Micro-Finance Bank* mbona haina Bodi, ina Bodi bwana, imeshateua Bodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu misahama ya madeni, hii misamaha ya madeni niliishaeleza sana. Lakini katika makubaliano ya *Paris Club* tuliambiwa nyie Tanzania mnataka sisi wakubwa tuwasamehe madeni, je, kwa nini na nyie msisamehe wadogo wenzenu na sisi tulikuwa tunamdai Uganda, toka vita vya Amini tulikuwa tunamdai, tukasema basi Uganda tunamsamehe ndiyo mdogo mwenzetu, hatukuwa tumemkopesha mtu mwingine sisi. Lakini kuna wanaotudai wadogo pia Zimbabwe na Libya.

MBUNGE FULANI: Angola.

WAZIRI WA FEDHA: Angola, wanatudai na wale tunazungumza nao, tulikopeshwa mafuta huko na vitu vya namna ile. Zimbabwe tulikopa bidhaa za kujengea mji huu wa Dodoma, wakati ule tulikuwa hatuna vifaa vya ujenzi tulikopa huko. Kwa hiyo, hawa ndiyo tunaendelea kuzungumza nao. Lakini jambo kubwa katika madeni wala siyo hilo. Jambo kubwa kwenye madeni je, utaweza kuendelea kulipa hayo madeni yaliyobaki? Hii ndiyo hoja, kwa sababu itafika siku tutatumia fedha zetu zote kulipa madeni, tutakosa tena fedha za elimu na za mambo mengine mazuri kama yale niliyoyataja kwenye bajeti hii.

Hiyo *debt sustainability*, suala hili linazungumzwa sasa kwenye vikao vya Kimataifa, mwezi uliopita wamezungumza ndiyo lilikuwa suala mojawapo kule Abdijan na hivi kesho kule Ugiriki nasikia wakubwa watakutana, mambo kama hayo leo hii ndiyo yanazungumzwa. Wale wakubwa wanazungumza mambo kama hayo tutafanyaje nchi hizi maskini ambazo tumekwishazisamehe madeni zisirudi tena kwenye madeni?

Debt sustainability ni somo kubwa. Kwa hiyo, hayo ndiyo tunaendelea kuzingatia pamoja na kuzungumza na wale ambao wamekataa, baadhi ya nchi za kati zinasema aah, sisi siyo wanachama wa *Paris Club*, kwa nini mnatuingiza kwenye masharti ya *Paris Club*, hao ndiyo tunaendelea kuzungumza nao na huku tunaendelea kubana wakubwa waendelee kuhakikisha kwamba, sisi hatutaingia tena kwenye madeni.

Mheshimiwa Spika na wala msiogope kukopa, suala kubwa siyo kukopa, suala kubwa ni ukope na uweze kulipa, ndiyo kubwa hakuna nchi inayoishi bila kukopa. Marekani ni mkopaji mkubwa, pamoja na utajiri wote Marekani ndiyo mkopaji mkubwa kuliko wakopaji wote duniani, ni wakopaji wakubwa. Lakini wanajua watalipaje baadaye, hata sisi hatuwezi kukaa hapa tunasema ooh, tegemezi tu, unalia unaogopa kutegemea hapana, kopa upate nguvu ili kesho uweze kujitegemea ndiyo namna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la riba tumelizungumza sana hapa, kwenye maswali ya Waheshimiwa Wabunge tumelizungumza sana. Lakini mimi niseme tu kwamba, zipo dalili sasa hivi kwamba riba inaendelea kuteremka kwenye mabenki yetu na inaendelea kuteremka kwa sababu ya ushindani tu wa

biashara ya kibenki. Lakini tulipokutana Mawaziri wa Fedha Arusha, kuzungumzia jambo hili, tumeamua kwamba, Magavana wetu watatu wa Benki zetu Kuu, wawe wanajadili jambo hili la *interest rates* liko kubwa sana Kenya, ni kubwa sana hapa na ni kubwa Uganda, ili tuweze kufanya jambo ambalo linaeleweka eleweka zaidi kuliko ilivyo sasa hivi. Tumekwishaagiza Magavana wetu watakuwa wanakutana na sisi tunaendelea kuweka mazingira bora ili benki zetu zishawishike kukopesha. Kati ya mambo hayo ni pamoja na hayo niliyoleta kwenye Bajeti hii. Mazingira mazuri, Benki ziweze kukopesha.

Kwa mfano, mimi nikisema nitamdhamini fulani akope fedha anunue trekta, kwa sababu huyu hana udhamini, lakini Serikali inamdhamini, wale watamkopesha, tayari ni kishawishi. Yaani hii mifuko ya udhamini ni ya kutia Benki majaribuni na kuzitia hizi Benki majaribuni zikopeshe. Ni njia mojawapo. *(Makofi)*

Kuna mambo mengine mengi kwa mfano, mambo ya kisheria yanayohusiana na ardhi, yanayohusiana na Mahakama kukazia hukumu pale mtu anaposhindwa kulipa na mambo mengine ya namna hiyo ambayo tumaini letu ni kwamba, kabla ya mwaka 2004, Bunge lako likikubali mambo haya, linaweza likawa limeshapitisha sheria ambazo itabidi zibadilishwe ili Benki zetu sasa ziweze kuwaambia kwa dhati, tuweze kuwanyooshea kidole.

Kwa sasa hivi hatuwezi kwa sababu watatuambia hili linatunyima raha, hili kwetu linatuzuia kufanya kazi tukimaliza mambo hayo ikifika mwisho wa mwaka, mwakani na sisi tunaanza kuwanyooshea vidole, mbona mlisema fanyeni basi, mbona mlisema fanyeni basi. Hii ndiyo kazi ambayo iko mikononi mwetu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anaifuatilia kwa makini kabisa na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Waziri wa Viwanda na Biashara na mimi hapa ndio tunaohusika na mambo hayo. Tunakazana usiku na mchana kuhakikisha kwamba, kabla ya mwisho wa mwaka jambo hili linakwisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala hili la *STABEX* ni Mfuko wa siku nyingi sana uliokuwa unatolewa na Jumuiya ya Ulaya kwa ajili ya zao la kahawa. Huko nyuma *STABEX* iliwezekana kwa sababu ilibidi kuwe na orodha ya kila mkulima na kiasi cha mazao alichouza ili kusudi uweze kumlipa fedha kulingana na alivyouza. Hapa kati kati orodha hiyo haiko tena kwa sababu imevurugika baada ya soko huria kuingia kwenye ununuzi wa mazao husika. Kwa hiyo, tumeanza kuzungumza nao. Waziri wa Kilimo na Chakula, mimi hapa tunatumia muda mrefu sana kuzungumza nao. Ningependa kusema kwamba na hili ni mahsusi kwa ndugu yangu Ngawaiya. Yeye ni mtu ambaye anapenda sana hili somo na wengine wanaopenda hili somo. Tena mnisikilize kwa makini niwaeleze la kuwaambia watu wenu. Wapiga kura wenu waambieni hivi, fedha za *STABEX* zipo, lakini hazitumiki kama zamani kugawia mtu mmoja mmoja kwa sababu historia hiyo imeshakwisha.

Kwa hiyo, mwaka huu zitakwenda wapi? Kwanza kuendeleza kilimo Wilayani, *Agricultural Sector Development Plan (ASDP)*, kama atakavyokuja kueleza Mheshimiwa Keenja, kilimo Wilayani. *Euro 18* milioni ukarabati wa barabara muhimu kwenye maeneo ya kuzalisha kahawa, *Euro 10* milioni fedha hizi zitapitia kwenye *Road Fund* na *TANROADS*. Tatu, utafiti wa zao la kahawa, pamoja na huduma za ugani *Euro 9* milioni. Nne, *Euro 1* milioni zitatumika kwa ajili ya ukaguzi, ushauri wa kitaalamu na tathmini nzima ya utekelezaji wa programu nzima ya *STABEX*. Kwa hiyo, jumla ni *Euro 38* au shilingi 42 bilioni.

Naomba sana mnisikilize mnaohusika na zao la kahawa, shilingi 42 bilioni au *Euro 38* ndio fedha zilizopo kwa kipindi hiki mpaka kitakapokwisha sio kwa mwaka huu tu. Mwaka huu tunatumia hizi 18. Mheshimiwa Keenja shilingi 30 bilioni na Mheshimiwa Keenja atakuja kulieleza hili jambo. Mimi fedha ninazo, kwa hiyo, subiri atakuja Waziri wa Kilimo na Chakula, ataeleza sawa sawa matumizi. Lakini ninachojua mimi nimeshasaini mkataba na Jumuiya ya Ulaya, fedha zitamiminika kwa mtiririko walioelewana.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kuanzishwa kwa *Unit Trust*. Niseme tu kwa kifupi kwamba, baada ya mtiririko wa shughuli hii ya kugeuza *Privatisation Trust* kuwa *Unit Trust* kwa Tanzania kwa mujibu wa sheria zilizokuwepo *Unit Trust of Tanzania* sasa imeandikishwa rasmi jana. Lakini nirudie nilichosema siku ile wakati nikizungumzia hoja hapa wiki iliyopita kwamba, haya mambo ya hisa na

biashara ya hisa ni mapya sana kwetu. Mimi nitashangaa kama kuna watu zaidi ya 20 hapa ndani wanaoelewa biashara hiyo. Mimi najua wawili kwa sababu ya historia zao. Hata mimi hapa nilikuwa sifahamu. Ni mjinga nilinunua hisa nikaziweka kama vile nimeziweka kwenye *Bank Account*. Fedha hizi haziwekwi kwenye *Bank Account* zinazunguka. Zinatakiwa zizunguke. Wewe ulinunua hisa za *DAHACO* kwa shilingi 250 zilipopanda zikafikia shilingi 600 ungeuza. Ungeuza mara moja. Sasa zinateremka, kama hukuuza umeshapata hasara. *(Makofi/Kicheko)*

Hii biashara inatakiwa kila siku ujue mtiririko wa soko unakwendaje. Zikiteremka unanunua, zikipanda unauza. Narudia, ujue mtiririko kila siku zikiteremka nunua, zikipanda uza. Inazungumza hivyo kwa kila aina ya bidhaa. Kuna sigara, bia na kadhalika, unaendelea kufanya biashara tu. Unaweza ukahama kwenye soko hili ukaenda kwenye soko lingine. Haya mambo sisi hatufahamu. Kwa hiyo, wale waliokuwa wanalalamika ooh! mbona fedha nyingi zilitumika kutoa elimu na kadhalika, nasema hata hii *Unit Trust of Tanzania* kazi yake ya kwanza itahitaji sana watu wengi kuelimika. Sio kosa letu kwa mfano, ukilinganisha na Kenya, Kenya wamekuwa na soko hili kwa miaka mingi kwa miaka 20 au 30. Sisi hapa ndio tunaanza, tuko mbali. Kwa hiyo, ndugu zangu mimi nawashawishi Waheshimiwa Wabunge, tuendelee tu kujifunza *the hard way*. Tukikuta mtu anayefahamu jambo hili, MaProfesa wawili hapa nawafahamu, Profesa Joseph Mungai anaelewa, Profesa Iddi Simba, Mkurugenzi wa mambo haya mawili na wengine humu ndani wapo.

WABUNGE FULANI: Na wewe je?

WAZIRI WA FEDHA: Mimi siyo Profesa, tena msije kwangu. Lakini njia rahisi kuna wale watu wanaoitwa *Agency* wale *Brokers*, kuna Kampuni za *Brokers* wale unawaendea tu unawapa *instructions* wanakufanyia biashara wewe ukiwa huku Bungeni unamsikiliza Mheshimiwa Mramba na huku wanakutafutia fedha. Kesho wanakupa jibu unawapa tena nyingine unamsikiliza Waziri mwingine huku unaingiza fedha, unaingiza maneno na huku unapiga kura, ndiyo namna ya kufanya biashara hiyo. Huna haja ya kwenda kama mnada wa ng'ombe, hapana. Huu sio mnada wa ng'ombe, ni mnada wa hisa. Kwa hiyo, kujifunza ndio hoja kubwa. Wale wenye televisheni muangalie sana *CNN* kile kipindi cha biashara utaona yale mambo kwenye *CNN*. Wanatangaza zile hisa zinazouzwa hapo kwa hapo *on the window*. Hapo kwa hapo tu unauza na unakwenda zako. Lakini kuna nyingine. Basi muangalie *CNN* kuna elimu kubwa sana ya mambo hayo na televisheni nyingine.

Liko swali liliulizwa hapa na Mheshimiwa Marmo nadhani, huyu Gavana wa Benki mbona hadhibiti hizi Benki. Niseme tu kwa kifupi Benki ni biashara kama biashara nyingine yoyote. Benki ni biashara na biashara zikiendeshwa vibaya huwa zinafilisika. Biashara yoyote hata ya karanga, ukiiendesha vibaya inafilisika. Ukiibiwa inafilisika, ukimweka mtu akuendeshee akakuzunguka unafilisika. Kwa hiyo, hakuna mtu anayeweza kujua Benki yoyote iliyomo nchini leo itakuwa wapi mwaka ujao. Lakini kuna vitu vya msingi ambavyo angalau viwepo, mtaji uwe unatosheleza, utaalam uwe unatosheleza, teknolojia iwe inatosheleza, soko liwe sawa sawa, utaratibu wa kuweka hesabu uwe unaeleweka, haya ndiyo mambo yanayosimamiwa na Benki Kuu. Benki Kuu huwa inaona mapema kabisa hatari inapotaka kuja. Inawaita wale Wakurugenzi inawaambia mimi naona Benki yenu hapa ina tatizo hili na hili na kwa sababu hiyo fanyeni hivi na hivi, wakikubali wanafanya Benki inabadilika, wasipokubali maana mambo haya ni biashara hasa wenye hisa wenyewe wanaweza wakaibiana, hata Wakurugenzi kwa Wakurugenzi wanaweza wakaibiana, kwa hiyo mambo hayo yanaweza kutokea.

Kwa hiyo, unasikia Benki imepata mtingishiko. Sasa ikitokea hivyo, Gavana kazi yake kubwa ni kuikamata mapema ili fedha za wananchi zilizomo kule ndani zisipotee. Kazi ya Gavana ni kuikamata mara moja na kuizuia isifanye biashara. Ndivyo ilivyotokea kwa Mabenki yote yaliyofilisika ndani ya nchi hii toka tuanze biashara huria za Kibenki. Kwa hiyo, msishangae kama mnasoma magazeti ya *East Africa* na kusikiliza redio, mnajua jinsi Benki za nchi moja jirani zinavyofilisika, jina nalihifadhi. Wao wanasema ni ufisadi lakini zaidi ya ufisadi.

Kwa hiyo, Gavana anajitahidi, sheria zipo na juzi juzi mwezi Januari, nadhani tulibadilisha tena sheria kumpa Gavana madaraka zaidi lakini kwa bahati mbaya huwa inatokea hapa na pale lakini tusishangae sana.

Mheshimiwa Spika, niliulizwa hapa kuhusu ununuzi wa ndege na rada, kiasi sikutaka kutoa habari hizi hapa. Lakini nikaona nisipozitoa nitakuwa sijawatendea haki Wabunge wa CCM na wananchi kwa ujumla. Jambo hili la ununuzi wa ndege ya Rais liliamuliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2002, lilishakwisha. Kumbe uamuzi ule umekuwa ni mtaji mkubwa wa kisiasa kwa baadhi ya watu. Watu wanazunguka nchini wakizungumzia habari ya ndege ya Rais, ndege ya Rais. Lakini wote tumeamua hapa. Unajua hizi kazi zetu ni ngumu sana kwa sababu wakati mwingine lazima uwe mkweli, *you have to face the truth* na ukishaamua ni lazima useme niliamua, ilikuwa ni sehemu ya uamuzi. Lakini kama sasa umebadilisha, lete hoja hapa ya kubadilisha. Hapa ndio tunaweza kubadilisha jambo hakuna mtu mwingine. Hata mpiga kura huko asipokuja hapa akabadilisha hakuna kitu kinaweza kikabadilishwa kule. Maana limepita hapa na wananchi wetu wameshaamua kwamba, Rais wao hawezi kutembelea punda. *(Makofi)*

Maana kuna siku Rais wetu alikwenda Afrika ya Magharibi, akapata mkosi huko ndege ikawa haiendi vizuri kule mwanzoni mwa kipindi chake. Akapewa lifti na Rais mmoja wa nchi jirani. Magazeti haya haya yanayopiga kelele leo, ndiyo yalikuwa ya kwanza kusema Rais wetu anaidhalilisha nchi mbona alipewa lifti. Mnakumbuka hili neno. Sasa inafika siku tunamnunulia Rais ndege inakuwa tena ni nongwa, Rais mbona hapandi punda. Sasa tuamue kama unaweza kwenda London kwa punda tuseme hivyo. Mimi ningependa kuwashauri wale Wabunge wenzetu wasichokonoe chokonoe vitu kwenye Majimbo yetu. Sisi hapa tukikaa ni kitu kimoja, ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano, kama unataka kufanya vitu vyako fanya hadharani na kila mtu ajue. Lakini unachokonoa chokonoa unakwenda kule unamsema huyu au yule, halafu ukija hapa unasema mimi ni Mbunge mwenzako, mwenzangu wapi wakati usiku unaniuma na mchana unanitafuna. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndege ya Serikali fedha mlizotenga mwaka 2002 zipo, haijanunuliwa kwa sababu tunachukua uangalifu mkubwa ili tusifanye makosa na tukaja kulaumiwa. Lakini lazima tununue kitu kinachofanana na utaratibu upo, Katibu Mkuu Kiongozi ndiyo Mwenyekiti wa Kamati inayoshughulikia haya mambo na Bajeti ya mwaka huu fedha hizo ziko kwenye Wizara ya Mawasiliano. Nimetenga kiasi cha shilingi bilioni mbili, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi imetengewa kiasi hicho cha fedha. Halafu nikaulizwa na ile rada vipi? Rada imekuja inafanya kazi vizuri kabisa.

WABUNGE FULANI: Tunawaona pote sasa, tunawaona wakiwa njiani?

WAZIRI WA FEDHA: Hili tunalolizungumza hapa yule mtu wa rada anatuona tuko Dodoma. *(Makofi/Kicheko)*

Kama hamuelewi wiki iliyopita kuna ndege iliteremshwa kule Kenya. Kuna ndege ilikuwa angani inapita inaruka kinyemela, iliteremshwa kwa sababu ya rada, lakini ilikuwa inapita kinyemela tu. Kwa hiyo, haya mambo ya teknolojia hizi kwa sababu kwetu ni mapya na siwezi kumlaumu mtu ambaye haelewi, lakini tujitahidi kuyaelewa. Rada iko inafanya kazi Profesa Mwandosya ni shahidi, yeye ndiye aliyeipokea na kufundisha watu na mambo yanakwenda sawa sawa na ndege inakuja. Uamuzi ni wetu sisi wenyewe hapa hapa, sasa tusirukane. Nikisema ukweli watakataa kunipa kura hapa ndani wakati wa kupiga kura. Lakini mimi nasema ukweli kwa sababu ndio kazi iliyonileta hapa kusema ukweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niliulizwa hapa habari za madini. Kulikuwa na mjadala mrefu sana juu ya madini. Niseme tu kwamba, ziko hatua ambazo Serikali haikunyamaza. Kuna hatua ambazo tumekuwa tukichukua lakini matatizo bado yamebaki. Mimi niseme tu nitamwomba Waziri wa Nishati na Madini, aje kufafanua kwa undani zaidi mambo ambayo yanaendelea ndani ya Wizara yake. Lakini mimi naweza nikasema tu kwamba, Serikali inasikia haya mambo mnayosema na ushahidi nimeshautoa hapa leo asubuhi wakati nilipoanza kujibu nilisema hii habari ya kuzungumza hawa watu za kontrakta mmh, usichokoze nyuki bwana. Kwa hiyo, Waziri wa Nishati na Madini atakuja kueleza. Mimi ninachosema tu ni kwamba, yale ambayo yako ndani ya uwezo wa Serikali, Serikali itaendelea kuyatafakari na kuona nini kifanyike, yale ambayo hayako kwenye uwezo wa Serikali tutasaidiana mawazo na Wabunge tujue tufanye nini.

Lakini kuna moja ambalo kati ya hayo mengi tunayofanya mengine ni ya kitaalam sana, nisipoteze muda sana. Lakini moja tunalofanya ni ile hoja ya kusema mchanga unapelekwa ng'ambo hilo tayari

tunalifanyia kazi. Tumekuwa kwa miezi kadhaa sasa tunatafuta watu wa kufanya kitu kinachoitwa *assign and auditing*. Tumekwishafahamu wataalamu wanaoweza wakafanya kazi hiyo ya *assign and auditing*. Tukifikia maelewano na watu wenye utaalamu wa kuchekecha ule mchanga na kujua una nini, una *copper* asilimia ngapi, una *gold* asilimia ngapi, una *silver* asilimia ngapi na watu wengine wa kutusaidia ni *audit* ya huo mchanga wenyewe wa mtiririko wa fedha zile tunapouza bidhaa hizi na kuziingiza kwenye *score account* na kuzileta nchini na kadhalika. Hiyo kazi angalau tunataka tuifanye tuanze kujibu ile hoja ya mwaka 2002. Mchanga unapokwenda ni kitu gani tunapoteza na ni kitu gani tunapata. Hiyo iko mbioni lakini hatujasaini mikataba, maana nisije nikasema tumesaini, hatujasaini mikataba ila tumepata watu tunaendelea kuzungumza nao angalau tuanze na hilo. Sasa kuna mengine haya yaliyojitokeza hapa yale kwa kweli tutaendelea kuyatafakari kadri yanavyojitokeza.

Hili la *Tanzanite*, hoja kubwa sana kama wewe una kitu kama *Tanzanite*, ambacho duniani hakiko kwa nini unakifanya kama mchanga. Kwa muda mrefu *Tanzanite* na mchanga ni sawa sawa tu na peremende ni sawa sawa tu. Halafu wanaofaidika ni wengine sio watu wale ambao Mungu alishawabariki kwa kuwaletea kitu ambacho hakiko duniani. Kwa hiyo, hili tunalizungumza Serikali imeshaamua na kazi zinaendelea za kuzingira eneo lile la Mererani na kulifanya eneo la ulinzi mkali na usalama. *(Makofi)*

Wale wanaotoka Shinyanga ya zamani wanajua *Williamson Diamonds* ilikuwa inatumia sheria inayoitwa *The Diamond Protection Ordinance* ya wakoloni, ambayo ilikuwa inalinda almasi, huwezi kuingia pale Mwadui bila ya kuwa na vibali fulani na ushahidi fulani na huwezi kutoka na hivi. Eneo lile sasa litakuwa ni eneo lenye ulinzi mkali ili kusudi wanaochimba kule wabakie na mawe kule na mawe yale yauzwe kwa utaratibu utakaokuwa umewekwa na Serikali na sasa nimeongeza na wakate. Kwa sababu wewe ukiwa na *Tanzanite* jiwe la namna ile unaweka tu mfukoni unatembea nalo unakwenda kuuza huko vichochoroni. Maana yake ni sawa sawa na mtu aliyenunua chungwa au papai akaenda kuliuza huko mtaani. Hii ni kujidhalilisha tena wala hatuonyeshi shukrani kwa Mungu. Ile inakatwa unaweza ukapata mara tano au kumi ya bei yake duniani. Ukikata tu bei yake inakwenda juu, watu wanapata kazi, wanapata ujuzi. Hivi ndivyo mimi nilivyosema, kama mtu, kazi yangu ni kulinda raslimali za nchi hii.

Mimi sio Waziri wa Madini, lakini kazi yangu ni kulinda raslimali, nimesema isitoke bila kukatwa. Waziri wa Madini weka utaratibu, kusanya hiyo fedha, maneno kwisha. Mimi napata kodi yangu pale naendelea kuwapeni huduma. Ndiyo kazi yangu mimi. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Mambo hayo.

WAZIRI WA FEDHA: Kwa hiyo, tunaendelea tunaanza hivyo na kuna waliokuwa wanasema sasa wewe umeshaweka *stop*. Mimi sikuweka *stop* kama ya *switch* ya umeme. Nimesema tuanze sasa kukata. Lakini wasiposikiliza haya maneno, kuna siku nitasema *stop*. Mimi nimetoa tahadhari, maana naelewa siwezi kutamka leo, maana sikuwa nimewaandaa sasa nawaandaa. Kuna siku ndani ya miezi sita au kumi na mbili nitasema *stop*. Hujakata, hujauza nje, uza humu ndani. Hayo ndiyo mambo tunayofanya ya kulinda, mali tumepewa na Mungu jamani na fedha ipatikane humo. Mimi sipendi kabisa kuingia mfukoni kwa mtu kutafuta fedha ya kuendesha nchi hii. Iko nyingi Mungu ameshatupa mojawapo hiyo ya madini. *(Makofi)*

Sasa kuna watu wanasema kwa nini usihamie kwenye madini mengine, mimi mwaka huu nimekamata *Tanzanite* na mafuta. *Tanzanite* na mafuta ndiyo nimekamata kwenye Wizara ile, yale madini mengine yana utaratibu. Lakini sijamaliza najua haya mambo usiende kwa papara bwana. Papara ikitokea hapa tukashindwa kulipa mishahara watanigeuka tena watasema ooh wewe ndio uliyefanya mambo mabaya haya. Kwa hiyo, lazima niende kwa utaratibu. *(Makofi/Kicheko)*

Liko lingine la umeme. Ni kweli kabisa mimi kwenye ile Wizara nimebarikiwa, nina watu wanaoelewa uchumi. Mmojawapo hapa msaidizi wangu Dr. Limbu. Dr. Limbu nimempa *assignment* hiyo, tuambie wewe Dokta wa Uchumi jinsi uchumi wa nchi hiyo unaweza ukawa uchumi *competitive*. Nimempa hiyo kazi ana *Ph.D.* ni Dokta, mimi sina *Ph.D*. Yuko mbioni kweli kweli kuleta haya maneno. Yuko mbioni kabisa na Dr. Ngasongwa, tayari nimeshampa hiyo kazi na yeye ni mkereketwa kwa sababu viwanda vyake vitaumia sana bila jibu hilo. Tayari yeye ameshaleta mawazo nasubiri *CTI*, nasubiri ya *TANESCO* yenyewe na nasubiri ya wataalam. Halafu ukishafanya hivyo, ukishapata jibu hilo lazima

uamue *TANESCO* utafanya nao nini, kuna kitu kinaitwa *unbundling of TANESCO*. Je na hiyo ni *relevant* ama hapana na utafanya nini na gesi ya *Mnazi Bay* na gesi ya Songo Songo na *IPTL* na hata kama ungekwenda mbali zaidi na *Kiwira Coal?* Ni Miwanje kule Njombe na mitambo iliyokuweko kule zamani ambayo haijafufuliwa. Kuna mmoja Kikaletwa, kuna mmoja kule Tosamaganga kuna mwingine pale Mbalizi, Mbeya. Utafanya nini na mitambo mingine yote mingine inaitwa *ceramal?* Kwa hiyo, umeme wote ule. Ukusanye mawazo yote uamue basi *this is a right direction.*

Kwa hiyo, tumeshafungua macho, njia tumeiona, lakini hatujaamua kama ni mlango wa mbele au wa nyuma. Hii ndiyo kazi inayoendelea. Ningependa mniamini kwa sababu mimi nataka kuwa *a competative economy.* Tanzania hapa lazima iwe *a competitive economy*. Tusipokuwa *competitive economy* hatuwezi ku-*survive* hapa. Kwa hiyo, ni kazi kubwa lakini ndiyo tumeianza hivi na tunaendelea nayo. Mtu yeyote hapa mwenye mawazo, Mheshimiwa Mbunge yeyote hapa kama alivyonisaidia yule Mbunge wa Muheza, nitafurahi sana. Mbunge yeyote mwenye mawazo kesho asubuhi nitashukuru kuyapata kwa sababu tunayaweka kwenye mtambo tutayachambua na wataalam wengine tutaamua tu. Lakini ni kweli hakuna mtu anayefurahia hali ya sasa ya umeme ukilinganisha na uchumi tunaotaka tuwe nao huko mbele ya safari, hakuna.

Mheshimiwa Spika, mwisho mimi nimefurahi na nimefarijika sana, kusema kweli Bajeti hii na mlivyoitikia Waheshimiwa Wabunge na hasa *historically* pamoja na Kambi ya Ndugu hawa wa Upinzani. Nimewajibu vizuri kwa makusudi ili wasije wakasema niliwapuuza. Mheshimiwa Ngawaiya, nimeshamjibu kama hajatosheka basi ataitwa Roho Mtakatifu ndiyo ataweza kufanya hiyo kazi. Ndugu yangu Mheshimiwa Slaa, nimeshamjibu, ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, nimeshamjibu, wote wale nimeshawajibu wale wapya na wale wa zamani.

Waheshimiwa Wabunge, ninawaombeni kitu kimoja nipeni kura zenu kwenye Bajeti hii iwe ya kihistoria. Kambi ya Upinzani msipochukua nafasi hii sijui mtapata ipi tena. Angalau muonekane onekane kwamba, mpo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kwa sababu taratibu za Spika haziniruhusu naomba mkitoka nje mkumbuke kitu kimoja, haya yote tunayozungumza hapa ni shauri ya kazi kubwa ya Mheshimiwa Rais wetu aliyoifanya Kimataifa na Kitaifa na wasaidizi wake wakuu, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na sisi wote Serikalini na nyie wote Wabunge, tumeshirikiana mkitoka nje muimbe ule wimbo wa “Mpeni Raha Mkapa”.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati umefika wa kufanya uamuzi. Hoja ni kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004. Kila Mheshimiwa Mbunge, anayeafiki hoja hiyo atasema "ndiyo" wakati jina lake litakapotajwa na Katibu, ila Mbunge asiyeafiki atasema "siyo" wakati jina lake linatajwa.

Waheshimiwa Wabunge, huwa tuna utaratibu wa kupiga kengele ili kusudi Wabunge walioko nje waweze kuingia Ukumbini.

(Hapa kengele ilipigwa ili Wabunge waliopo nje waingie ndani ya Ukumbi wa Bunge wapige kura)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004

(Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga Kura zao za "Ndiyo" au "Hapana")

1. Mheshimiwa Frederick T. Sumaye - Ndiyo
2. Mheshimiwa William V. Lukuvi - Ndiyo

3. Mheshimiwa Anna M. Abdallah - Ndiyo
4. Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib - Ndiyo
5. Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete - Hakuwepo
6. Mheshimiwa Zakia H. Meghji - Ndiyo
7. Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Y. Ng'wandu - Ndiyo
8. Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo - Ndiyo
9. Mheshimiwa Daniel N. Yona - Hakuwepo
10. Mheshimiwa Harith B. Mwapachu - Ndiyo
11. Mheshimiwa Gideon A. Cheyo - Ndiyo
12. Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda - Ndiyo
13. Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya - Ndiyo
14. Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu - Ndiyo
15. Mheshimiwa Edward N. Lowassa - Ndiyo
16. Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Ndiyo
17. Mheshimiwa John P. Magufuli - Ndiyo
18. Mheshimiwa Basil P. Mramba - Ndiyo
19. Mheshimiwa Prof. Phille mon M. Sarungi - Ndiyo
20. Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri - Ndiyo
21. Mheshimiwa Charles N. Keenja - Ndiyo
22. Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya - Ndiyo
23. Mheshimiwa Joseph J. Mungai - Ndiyo
24. Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa - Ndiyo
25. Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngwilizi - Ndiyo
26. Mheshimiwa Balozi George C. Kahama - Ndiyo
27. Mheshimiwa Dr. Asha-Rose M. Migiro - Ndiyo
28. Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa - Ndiyo
29. Mheshimiwa Andrew J. Chenge - Ndiyo
30. Mheshimiwa Juma J. Akukweti - Ndiyo
31. Mheshimiwa Shamim P. Khan - Ndiyo
32. Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari - Ndiyo
33. Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu - Ndiyo
34. Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi - Ndiyo
35. Mheshimiwa Prof. Pius P. Mbawala - Ndiyo
36. Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir - Ndiyo
37. Mheshimiwa Bujiku K. Sakila - Hakuwepo
38. Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda - Ndiyo
39. Mheshimiwa Zabein M. Mhita - Ndiyo
40. Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati - Ndiyo
41. Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. R. Msabaha - Ndiyo
42. Mheshimiwa Dr. Hussein A. Mwinyi - Ndiyo
43. Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje - Ndiyo
44. Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu - Ndiyo
45. Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha - Ndiyo
46. Mheshimiwa Anthony M. Diallo - Ndiyo
47. Mheshimiwa Dr. Abdulkader A. M. Shareef - Ndiyo
48. Mheshimiwa Rita L. Mlaki - Ndiyo
49. Mheshimiwa Njelu E. M. Kasaka - Hakuwepo
50. Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo - Hakuwepo
51. Mheshimiwa William H. Shellukindo - Ndiyo
52. Mheshimiwa Dr. William F. Shija - Ndiyo
53. Mheshimiwa John S. Malecela - Ndiyo
54. Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa - Ndiyo
55. Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' - Ndiyo
56. Mheshimiwa Anne S. Makinda - Ndiyo
57. Mheshimiwa Sophia M. Simba - Ndiyo
58. Mheshimiwa Mgana I. Msindai - Ndiyo

59. Mheshimiwa Prof. Henry R. Mgombelo - Ndiyo
60. Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah - Ndiyo
61. Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah - Ndiyo
62. Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah - Ndiyo
63. Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz - Ndiyo
64. Mheshimiwa Bahati Ali Abeid - Ndiyo
65. Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud - Ndiyo
66. Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali - Ndiyo
67. Mheshimiwa Omar Mjaka Ali - Ndiyo
68. Mheshimiwa Salim Omar Ali - Ndiyo
69. Mheshimiwa Fatma Said Ali - Ndiyo
70. Mheshimiwa Khamis Salum Ali - Ndiyo
71. Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali - Ndiyo
72. Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally - Ndiyo
73. Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir - Ndiyo
74. Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir - Ndiyo
75. Mheshimiwa Rostam Aziz - Hakuwepo
76. Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar - Ndiyo
77. Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga - Ndiyo
78. Mheshimiwa Joel N. Bendera - Ndiyo
79. Mheshimiwa Lydia T. Boma - Hakuwepo
80. Mheshimiwa Zamda S. Bozzen - Ndiyo
81. Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian - Hakuwepo
82. Mheshimiwa Robert J. Buzuka - Hakuwepo
83. Mheshimiwa Margareth J. Bwana - Ndiyo
84. Mheshimiwa Kisyeri W. Chambiri - Hakuwepo
85. Mheshimiwa Isaac M. Cheyo - Ndiyo
86. Mheshimiwa Dr. Aaron D. Chiduo - Ndiyo
87. Mheshimiwa Diana M. Chilolo - Ndiyo
88. Mheshimiwa Samwel M. Chitalilo - Ndiyo
89. Mheshimiwa Anatory K. Choya - Ndiyo
90. Mheshimiwa Omar S. Chubi - Ndiyo
91. Mheshimiwa Paschal C. Degera - Ndiyo
92. Mheshimiwa Leonard N. Derefa - Ndiyo
93. Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria - Hakuwepo
94. Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail - Hakuwepo
95. Mheshimiwa Bakari Shamis Faki - Ndiyo
96. Mheshimiwa Abdallah Khamis Feruzi - Ndiyo
97. Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira - Ndiyo
98. Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama - Ndiyo
99. Mheshimiwa Dr. Lawrence M. Gama - Hakuwepo
100. Mheshimiwa Lephy Benjamin Gembe - Ndiyo
101. Mheshimiwa Jina Khatib Haji - Ndiyo
102. Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji - Ndiyo
103. Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji - Ndiyo
104. Mheshimiwa Edson M. Halinga - Ndiyo
105. Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan - Ndiyo
106. Mheshimiwa Salama Khamis Islam - Ndiyo
107. Mheshimiwa Yahya Kassim Issa - Ndiyo
108. Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa - Ndiyo
109. Mheshimiwa Ismail J. R. Iwvatta - Ndiyo
110. Mheshimiwa Mwadini Abbass Jecha - Ndiyo
111. Mheshimiwa Shoka Khamis Juma - Ndiyo
112. Mheshimiwa Yusuph Kombo Juma - Ndiyo
113. Mheshimiwa Ali Said Juma - Ndiyo
114. Mheshimiwa Peter Kabisa - Ndiyo

115. Mheshimiwa Charles H. Kagonji - Ndiyo
116. Mheshimiwa Janet B. Kahama - Ndiyo
117. Mheshimiwa Rhoda L. Kahatano - Ndiyo
118. Mheshimiwa Stephen M. Kahumbi - Ndiyo
119. Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala - Ndiyo
120. Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi - Ndiyo
121. Mheshimiwa Ally Amani Karavina - Ndiyo
122. Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira - Ndiyo
123. Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu - Hakuwepo
124. Mheshimiwa Stephen M. Kazi - Ndiyo
125. Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa - Ndiyo
126. Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalfan - Ndiyo
127. Mheshimiwa Zahor Juma Khamis - Ndiyo
128. Mheshimiwa Sharifa Mbarouk Khamis - Ndiyo
129. Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib - Ndiyo
130. Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib - Ndiyo
131. Mheshimiwa Juma S. Kidunda - Ndiyo
132. Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda - Ndiyo
133. Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo - Ndiyo
134. Mheshimiwa Anne K. Kilango - Hakuwepo
135. Mheshimiwa Estherina Kilasi - Ndiyo
136. Mheshimiwa Halima Omar Kimbau - Ndiyo
137. Mheshimiwa Paul P. Kimiti - Ndiyo
138. Mheshimiwa Emmanuel E. Kipole - Ndiyo
139. Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi - Ndiyo
140. Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga - Ndiyo
141. Mheshimiwa Grace S. Kiwelu - Hakuwepo
142. Mheshimiwa Stanley H. Kolimba - Ndiyo
143. Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo - Ndiyo
144. Mheshimiwa Parseko V. Kone - Hakuwepo
145. Mheshimiwa Khadija K. Kusaga - Ndiyo
146. Mheshimiwa William J. Kusila - Ndiyo
147. Mheshimiwa Lekule M. Laizer - Ndiyo
148. Mheshimiwa Dr. Masumbuko R. M. Lamwai - Hakuwepo
149. Mheshimiwa Benedict K. Losurutia - Ndiyo
150. Mheshimiwa George M. Lubeleje - Ndiyo
151. Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga - Ndiyo
152. Mheshimiwa Musa A. Lupatu - Ndiyo
153. Mheshimiwa Abdula S. Lutavi - Ndiyo
154. Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare - Ndiyo
155. Mheshimiwa Ernest G. Mabina - Ndiyo
156. Mheshimiwa Philip A. Magani - Ndiyo
157. Mheshimiwa Beatus R. Magayane - Ndiyo
158. Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe - Ndiyo
159. Mheshimiwa Aisha P. Magina - Ndiyo
160. Mheshimiwa Frank G. Magoba - Ndiyo
161. Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga - Ndiyo
162. Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame - Ndiyo
163. Mheshimiwa Paul N. Makolo - Ndiyo
164. Mheshimiwa Major Jesse J. Makundi - Ndiyo
165. Mheshimiwa Jackson M. Makwetta - Ndiyo
166. Mheshimiwa Benito W. Malangalila - Ndiyo
167. Mheshimiwa Philip S. Marmo - Ndiyo
168. Mheshimiwa Ibrahimu W. Marwa - Hakuwepo
169. Mheshimiwa Robert K. Mashala - Ndiyo
170. Mheshimiwa Janeth E. Mashele - Ndiyo

171. Mheshimiwa Haroub Said Masoud - Ndiyo
172. Mheshimiwa Dr. Chegeni R. Masunga - Ndiyo
173. Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid - Ndiyo
174. Mheshimiwa Halimenshi K. R. Mayonga - Ndiyo
175. Mheshimiwa Salome J. Mbatia - Ndiyo
176. Mheshimiwa Monica N. Mbega - Ndiyo
177. Mheshimiwa Prof. Simon M. Mbilinyi - Ndiyo
178. Mheshimiwa Talala B. Mbise - Ndiyo
179. Mheshimiwa Bakari M. Mbonde - Ndiyo
180. Mheshimiwa Freeman A. Mbowe - Hakuwepo
181. Mheshimiwa Mchande Salim Mchande - Ndiyo
182. Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba - Ndiyo
183. Mheshimiwa Benard K. Membe - Ndiyo
184. Mheshimiwa Mariam S. Mfaki - Ndiyo
185. Mheshimiwa Muttamwega B. Mgaywa - Hakuwepo
186. Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni - Ndiyo
187. Mheshimiwa Jenista J. Mhagama - Ndiyo
188. Mheshimiwa Prof. Juma M. Mikidadi - Ndiyo
189. Mheshimiwa Mohamed H. Missanga - Ndiyo
190. Mheshimiwa Margareth A. Mkanga - Ndiyo
191. Mheshimiwa Adelastela E. Mkilindi - Ndiyo
192. Mheshimiwa Nimrod E. Mkono - Ndiyo
193. Mheshimiwa George F. Mlawa - Ndiyo
194. Mheshimiwa Oscar T. Mloka - Ndiyo
195. Mheshimiwa Raphael Mlolwa - Ndiyo
196. Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o - Ndiyo
197. Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed - Ndiyo
198. Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed - Ndiyo
199. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Ndiyo
200. Mheshimiwa Sumri Abdallah Salum Mohamed - Ndiyo
201. Mheshimiwa Elisa D. Mollel - Ndiyo
202. Mheshimiwa Balozi Getrude I. Mongella - Hakuwepo
203. Mheshimiwa Alhaji Ahamadi H. Mpeme - Hakuwepo
204. Mheshimiwa Benson M. Mpesya - Ndiyo
205. Mheshimiwa Kilontsi M. M. Mporogomyi - Hakuwepo
206. Mheshimiwa Felix C. Mrema - Ndiyo
207. Mheshimiwa Raynald A. Mrope - Ndiyo
208. Mheshimiwa Ruth B. Msafiri - Hakuwepo
209. Mheshimiwa Dr. James A. Msekela - Ndiyo
210. Mheshimiwa Herbert J. Mntangi - Ndiyo
211. Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte - Hakuwepo
212. Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji - Ndiyo
213. Mheshimiwa James P. Musalika - Ndiyo
214. Mheshimiwa Ali Machano Mussa - Ndiyo
215. Mheshimiwa Ali Sheha Mussa - Ndiyo
216. Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa - Ndiyo
217. Mheshimiwa Frank Michael Mussati - Ndiyo
218. Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi - Ndiyo
219. Mheshimiwa Prof. Daimon M. Mwaga - Ndiyo
220. Mheshimiwa John L. Mwakipesile - Ndiyo
221. Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa - Hakuwepo
222. Mheshimiwa Yete S. Mwalyego - Ndiyo
223. Mheshimiwa Venance M. Mwamoto - Ndiyo
224. Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro - Ndiyo
225. Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga - Ndiyo
226. Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila - Ndiyo

227. Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri - Ndiyo
228. Mheshimiwa Omar M. Mwenda - Ndiyo
229. Mheshimiwa Chrisant M. Mzindakaya - Hakuwepo
230. Mheshimiwa Damas P. Nakei - Ndiyo
231. Mheshimiwa Abdilahi O. Namkulala - Ndiyo
232. Mheshimiwa Benardine R. Ndaboine - Ndiyo
233. Mheshimiwa Edward N. Ndeka - Ndiyo
234. Mheshimiwa Job Yustino Ndugai - Ndiyo
235. Mheshimiwa Thomas Ngawaiya - Ndiyo
236. Mheshimiwa Asha A. Ngede - Ndiyo
237. Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru - Ndiyo
238. Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye - Ndiyo
239. Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi - Ndiyo
240. Mheshimiwa Jumanne Hamisi Nguli - Ndiyo
241. Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura - Ndiyo
242. Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga - Ndiyo
243. Mheshimiwa Said J. Nkumba - Ndiyo
244. Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya - Ndiyo
245. Mheshimiwa Paul E. Ntwina - Ndiyo
246. Mheshimiwa Tembe K. Nyaburi - Ndiyo
247. Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu - Ndiyo
248. Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami - Ndiyo
249. Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa - Ndiyo
250. Mheshimiwa Rosemary H. K. Nyerere - Hakuwepo
251. Mheshimiwa Thomas S. Nyimbo - Ndiyo
252. Mheshimiwa Mathew Taki Ole-Timan - Ndiyo
253. Mheshimiwa Omar Juma Omar - Ndiyo
254. Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar - Ndiyo
255. Mheshimiwa Karim Said Othman - Ndiyo
256. Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu - Ndiyo
257. Mheshimiwa Semindu K. Pawa - Ndiyo
258. Mheshimiwa Mwaka Abrahman Ramadhani - Ndiyo
259. Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba - Ndiyo
260. Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq - Ndiyo
261. Mheshimiwa Hashim A. Z. Saggaf - Ndiyo
262. Mheshimiwa Mohamed Ali Said - Ndiyo
263. Mheshimiwa Khamis Ali Saleh - Ndiyo
264. Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh - Ndiyo
265. Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim - Ndiyo
266. Mheshimiwa Issa Mohamed Salim - Ndiyo
267. Mheshimiwa Ali Said Salim - Ndiyo
268. Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili - Hakuwepo
269. Mheshimiwa Lucas L. Selelii - Ndiyo
270. Mheshimiwa Haji Juma Sereweji - Ndiyo
271. Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame - Ndiyo
272. Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah - Ndiyo
273. Mheshimiwa Leonard M. Shango - Hakuwepo
274. Mheshimiwa Henry D. Shekiffu - Ndiyo
275. Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti - Ndiyo
276. Mheshimiwa Iddi M. Simba - Ndiyo
277. Mheshimiwa John E. Singo - Ndiyo
278. Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa - Ndiyo
279. Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud - Ndiyo
280. Mheshimiwa Esha H. Stima - Ndiyo
281. Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman - Ndiyo
282. Mheshimiwa Khalid S. Suru - Ndiyo

283. Mheshimiwa Aridi M. Uledi - Ndiyo
284. Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha - Hakuwepo
285. Mheshimiwa Maria D. Watondoha - Hakuwepo
286. Mheshimiwa Christopher S. Wegga - Ndiyo
287. Mheshimiwa Martha M. Wejja - Ndiyo
288. Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir - Ndiyo

(Hapa Ukumbi uliingiwa na nderemo na chereko Wabunge wakishangilia baada ya Wabunge wote wakiwemo wa Upinzani kupiga kura za "Ndiyo" ili kupitisha Bajeti ya Serikali)

MATOKEO YA KURA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, matokeo ya upigaji kura ni kama ifuatavyo: Idadi kamili ya Wabunge ni 292, lakini wanne wamesimamishwa kazi ya Ubunge. Kati ya Wabunge 288 waliotakiwa kupiga kura, 33 hawakuwepo Bungeni, Wabunge 255 waliobaki wote wamepiga kura za ndiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, natangaza kwamba, Bunge limepitisha Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2003/2004 kwa kiwango kinachotakiwa. *(Makofi)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004 yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kazi zilizopangwa kwa kikao cha leo tarehe 20 Juni, 2003, zimekamilika. Kwa hiyo, kabla sijaahirisha Bunge niwakumbushe kuhusu Semina ya kesho. Ratiba zimekwishagawiwa na tutafuata kama zilivyopangwa. Vile vile, kuna ratiba ya burudani kwa kesho ambayo pia imekwishagawiwa, nayo tutaifuata kama ilivyopangwa.

Baada ya maelezo hayo, sasa naahirisha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu Saa Tatu Asubuhi.

(Saa 12.28 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu Tarehe 23 Juni, 2003 Saa Tatu Asubuhi)